# Majibu kwa Maswali ya Kawaida
## Juu ya *Ushirika wa Mtu na Mungu*

### *Ushirika wa Mtu na Mungu* ni Nini?

*Ushirika wa Mtu na Mungu ni mchakato wa mafunzo ya uanafunzi wa majuma kumi na tano am*bayo yanakuunganisha moja kwa moja na Mungu:

***Ni Njia*** inayomwongoza mtu kumjua Yesu binafsi,

***Ni Mtindo wa maisha*** wa kutembea kila siku katika ushirika wa karibu na Yeye,

***Ni Nyenzo*** kwa ajili ya kuwafanya watu kuwa wanafunzi na kuzalisha walimu wa wanafunzi.

### Jinsi gani mafunzo ya *Ushirika wa Mtu na Mungu* yanafanya kazi?

**Mpango Hasili ni:**

- Kukutana mara moja kwa juma kwa muda wa majuma kumi na tano mfululizo.
    - Kwa nini yawe majuma kumi na tano?
        - Wanasema inachukua majuma kumi na tano kujenga mwelekeo katika maisha yetu au kuanzisha mtindo wa maisha.
    - Kwa nini mfululizo wa majuma?
        - Ili kudumisha kasi au mwendo kasi.
    - Ruhusu masaa mawili kwa kila kipindi.
        - Kwa nini masaa mawili na siyo chini ya masaa hayo?
            - Kwa kawaida inachukua masaa mawili kukamilisha masomo na kumpa kila mtu fursa ya kushiriki na kujifunza jinsi ya kufanya mambo tunayowahamasisha kuyafanya.
    - Mnakutana katika vikundi vidogovidogo na kiongozi na wanafunzi wasiwe zaidi ya sita.

## Inakuwaje kama hutaweza kuwa na mazingira mazuri yaliyoelezwa hapo juu?

Chukuliana na mazingira, lakini hakikisha kwamba unakamilisha masomo yote na kwamba wanafunzi wako wanaelewa jinsi ya kuzitumia kweli hizo.

## Je, ni baadhi ya mifano gani iliyo chini ya uhalisi wa mazingira ambapo umewapitisha watu katika masomo ya *Ushirika wa Mtu na Mungu?*

Kama mara mbili tuliweza kuwafundisha zaidi ya watu sabini katika vikundi vidogovidogo kwa kipindi cha zaidi ya majuma nane kwa kukutana na kila kikundi mara mbili kwa juma.

Wakati fulani, katika juma ambalo tuliliita "J-term" katika seminari, tulilipitisha kundi katika mafunzo ya *Ushirika wa Mtu na Mungu*, tukikamilisha masaa yetu yote thelathini katika kipindi cha siku tano.

Ikiwa una kipindi cha majuma nane au kumi na mbili tu ambacho utafundisha, tunapendekeza kwamba uagize mwongozo wa kiongozi wa vipindi nane au kumi na mbili. Itakuwa rahisi zaidi kwako. Tafadhali zingatia kwamba kwa vipindi hivi vya muda mfupi, ni muhimu sana kwako kuwahamasisha wanafunzi wako kujiwekea nadhiri ya keundelea kuzitendea kazi kanuni walizojifunza katika mafunzo ya *Ushirika wa Mtu na Mungu* kwa jumla ya majuma kumi na tano au mpaka kanuni zimekuwa sehemu ya kawaida katika maisha yao.

***Ufunguo*—ni kuizoea hali bila kuutoa mhanga muda unaotakiwa kwa ajili ya Mungu ili kuzalisha wanafunzi na walimu wa wanafunzi imara kupitia kwako.**

***Lakini kumbuka*—uhalisi ni kukutana kwa majuma kumi na tano mfululizo, kwa masaa mawili kila juma.**

## Je, inakuwaje ikiwa watu ninaowafundisha hawafanyi wanafunzi?

Endelea kuwaombea na kuwatia moyo wanafunzi wako waweze kufanya wanafunzi, lakini kumbuka kwamba *tunakwenda katika nguvu na kwa uongozi wa Roho Mtakatifu, na matokeo tunamwachia Mungu*. Yeye ndiye anayepaswa kutia nuru ufahamu wao na kuwasadikisha mioyoni mwao ili waweze kufanya wanafunzi.

Uwe mwaminifu katika agizo na mwito wa Mungu katika maisha yako wa kuwafanya wanafunzi, na kwa wakati uliokubalika wewe mwenyewe utayaona matokeo.

# YALIYOMO

Majibu kwa Maswali ya Kawaida ---------------------------------- i
Yaliyomo --------------------------------------------------------------iii
Tabaruki ---------------------------------------------------------------v
Utangulizi -------------------------------------------------------------1
Vidokezo katika Kuongoza Vikundi vya
*Ushirika wa mtu na Mungu* ------------------------------------------3
Picha Kubwa ya Uanafunzi------------------------------------------5
Changamoto—Kuyaacha Matunda Yanayodumu ---------------- 11
Kipindi cha 1 ------------------------------------------------------ 15
Kipindi cha 2 ------------------------------------------------------ 31
Kipindi cha 3 ------------------------------------------------------ 41
Kipindi cha 4 ------------------------------------------------------ 51
Kipindi cha 5 ------------------------------------------------------ 61
Kipindi cha 6 ------------------------------------------------------ 77
Kipindi cha 7 ------------------------------------------------------ 93
Kipindi cha 8 -----------------------------------------------------103
Kipindi cha 9 -----------------------------------------------------115
Kipindi cha 10---------------------------------------------------135
Kipindi cha 11 ---------------------------------------------------147
Kipindi cha 12---------------------------------------------------157
Kipindi cha 13---------------------------------------------------165
Kipindi cha 14---------------------------------------------------177
Kipindi cha 15---------------------------------------------------189

# TABARUKI

Mafunzo ya *Ushirika wa Mtu na Mungu* tumeyatabaruki kwa wazazi wetu, watoto, wajukuu na vizazi vijavyo vya familia yetu, na kwa wanafunzi wote wenye utayari wa kuwekeza maisha yao katika kuwafanya wanafunzi ambao nao watafanya wanafunzi.

Kutokana na ujumbe wetu katika mwongozo huu wa kiongozi na kitabu cha maelezo (notebook) cha mafunzo ya *Ushirika wa Mtu na Mungu*, utaweza kuona kanuni nyingi ambazo Mungu atazitumia kukubariki. Zitafakari na kuzitumia katika maisha yako. Tunakuhamasisha kuenenda katika maisha yako macho yako yakimtazama Yesu, jiachilie katika udhibiti wa Roho Mtakatifu. Mruhusu Yeye awe msimamizi katika maisha yako kila siku. Katika safari yako, kila siku yajaze maisha yako kwa Neno la Mungu, na maombi; na mfanye Yesu awe kitovu cha maisha yako ambaye kwa Yeye vitu vyote vinamzunguka. Ruhusu kusudi lako la dhati liwe kumjua Yesu kwa kina, kwa undani na kibinfasi. Azimia kuijua Biblia na mara utagundua kwamba yenyewe ndio inakumudu wewe. Wekeza maisha yako katika hilo ambalo ni la milele. Mjue Mungu, kwa kuwa Yeye ni wa milele. Yajaze maisha yako kwa Neno la Mungu, Biblia, kwa kuwa ni ya milele. Fanya wanafunzi kwa kuwaleta watu kwa Kristo na kuwafundisha kutembea na Mungu, kwa kuwa nafsi za wanaume na wanawake, wavulana na wasichana ni za milele. Zifanyie mazoezi kanuni hizi, na utakuwa kama kioo ambapo kupitia hicho Yesu atajiakisi Mwenyewe kwa kila mtu unayemjua. Kadri unavyoenenda katika maisha, fanya wanafunzi. Hii ndiyo njia kuu unayoweza kuonyesha upendo wako kwa Yesu na kwa wengine. Yesu mwenyewe ndiye kielelezo chetu. Kamwe usikate tamaa! Yesu ndiye tumaini letu! Yeye ndiye mwenye nguvu ya kuvitawala vitu vyote! Yeye ni mwaminifu, na Atarudi tena!

Katika Yeye,

Jerry na Marilyn Fine

# UTANGULIZI

Tunakuhamasisha kuyafanya mafunzo ya Ushirika wa mtu na Mungu kuwa yako mwenyewe. Mchungaji niliyemfundisha alisema, "Huko nyuma niliyazungumzia mafunzo ya *Ushirika wa Mtu na Mungu* kama ya Jerry na Marilyn, lakini sasa ninayaona kuwa ya kwangu."

Tafadhali uwe huru kutumia vielelezo na hadithi katika jumbe za mwandishi wakati unapowafanya wanafunzi, lakini tunataka pia uwe huru kubadilisha vielelezo na hadithi zako mwenyewe. Kwa hakika, tunakuhamasisha kufanya hivyo. Pale unapoanza kushirikisha vielelezo vyako mwenyewe unapowafundisha wengine; mafunzo ya *Ushirika wa Mtu na Mungu* yatakuwa ya kwako zaidi.

Ni maombi yetu kwako kwamba pale unapomtumaini Mungu na, kama tendo la uaminifu kwa Yesu, fanyia mazoezi na kuwasilisha kanuni zote za kibiblia zilizomo katika mafunzo ya *Ushirika wa Mtu na Mungu*.

Mungu akubariki "*Unapokwenda na kuwafanya wanafunzi.*"

# VIDOKEZO KWA AJILI YA KUONGOZA VIKUNDI VYA

## *Ushirika wa mtu na Mungu*

Vidokezo vifuatavyo ni mambo ambayo tumejifunza kwa zaidi ya miaka thelathini ya kuongoza vikundi hivi vidogovidogo:

1. Mwanafunzi mmoja pekee yake au hadi wanafunzi sita kufundishwa katika kikundi kimoja hilo linakubalika. **Wanafunzi wanne wanafundishwa katika kikundi kimoja hilo linaweza kuwa nzuri kwa sababu:**
   - Kuna muda wa kutosha kwa ajili ya kila mmoja kushiriki katika darasa.
   - Wanakikundi wanajifunza na wanahamasishana wao kwa wao.
   - Wana maombi wenza kwa ajili ya wanafunzi wanaweza kuwa washiriki wengine wa darasa.
2. Mwanzoni tulipoanza kuwafanya wanafunzi, tulikutana na mwanafunzi mmoja tu kwa wakati mmoja. Faida moja katika hili ilikuwa kwamba tungeweza kuwajumuisha wanafunzi katika maisha na huduma yetu binafsi. Kumbuka kwamba mtindo wa maisha wa mafunzo ya *Ushirika wa mtu na Mungu* unashikwa na kufundishwa pia.

3. Ni busara kwa wanaume kuwafundisha wanaume na wanawake kuwafundisha wanawake. Kama itakuwa kuna ulazima kwa mwanamme au mwanamke kufundisha watu wa jinsia tofauti na yake, hakikisha inafanyika katika kikundi. Kamwe usikutane kumfundisha mtu mmoja tu wa jinsia tofauti na yako isipokuwa ninyi ni mme na mke.

4. Ikiwezekana, mkutane kwenye nyumba isiyo na kelele au usumbufu au hata kama utakuwepo uwe kidogo kadri iwezekanavyo. Nyumba yenye hali ya utulivu, mazingira yenye utulivu husaidia sana.

5. Ruhusu kama masaa mawili kwa kila kipindi, japokuwa baadhi ya vipindi vinaweza visihitaji muda huo wote.

6. Ikiwa kutakuwa na viburudisho, viwe vya kawaida na visivyochukua muda. Kahawa, chai, au vinywaji baridi vinaweza kufaa.

7. Fanyia mazoezi kile unachofundisha. Mungu na wanafunzi wanakutazama wewe.

8. Usikose amani au uvumilivu ukiona kuna vipindi vya ukimya pale unapouliza maswali. Waache wanafunzi wajue kwamba ni hali ya kawaida kufikiri juu ya mwitikio au majibu yao. Unaweza kuhitaji kulipangilia upya swali lako.

9. Fundisha kwa unyenyekevu. Ruhusu wanafunzi wajue kwamba wewe pia uko katika safari hii ya ukuaji wa kiroho.

10. Kusudi letu katika kufundisha ni kuzalisha wanafunzi wa kweli ambao watawekeza maisha yao katika kuwafanya wanafunzi. Jambo hili linaweza kufikiwa kikamilifu kwa kuyafanya makundi yako kuwa madogo—kila kikundi watu sita au pungufu.

# Picha Kubwa ya kufanya Wanafunzi

*Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia, "Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyo waamuru ninyi..."* (Mathayo 28:18-20 SUV).

**Mathayo 28:18-20 siyo agizo kuu. Ni Agizo Kuu, na ni Agizo *letu* Kuu**. Kila mwamini wa kweli anakiwa kuhusika katika jukumu la kujihusisha katika vipengele vitano vya kufanya wanafunzi:

- **Enendeni**—Hatupaswi kukaa nyuma na kimya tukisubiri watu kuja kwetu. Tunapaswa kuwaendea na tunapaswa kwenda tukiwa na kusudi.
- **Hubiri au Fanya Uinjilisti**—Ni akina nani walikuwa wakibatizwa na wanafunzi wa Yesu? Waamini wapya waliowaongoza kwa Kristo (wale waliowahubiri).
- **Kubatiza**—Waamini hawa wapya walitakiwa kujitambulisha kwa haraka kama wafuasi watiifu wa Yesu kwa kubatizwa.
- **Kufundisha**—Waamini hawa wapya walitakiwa kufundishwa jinsi ya kumjua Mungu, kumpenda Mungu, kumtumikia Mungu na kuenenda na Mungu katika utii halisi.
- **Kuongeza au Kuzidisha**—Wanafunzi hawa walitakiwa kutumwa katika kazi ya umisheni wakiwa na ushawishi na ufahamu wa kuzalisha kiroho siyo tu wanafunzi bali walimu wa wanafunzi. Jambo hili ni kweli kwa kila mwamini wa kweli katika vizazi vyote.

## Wahusika—Yesu na Wanafunzi wa kweli

**Uanafunzi wa kweli ni nini?**

- Kwa nini tunatumia usemi huu ***mwanafunzi wa kweli***? Watu waliomfuata Yesu walikuwa wakiitwa wanafunzi. Katika Yohana 6:66, imeandikwa kwamba, *"Kuanzia wakati huu wengi miongoni mwa wanafunzi wake wakarejea nyuma, wasiandamane naye tena."* Ukweli kwamba hawakufuatana Naye tena ulikuwa ni uthibitisho kwamba hawakuwa wanafunzi wa kweli (1Yohana 2:19).

- **Mwanafunzi wa Kweli** anapaswa kuwa na shauku kubwa ili kumruhusu Roho kutawala maisha yake na kufanana na Yesu zaidi: *"...Tuweze kuwa vioo ambavyo vinabadilishwa na kufanana na utukufu wa Bwana. Na kama vile Roho wa Bwana*

*atendavyo ndani yetu, tufanane Naye zaidi"* (2 Wakorintho 3:18 3:18 LIV).

- Maisha ya **mwanafunzi wa kweli** ni maisha yenye uzima, ambayo yanamaanisha ni maisha yanayobadilika mara kwa mara (wakati wote). Aidha tunasonga mbele, tukiendelea kukua na kukomaa kiroho, au tunarudi nyuma, mbali na Mungu.

**Katika Uanafunzi wa Kweli . . .**

- **Yesu ni mchezaji bora (mhusika mkuu), na sisi ni wachezaji wa kawaida tu.** Ni yeye ndiye anayembadilisha mtu asiyeamini kuwa mwanafunzi na kisha kumbadilisha mwanafunzi mpya kuwa mwalimu wa wanafunzi. Bado anatutuma sisi *"Kwenda kuwafanya wanafunzi,"* ambapo kwa maana rahisi; ni kushirikiana pamoja naye na kuwa Mabalozi Wake (2 Wakorintho 5:20)—Kupitia wanafunzi hao Yeye anaweza kueneza ujumbe Wake kuufikia ulimwengu kwa upendo Wake.
- **Yesu, mzalishaji pekee aliye mkamilifu wa walimu wa wanafunzi, ni mwalimu na kielelezo chetu.** Tunajifunza siyo tu kutokana na kile Alichosema lakini kutokana na kile alichokifanya. Yesu alituagiza sisi kuwafanya wanafunzi (Mathayo 28:19). Japokuwa hakutumia maneno halisi "zalisha walimu wa wanafunzi," hapa kuna mambo matatu ambayo yanawasilisha kweli hii:
    1. Yesu alifanyika mzalishaji wa walimu wa wanafunzi pale wanafunzi wake walipoanza kuwafanya wengine kuwa wanafunzi.
    2. Mathayo 28:20 inazungumzia kizazi kijacho cha wanafunzi wapya. Yesu alisema, *"na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru,"* mara tu baada ya kusema, *"Enendeni makawafanye wanafunzi"* (Mathayo 28:19). Kwa hiyo, kila mwamini mpya anapaswa kufundishwa kutii amri ya "kwenda na kuwafanya wanafunzi". Yohana 8:31 AMP inawaelezea wanafunzi wa kweli kuwa ni wale ambao wanamwamini Yeye, wanaokaa katika Neno lake, na kutii mafundisho yake. **Pale tunapokuwa watii katika kuwafanya wanafunzi na wale waliofundishwa kuwa watii kufanya wanafunzi, tunafanyika wazalishaji wa walimu wa wanafunzi.**
    3. Paulo alielewa kanuni hii ya kuzalisha walimu wa wanafunzi. Matokeo yake, alimwelekeza Timotheo, *"Na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uyakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine"* (2 Timotheo 2:2 NIV1984).

## Shauku—Kufanya Wanafunzi

**Kwa nini tufanye wanafunzi?**

- Yesu alituamuru kuwafanya wanafunzi (Mathayo 28:18-20).

- **Watu wasio na Yesu hawana tumaini**, *"...mlikuwa hamna Kristo ...mmefarakana na jamii ya Israeli ...mlikuwa hamna Mungu na hamna tumaini"* (Efeso 2:12 NLT).

## Mchakato—Uanafunzi

**Neno *Mwanafunzi* halinamwelezei tu mtu bali ni mchakato. Yesu ametualika na kutuelekeza sisi pia kuhusika katika mchakato huu.**

- Mwanafunzi ni matokeo ya mchakato wa uanafunzi, ambao hatimaye unategemea nguvu ya Mungu inayobadilisha. Tunaposema "tumemfundisha" mtu fulani, tunamaanisha kwamba Mungu ameturuhusu kuhusika katika mchakato.

- Tunapaswa kuendelea kukua, kukomaa, na kufundishwa vizuri zaidi ili kwamba tuweze kuwa nyenzo zinazofaa kutumika zaidi mikononi mwa Mungu (Warumi 12:1-2), … *"tayari kwa lolote, imara katika tabia, wakamilifu na watimilifu bila kupungukiwa neno"* (Yakobo 1:4 LIV).

- • Paulo ametuwekea mfano wa kutokata tamaa kamwe, bali wakati wote kuzidi kuyachuchumilia na kuzidi kuwa vile Mungu alitaka yeye awe. *"...Bado sijawa vile nilivyopaswa kuwa bali ninatumia nguvu zangu zote kulibeba jambo hili moja. Nikiyasahau yaliyo nyuma, nikiyachuchumilia yaliyo mbele; nakaza mwendo kuufikia mwisho wa mashindano na kupokea thawabu ambayo Mungu anatuitia sisi mbinunguni kwa sababu ya kile Kristo Yesu alichokifanya kwa ajili yetu"* (Wafilipi 3:13-14 LIV).

**Katika mchakato wa uanafunzi/kufundisha, *wajibu wangu* ni nini; na nini *wajibu wa Roho Mtakatifu?***

- ***Wajibu wangu ni*:**

- Kupatikana au kuwepo—*"Njooni kwangu [Yesu]" na "mjifunze kwangu [Yesu]"* (Mathayo 11:28-29 AMP).

- Kushi chini ya udhibiti wa Mungu—*"... jitoeni wenyewe kwa Mungu"* (Warumi 6:13). Mruhusu Yeye kuwa msimamizi katika maisha yako leo.

- Kukaa ndani ya Yesu (Yohana 15:4).

- Kuishi katika Neno lake na kutii mafundisho yake (Yohana 8:31 AMP).

- *"Furahini siku zote, ombeni bila kukoma, mshukuruni Mungu kwa kila jambo..."* (1 Wathesalonike 5:16-18 ESV).

- Ujikane mwenyewe, uchukue msalaba wako kila siku, na kumfuata Yesu (Luka 9:23).

- Uwe balozi wa Yesu (2 Wakorintho 5:20). Uwe shahidi kwa ajili Yake [Yesu] (Mdo 1:8).

- Nenda kwa UWEZO au NGUVU za Yesu ili kawafanya wanafunzi—Anatutuma katika Uwezo Wake (Mathayo 28:18-20).

- Chagua MPANGO wa Yesu—unapoenenda, shirikisha ujumbe Wake (Mathayo 28:19-20).

- Simama katika AHADI za Yesu—*"Niko pamoja nanyi"* (Mathayo 28:20).

- Kimbia mbio zenye nidhamu (1 Wakorinto 9:24-27 JBP).

    - Weka lengo lako ili kushinda.

    - Jifunze kwa Bidii.

    - Uwe thabiti.

    - Jizoeze nidhamu na kujikana.

- ***Wajibu wa Roho Mtakatifu ni*:**

    - Huutia nuru ufahamu au akili (1 Wakorintho 2:12-14).

    - Huusadikisha moyo (Yohana 16:8-11).

- Hukaa ndani yetu (Warumi 8:11).
- Hutufundisha sisi (Yohana 14:26).
- Hutufariji sisi (Yohana 14:16).
- Hutusaidia sisi (Warumi 8:26).
- Hutuongoza (Yohana 16:13).
- Hutuwezesha (Mika 3:8).
- Huzaa matunda ndani yetu (Wagalatia 5:22-23).

## Matokeo—Walimu wa wanafunzi na Wazalishaji wa walimu wa wanafunzi

**Jinsi gani watu au makanisa yanaweza kuwa wafanyaji wa wanafunzi au wazalishaji wa walimu wa wanafunzi?**

- **Angalia mfano—**Yesu.
- **Kamata maono**—yaliyotolewa na Yesu.
- **Weka Lengo**—ili kuwekeza maisha yao katika kufanya wanafunzi ambao wataendelea kujizalisha wenyewe kiroho ndani ya wanafunzi ambao watawafanya wanafunzi.
- **Fuata mfano**—Yesu.
- **Rudia mchakato.**
    - Miaka kadhaa iliyopita nilisoma kijitabu chenye kichwa cha habari "Jinsi gani Yesu aliwafundisha Viongozi" kilichoandikwa na Dr. W. Maxfield Garrott, mmishenari aliyekwenda Japan. Sijawahi kusahau kauli yake aliyomalizia kuhusiana na kufundisha viongozi, kauli ambayo pia ina ukweli juu ya kuwafanya wanafunzi. Alisema, **"Ili kupata matokeo yatakayolinganishwa na Yake (Yesu), unachopaswa kufanya ni kuwa kama Yesu na kuishi karibu kabisa na watu wachache ili wao waweza kuiona sura au taswira Yake kupitia wewe. Rahisi sana."**

**Unaweza kuwa**

**yule MWANAFUNZI WA KWELI,**

***MWALIMU WA WANAFUNZI*,**

***na MZALISHAJI WA WALIMU WA WANAFUNZI***

**Mungu anakutaka wewe uwe hivyo!**

**Ni kuchukua hatua inayofuata tu.**

# Changamoto ambayo Mungu Ametupatia—Kuyaacha Matunda Yanayodumu

Moja ya changamoto kubwa katika Biblia ni pale **Yesu anapotukumbusha kwamba Alituchagua na kutuweka ili tuzae na kuacha matunda yanayodumu.**

> *Si ninyi mlionichagua mimi, bali ni mimi niliyewachagua ninyi; nami nikawaweka mwende mkazae matunda; na matunda yenu yapte kukaa* (Yohana 15:16 NIV).

**Je unaacha matunda yanayodumu?**

Jinsi gani tunayaacha matunda—matunda ambayo yatadumu milele?

Yesu alitoa muhtasari wa jinsi ya kuacha matunda yanayodumu pale aliposema, "***Enendeni mkawafanye wanafunzi"*** (Mathayo 28:19 NIV). Kuwafanya wanafunzi kunahusisha kwenda, kuhubiri, kubatiza, kufundisha na kisha kuwatuma wanafunzi wapya nje ili kuongeza (kufanya wanafunzi).

Uanfunzi ni jinsi unavyoizidisha huduma ambayo Mungu amekupatia.

Kama tungekufa miaka thelathini na mbili iliyopita, kungekuwa na watu wachache sana huko mbinguni kama matokeo ya huduma yetu kwa sababu japokuwa tulikuwa tunashuhudia na kuwashirikisha wengine habari za Kristo, tulikuwa hatufundishi. Tungekuwa tumeacha matunda kidogo sana yanayodumu. Katika miaka thelathini na mbili tumeweza kuwekeza maisha yetu siyo tu katika kushirikisha habari za Kristo kwa waliopotea bali katika kufanya wanafunzi na kuzalisha walimu wa wanafunzi. Sasa wale tuliowafundisha wamesambaa ulimwengu mzima, wakifanya wanafunzi na kuacha matunda yanayodumu. Pale tutakapokufa, huduma ambayo Mungu ametupa itakuwa ikiongezeka mwaka baada ya mwaka kadri wale tuliowafundisha wanavyoendelea kuwafundisha wengine. *Tuliyaona yale aliyoyafanya Yesu wakati alipokuwa hapa duniani nasi tukaamua kuwekeza maisha yetu katika jambo kama hilo: tukiweka kipaumbele katika kuwafanya wanafunzi.*

Hapa kuna mpango ambao utakufanya uwe na ufanisi katika kuyaacha ***matunda yatakayodumu*** lakini ***unapaswa kuwa na utayari kuufanyia kazi mpango.***

> ***Fundisha angalau kundi moja la wanafunzi kwa mwaka*** —Kila mwaka pata kundi la watu wawili hadi sita litakalopitia mafunzo ya Ushirika wa Mtu na Mungu. Kutaneni mara moja kwa juma kwa majuma kumi na tano, na ruhusu masaa mawili kwa kila kipindi.
>
> ***Endeleeni kukutana mara moja kwa mwezi kwa miezi saba zaidi***—Baada ya kumaliza mafunzo ya *Ushirika wa mtu na Mungu* na kikundi, kutaneni mara moja kwa mwezi kwa miezi saba zaidi ili kutiana moyo na kuwajibishana ninyi kwa ninyi kwa ajili ya kuendelea kuzifanyia mazoezi kanuni mlizojifunza katika mafunzo ya *Ushirika wa Mtu na Mungu.*

> ***Ongeza*****—**Hamasisha na kuwatuma wanafunzi wako **kuacha matunda yanayodumu au yanayokaa** kwa kutii amri ya "Kwenda na kuwafanya wanafunzi" (Mathayo 28:19).

## Mfano wa Kuacha matunda yanayodumu

Jerry na Marilyn waliwafundisha wanandoa wapya wakati mme alipokuwa chuo cha udaktari. Alipomaliza muda wake wa mafunzo ya utabibu, walihamia kwenye makazi ya chuo kikuu na walianza kufanya wanafunzi wa Yesu. Baada ya takribana mwaka mmoja, waliamua kwamba ufanyaji wanafunzi wao ulikuwa ukienda kwa kasi ndogo sana. Walihisi kwamba itakuwa vizuri kwao kuwekeza muda wao kwa makundi makubwa badala ya kufundisha watu wachache kwa mara moja. Kwa hiyo kwa takribani miaka kumi na tano au zaidi iliyofuata, wanandoa hawa waliwekeza maisha yao katika makundi makubwa ya wanafunzi wa kimataifa. Waliwapenda,waliwatia moyo, walijaribu kuwasaidia kupata mahitaji yao, waliwakabirisha nyumbani kwao, waliwasaidia katika kukabiliana na maisha ya Marekani, waliwashuhudia, waliwaalika kanisani kwao, na baadhi yao waliwaleta katika imani kwa Yesu kama Bwana na Mwokozi wao.

Hata hivyo, miaka kumi na sita na nusu baadaye, wana ndoa hawa walituita. Mme alituambia kwamba mwaka uliopita, Mungu amekuwa akimsadikisha katika Yohana 15:16 kwa wazo hili: Ya wapi Matunda yadumuyo katika maisha yako? Mwitikio wake ulikuwa kwamba hakuna matunda yanayodumu katika maisha yao. Alisema,

> Simaanishi kwamba hatukuwa na huduma kwa sababu tunayo. Tumekuwa tukijihusisha katika maisha ya wanafunzi wa kimataifa takribani 400. Lakini hatuna tunda lo lote linalodumu kwa sababu hatukuwafanya wanafunzi na kuwafundisha jinsi gani ya kuenenda kwa ukaribu wa ndani na wa binafsi na Mungu na jinsi ya kujizalisha wenyewe kiroho katika maisha ya watu wengine. Sasa wengi wao wamerejea katika nchi zao, lakini hawakuandaliwa kujisimamia watakapokutana na shinkizo nyumbani, na hawakuandaliwa kufanya wanafunzi na kuzalisha wafanyaji wa wanafunzi. Labda Mungu afanye muujizi katika maisha yao, hatuna matunda yanayodumu ambayo yatakwenda zaidi ya kizazi hiki kupenyeza kizazi kinachofuata. Tutumie baadhi ya vitabu vya wanafunzi vya *Ushirika wa Mtu na Mungu*! Tunarudi tena katika kile kilichotusaidia sisi binafsi kufundishwa. Tutaanza kuwafundisha wengine.

Moja ya kundi la mwanzo la wanandoa ambalo mme na mke hawa waliwafundisha baada ya kupokea vitabu walikuwa wanatokea China. Mwanamme alikuwa anaendelea na digrii ya Uzamivu (Ph.D) katika uhandisi wa umeme na mke wake alikuwa akiendelea na masomo chuoni pia. Walipokuwa wanapitia *Ushirika wa Mtu na Mungu*, wote wawili walimpokea Kristo kama Bwana na Mwokozi wao. Walipohitimu, walihamia

New Mexico, ambako mme alianza kufanya kazi serikalini. Mke aliwasiliana nasi kwa sababu alihisi kwamba Mungu hakutaka yeye afanye kazi, badala yake, alimtaka kuitafsiri *Ushirika wa Mtu na Mungu* kaktika Kichina kwa ajili ya watu wake. Tulimpa ruhusa kutafsiri *Ushirika wa Mtu na Mungu*, na alianza kazi hii ngumu. Kwa msaada kutoka kwa mme wake katika siku za mwisho za ujauzito wake, alitupatia toleo la awali la *Ushirika wa Mtu na Mungu* katika Kichina. Leo, baada ya miaka mingi na kwa msaada wa wengine wengi, tunachapisha na kufanya wanafunzi kwa kutumia *Ushirika wa Mtu na Mungu* katika namna Iliyorahisishwa na Utamaduni wa Kichina tukiwa Marekani na nchi nyingine.

Daktari tabibu na mke wake sasa wanayo matunda yanayodumu, na tunaomba kwamba uwekezaji wao katika kufanya wanafunzi na kuzalisha wafanyaji wa wanafunzi utaweza kupenya kila kizazi mpaka Yesu atakaporudi tena. Hawakujua kwamba uwekezaji wa muda wao katika jozi moja ya wanandoa katika kundi dogo kutaleta matokeo katika tafsri ambazo sasa zinapatikana katika lugha za takribani theluthi ya watu wote ulimwenguni.

## Mwongozo wa Kiongozi na Ujumbe wa Mwandishi.......................Kipindi cha 1

1. Anza kwa maombi.

2. Mkaribishe kila mmoja.

3. Mpe kila mtu kijitabu cha maelezo cha mwanafunzi.

    ***Elezea:*** Waeleze na kuwaonyesha wanafunzi jinsi ya kutumia kijitabu cha maelezo cha mwanafunzi. Usichukulie tu kwamba wanajua jinsi ya kutumia.

    - Hiki si kitabu ambacho unakisoma mfululizo kutoka ukurasa wa kwanza hadi ukurasa wa mwisho wa kijitabu cha maelezo cha mwanafunzi.

    - Kijitabu cha maelezo cha mwanafunzi kimegawanyika katika sehemu saba zifuatazo:

        **Utangulizi** (Kurasa 9-46)

        **Soma** (Kurasa 47-72)

        **Meditate** (Kurasa 73-78)

        **Tafakari** (Kurasa 79-86)

        **Kujifunza** (Kurasa 87-232)

        **Kushika** (Kurasa 233-238)

        **Kazi za Ziada** (Kurasa 239-286)

    - Kila ukurasa una kisanduku cheusi pembeni ukingoni mwa ukurasa, kikitambulisha sehemu ambako ukurasa huo unahusika.

    ***Kielelezo:*** Fikiria sehemu hizo saba katika kijitabu cha maelezo cha mwanafunzi kama vyumba mbalimbali katika nyumba.

    - Kadri tunavyoendelea kukipitia kijitabu cha maelezo cha mwanafunzi, tutajikuta ndani ya "vyumba" hivyo kila siku.

    ***Kuweka namba katika kurasa:*** Kurasa zimewekwa namba katika kisanduku kilichotiwa kivuli chini ya kila ukurasa, ukingoni nje ya ukurasa.

***Tambua katika kila kipindi (vi) lini kila ukurasa utajadiliwa:*** Chini ya kila ukurasa, katika kisanduku kilichotiwa kivuli ndani ya ukingo wa ukurasa, inaonyesha kipindi (vi) ambapo huo ukurasa utajadiliwa.

***Uliza:*** Je kuna yeyote ana swali kuhusu utumiaji wa kijitabu cha maelezo?

4. Soma/Jadili **Nadhiri Yangu kwa Mafunzo ya Uanafunzi**, na kuwahasisha wanafunzi kuweka sahihi na tarehe ya nadhiri ya hiyo (Ukurasa 11).

    ***Maelezo:*** Ni muhimu kwa wale unaowafundisha kuonyesha kujiwekea nadhiri kwao katika mafunzo ya uanafunzi kwa faida yao wenyewe. Wana uwezekano mkubwa wa kumaliza na wewe ikiwa wataweka sahihi na tarehe ya kujiwekea nadhiri huku. Baraka kubwa zaidi ni kwa wanafunzi ambao watashiriki katika madarasa yote na kumaliza kazi wanazopewa kila siku.

    ***Wahamasishe:*** Mwishoni mwa kipindi cha kwanza, mhamasishe kila mwanafunzi kumwandikisha mshirika mwingine darasani kama mwana maombi mwenza. Wote wawili watakua kwa kuomba pamoja, na kuhamasishana na kusaidiana huku kutawawezesha kupita katika nyakati ngumu au za shida.

5. Soma/Jadili **"Kwa kuwa kusudi langu la dhati ni kwamba niweze kumjua Yeye"** (Ukurasa 9).

    ***Hadithi:*** Paulo alikuwa kifungoni huko Rumi wakati alipowaandikia Wafilipi. Chumba cha gereza ambacho wanazuoni wanaamini alikuwa ameshikiliwa kilikuwa kidogo. Hakikuwa na madirisha na wala milango; kwa hiyo, hakukuwa na mwanga uliotoka nje. Mfungwa alitelemshwa kwenye chumba kupitia tundu lililokuwa darini. Katika sehemu moja ya chumba kulikuwa na nguzo ambako inawezekana ndipo alifungwa kwa mnyororo. Kuta zilikuwa zimejengwa kwa mawe yaliyochongwa, na upande mmoja wa ukuta uliachwa ili kutoa nafasi kwa ajili ya kitanda. Kilikuwa na baridi, chenye unyevunyevu, na inawezekana kilikuwa kumejaa panya. Bado katika mazingira haya magumu na ya hatari, Paulo hakuwaza juu ya kuachiliwa kwake kutoka gerezani bali tu apate kumjua Kristo kwa kina na kwa undani zaidi kuliko alivyowahi kumjua.

***Maelezo:*** Neno *kujua* katika lugha ya Kiyunani halimaanishi ufahamu wa maarifa tu bali pia ni kujihusisha kwa karibu au kwa undani.

- Tito 1:16 (NIV): *"Wanakiri ya kwamba wanamjua Mungu, bali kwa matendo yao wanamkana. Ni wenye machukizo, waasi, wala kwa kila tendo jema hawafai."*

***Maswali:*** Waombe wanafunzi kuandika haya yafuatayo chini ya ukurasa wa 9:

**Maswali manne** juu ya kuweza kumjua Yesu:

1. Kama siyo hapa, wapi?
2. Kama siyo namna hii. Namna gani?
3. Kama siyo sasa, lini?
4. Kama hakuna kabisa, kwa nini?

***Uchunguzi:*** Wakati mwingine pale wanafunzi walipoanza kuzifanyia mazoezi kanuni za kiroho kama kusoma Biblia, kujifunza Biblia, kushika maandiko, kutafakari na kuomba, walikosea kwa kuanza kuziangalia kanuni kuliko kumwangalia Yesu na Yesu peke yake. Matokeo ni kwamba baadhi yao walianguka njiani na kutokuwa na ufanisi kwa ajili ya Mungu. Kwa hiyo, tutachunguza mstari huu kila juma kwa sababu kuu tatu:

1. **Ili kuyafanya macho yetu yamwelekee Yesu** na Yesu peke yake na kutukumbusha kwamba **kusudi letu la dhati ni kumjua Yeye**.

2. Ili kutukumbusha kwamba nidhamu au kanuni zenyewe haziwi mwisho. Bali **ni njia tu ambazo Mungu ametupatia ili tumjue Yesu** kwa kina, kwa undani na kibinafsi.

   ***Maelezo:*** Uzoefu wetu umetuonyesha kwamba tunazifanyia mazoezi kanuni hizi za kiroho kufikia lengo letu la kumjua Yeye, furaha inayojitokeza huzinga/hufunika kama kivuli kazi yoyote iliyotakiwa.

   ***Mifano:***

   - Je, ni vigumu kwa watu wanaopendana kuwa pamoja ili kufahamiana wao kwa wao?

- Je siyo furaha ndiyo inayoondoa wazo lolote lenye usumbufu au juhudi inayotakiwa ili kumshika mtoto au mjukuu katika mikono yako kadri unavyomjua zaidi mtoto huyo?

3. Ili kuzitafakari kweli zenye nguvu katika mstari huu. Ili kuzitoa kutoka kwenye ukurasa, kwenda vichwani mwetu, na kisha kwenda mioyoni mwetu kupitia kutafakari **ili kwamba Mungu aweze kuzitumia kutubadilisha katika mfano wa Yesu**.

6. Soma/Jadili **Makusudi ya Maisha kwa Ujumla** (Kurasa 12-13).

***Swali:*** Waombe wanafunzi kutaja baadhi ya malengo ambayo wanaume/wanawake wanayo siku za leo.

***Maneno ya Msingi:*** Ili kufikia lengo lolote, tunapaswa kuyafahamu maneno haya mawili: ***Ondosha*** na ***kumakinika*** (kuwa makini). Katika kuenenda kwetu na Mungu, inamaanisha kuondosha vitu vyote visivyo na umuhimu na kumakinika katika kile Mungu anakifikiria kuwa cha muhimu. Wengi wetu tunafanya makosa ya kuondosha kile Mungu anachofikiri ndicho cha muhimu zaidi na kumakinika katika kile ambacho hakina umuhimu.

Sasa yaangalie **Makusudi ya Maisha kwa Ujumla**. Utaona kwamba yanaakisi umilele kuliko mitazamo ya muda mfupi. Mungu anataka kutumia malengo haya kuyabadilisha maisha yetu, lakini lazima tuwe na utayari wa kuondoa na kumakinika. ***Malengo yafuatayo yanaweza na yanapaswa kuwa shauku inayomtawala kila Mkristo***.

1. **Kumjua Yeye katika namna nne:**

   - Katika hali endelevu, kwa kina, kwa ukaribu au undani na Kibinafsi

   - Kutambua, kukubaliana, na kuelewa maajabu ya mtu huyu, Yesu

   - Kwa kupata uzoefu katika maisha yetu ya kila siku kwamba ni nguvu ile ile ya kimiujiza ambayo aliionyesha katika Kufufuka Kwake

- Kwa kushirika katika mateso Yake kwa sababu ni kwa kupitia uzoefu huo ndipo Mungu anatubadilisha katika mfano Wake

2. **Ili Kumtukuza Yeye:**

- Katika 1Wakorintho 10:31. zungushia maneno, *"fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu."*

- *Kumtukuza* kunamaanisha, "kumheshimu na kumwadhimisha."

- Hii ndio inatakiwa kuwa dhamira yetu kwa kila wazo, neno, mwelekeo na tendo.

- Hata katika mambo ya kila siku na marahisi katika maisha, kama vile kula, na kunywa, tunaweza na tunapaswa kumpa utukufu Yesu.

- Katika Yohana 17:4 (NKJV) "Yesu alimtukuza Baba kupitia utii ulio dhahiri.

  - Inatuonyesha kwamba Mungu hutukuzwa kipekee kupitia utii wetu Kwake.

  ***Nukuu:*** "Maisha ni uwakili kutoka kwa Mungu ili yatumike kwa ajili ya utukufu Wake." —John MacArthur, Jr.

3. **Ili kuwa kama Yeye katika kusudi letu na katika tabia zetu.**

   ***Kufanana na Yeye katika kusudi letu***—Pale tunapofikia mahali pa kuwa na ujasiri mkubwa katika Mungu kiasi kwamba tunataka kusudi Lake zaidi kuliko la kwetu, tunalichagua kusudi Lake kuwa la kwetu wenyewe.

   - Katika Mathayo 26:39 (NIV), tunaiona picha nzuri ya Yesu katika maombi, akimwomba Baba, "*Kama ikiwezekana, kikombe hiki kiniepuke. Walakini si kama nitakavyo mimi, bali kama utakavyo wewe."*

     - Inawezekana huu ulikuwa uamuzi mgumu zaidi aliokabiliana nao Yesu kwa sababu *kikombe hiki* kinawakilisha hatia,

aibu na kutengwa mbali na Baba kwa sababu ya dhambi zetu na hii ilimaanisha:

- Yesu alipaswa kuzichukua dhambi zetu zote yeye Menyewe ili kulipia kwa ajili ya dhambi zetu. Fikiria juu ya hilo. Kamwe hakuwahi kupitia kutenda dhambi au ghadhabu ya Mungu itokanayo na dhambi.

- Kwa sababu Yesu alikuwa radhi kuwa mtii na kuchukua dhambi zetu juu yake mwenyewe, dhambi zetu zilimtenga Yeye mbali na Baba. Fikiria juu ya hilo. Kamwe Yesu hakuwahi kutengana mbali na Baba.

- Pale Yesu aliposema, "*Walakini si kama nitakavyo mimi, bali kama utakavyo wewe"* aliweka kielelezo au mfano kwa ajili yetu ili siku zote tutamani mapenzi ya Mungu zaidi kuliko mapenzi yetu wenyewe, bila kujali gharama.

***Kama Yeye katika tabia zetu***—Kidogo kidogo Mungu anatubadilisha katika mfano wake:

- **Utakatifu:** Usafi kamili katika kila eneo la maisha, tukijifunza kuishi kama Yeye, ni mchakato uliokamilishwa pale alipokwenda mbinguni.

- **Haki:**

  - Katika Warumi 10:10 *"Mtu huamini kwa moyo hata kupata haki."*

  - Ni haki yake, wala siyo yetu—Tito 3:5; Wafilipi 3:9; Warumi 10:3; Mathayo 6:33; 2 Wakorintho 5:21; Warumi 3:21-22.

  - ***Hadithi:*** Wakati wavulana wetu walipokuwa wadogo, waliagiza kizibo cha boksi la nafaka cha $2.00 kwa watengenezaji wa nafaka na wakaagiza kitabu

chenye mfumo unaotangaza juu ya boksi la nafaka. Kitabu kilipofika, kila ukurasa ulikuwa umejaa kwa herufi zenye mwendelezo zilizogeuzwa ili kwamba usiweze kusoma neno moja moja au sentensi. Lakini kitabu kilikuja na kipande cha karatasi ya plastiki chekundu kilichoangaza. Pale ulipoweka plastiki juu ya ukurasa wowote katika kitabu chenye mfumo, ilizuia baadhi ya herufi, na basi ungeweza kuusoma ujumbe. Nilipoona hilo, lilizungumza kwangu juu ya haki ya Mungu. Niliona kipande cha plastiki chekundu kinachoangaza kama damu ya Yesu iliyomwagika kwa ajili yangu pale msalabani. Na ilinisaidia mimi kuona kwamba kwa vile nimempokea Yesu moyoni mwangu kama Bwana na Mwokozi wangu, ninamtumaini Yeye, hata kama nikitenda dhambi, Baba ananiangalia, ananitazama kupitia damu ya Yesu, na hiyo huzuia dhambi zangu. Kwa hiyo, japokuwa ninatenda dhambi, Ananiona mimi kama mwenye haki kwa sababu dhambi zangu zimefunikwa kwa dhabihu ya damu ya Yesu aliyekufa badala yangu.

- 2 Wakorintho 3:18 (NLT)—Mstari huu unatupatia tumaini la ajabu. Kila mmoja wetu anaweza kuwa kioo kinachoakisi utukufu wa Bwana. Tunatakiwa kujitoa tu (Warumi 6:13) kwa Mungu na kumruhusu Yeye kutawala maisha yetu kila wakati kila siku ili kwamba aweze kufanya kazi kwa uhuru ndani yetu na kutufanya sisi kufanana na Yeye zaidi na wakati huo huo kututumia kama vioo ambavyo kupitia hivyo anajiakisi Mwenyewe kwa wengine. Ni Mungu wa ajabu namna gani!

- Warumi 12:2 (RSV):

    - Ule usemi. "***Wala msiifuatishe namna ya dunia hii***, imetafsiriwa na J. B. Phil-

lips kama ***"Usiruhusu ulimwengu unaokuzunguka ukubane katika namna yake."***

- Ule usemi ***"Kufanywa upya kwa nia zenu"*** imetafsiriwa katika Amplified Bible, *"Bali mgeuzwe (mbadilishwe) kwa (kwa ujumla) kufanywa upya nia zenu – kwa mawazo yenu mapya [malengo] na mitazamo yake mipya..."*

  - Shauku ya kufikia **Makusudi ya maisha kwa Ujumla** ni njia mojawapo ya kufanywa upya nia zetu.

  - Shauku ya kuifikia **misimamo mipya** ni njia nyingine ya kufanywa upya nia zetu. Wafilipi 2:5-8 (NIV) inasema, *"Iweni na nia iyo hiyo ambayo iliyokuwamo ndani ya Kristo Yesu."* Hapa ndivyo kifungu hiki kinavyouelezea msimamo Wake:
    - *"Yeye mwenyewe alijifanya kuwa si kitu"*
    - *"Alichukua ile asili ya mtumishi au mtumwa"*
    - *"Alijinyenyekeza"*
    - *"Akawa mtii hata mauti .... Naam mauti ya msalaba!"*
    - Inawezekana lililo kuu katika misimamo hii mipya linaweza kuwa **ni msimamo wa utii**, ambao unasema, "Bwana nitakutii; Wewe sema tu." Huu ni mtazamo ulioonyeshwa na Petro pale alipoitikia kwa Yesu kwa kusema, *"kwa Neno lako nitafanya"* (Luka 5:5 NKJV).

      - Msimamo wa utii unaweza kutusaidia kuiitikia kwa njia sahihi katika migogoro.

***Hadithi:*** Mchungaji mmoja alinisimulia hadithi hii juu ya mtu ambaye alihudhuria madarasa yangu ya uanafunzi kule Romania. Mtu huyu alikuwa Mkristo na alikuwa akifanya kazi kwenye gereji bubu (za mtaani). Alikuwa amejitoa kumtii Kristo bila kujali gharama. Siku moja miongoni mwa mabosi wake, kumi walimjia na kumwambia kwamba lazima aache Ukristo au kama hawezi kufanya hivyo watamwachisha kazi—na hiyo ilimaanisha kwamba angeweza kufungwa gerezani kwa kutofanya kazi. Yeye aliwapungia kuwaaga na akaanza kutoka nje ya mlango. Yeye alikuwa anafanyia kazi msimamo wa utii. Alikuwa amejitoa kutii ndipo Mungu akazungumza, na Mungu alikuwa tayari amezungumza naye achague ikiwa ni Mungu wake ama kazi kipi kilikuwa cha muhimu zaidi. Alikuwa ni mfanyakazi mzuri sana kiasi kwamba mabosi wake walimsimamisha na kumwambia atabakia

na kazi yake. Kama unavyoweza kukisia, kamwe hakupandishwa cheo, bali alikuwa na amani na furaha ambayo ilitokana na kujua kwamba alikuwa mwaminifu kwa Yesu.

***Swali:*** Baada ya kumaliza kusoma na kujadili Makusudi haya ya Maisha kwa Ujumla, waulize wanafunzi jinsi gani watayatumia makusudi haya matatu kuwasaidia kufanya maamuzi sahihi kila wakati.

***Jibu:*** Katika njia panda yoyote, kila wakati tunapotakiwa kufanya maamuzi, huwa tunajiuliza wenyewe maswali haya matatu kuhusiana na uchaguzi wetu:

1. Uchaguzi upi utanisaidia mimi kumjua Yesu vizuri zaidi?
2. Uchaguzi upi utanisaidia kumletea utukufu zaidi Yesu?
3. Uchaguzi upi utanisaidia kuwa kama Yesu katika kusudi langu na/au katika tabia yangu?

Kisha tunafanya uamuzi, kutegemeana na uchaguzi ambao utatupatia fursa kubwa zaidi za kuyafikia Makusudi yetu ya Maisha kwa Ujumla.

7. Soma/Jadili Katika kuliangalia Darasa Hili (Ukurasa 14).

***Maelezo:*** Wakati tunapoongea kuhusu mifumo ya Maisha (sehemu ya II, C. 2), ni muhimu kusisitiza kwamba njia mojawapo ya kujenga mifumo hii ni kwa kufanya kazi za ziada katika mafunzo ya *Ushirika wa mtu na Mungu* kila siku. Ni muhimu sana kufanya kazi za ziada kila siku kwa sababu siyo tu tunajaribu kufundisha kweli bali kujenga mtindo wa maisha ambao unamuakisi Yesu.

***Maelezo:*** Wakati tulipozungumzia kuhusu mpango (Sehemu III, A-E) ambao tutaufuatilia kadri tunavyopitia mafunzo ya Ushirika wa mtu na Mungu, ni muhimu kuelewa kwamba **Yesu alitumia mpango huu katika kuwafunza wanafunzi wake:**

- **Yesu alitambulisha somo.**

- **Yesu aliwaambia sababu (kwa nini).** Katika Mathayo 4:18-19, aliwataka kumfuata Yeye. Kwa nini? Alitaka kuwafanya wao kuwa watu ambao watawekeza maisha yao katika uvuvi wa watu.

- **Yesu aliwaonyesha jinsi ya kufanya (jinsi gani):** Marko 1:35 ni mfano wa jinsi Yesu alivyoonyesha mfano kwa wanafunzi wake jinsi ya kuwa pekee yake na Mungu kwa kutafuta mahali penye utulivu, mahali pasipo na watu alfajiri na mapema asubuhi mahali ambapo Yeye na Baba wasingesumbuliwa. Yesu alikuwa akisisitiza kwao na kwetu umuhimu wa kutafuta muda wa kuwa pekee yako na Mungu kila siku.

- **Yesu aliwawezesha au aliwafanya kuanza.** Katika Mathayo 28:19-20, Yesu ametuonyesha sisi kwamba wanafunzi wanaofanywa, wanahitajika kutumwa kwenda kuwafanya wanafunzi. Wanafunzi wote wa kweli wanapaswa kuwa na dhamira, wazalishaji wenye kusudi la wanafunzi ambao wanafanya wanafunzi. Kwa hiyo, kama Yesu, sisi pia tunapaswa kuwafanya (wanafunzi wetu wapya) kuanza kuzalisha walimu wa wanafunzi wengine.

- **Yesu alifuatilia.** Katika Mathayo 26:36 (NIV), Yesu alimwambia Petro na wana wawili wa Zebedayo, *"Kaeni hapa mkeshe pamoja nami."* Mara tatu katika Mathayo 26:40, 43, 45 Yesu aliwarudia kutoka kwenye muda wake binafsi (wa kuwa peke yake) na Mungu katika maombi kuwafuatilia.

8. Soma/Jadili Mstari Ulionipa Amani (Kurasa 15-16).

   ***Maelezo:*** "Mstari Ulionipa Amani" utakupa wewe fursa ya kugundua mambo mawili ya muhimu sana:

   - Je, kila mwanafunzi wako anao ujasiri juu ya uzoefu wake wa wokovu?

   - Je, wanafunzi wako wana mashaka na Neno la Mungu au kusimama katika ahadi Zake?

     - Wakati mwingine Wakristo hawana ufanisi kwa ajili ya Mungu kwa sababu Shetani anaendelea kuibua maswali katika akili zao kuhusu wokovu wao. Mungu anatutaka tuweze kutulia na tupate amani. Ametueleza kwamba tunaweza kujua kwa hakika

kwamba tumeokoka (1Yohana 5:13). Ikiwa tunalitilia mashaka Neno la Mungu, basi tunautilia mashaka uadilifu wa Mungu. Ni lazima tusimame kwa ujasiri katika ahadi zake.

- Unaweza kutaka kuwauliza wanafunzi wako maswali haya makuu ya Mlipuko wa Kiinjilisti:

    1. Je, umewahi kufikia mahali katika maisha yako ya kiroho ambapo unajua kwa hakika kwamba ikiwa ungetakiwa kufa leo ungekwenda mbinguni?

    2. Chukulia ungetakiwa kufa leo na kusimama mbele za Mungu na Akaweza kukuambia, “Kwa nini nikuruhusu wewe kuingia katika mbingu yangu?” Ungesema nini?

- Kwa miaka mingi tumeweza kupata upendeleo au heshima ya kuona watu wengi wakimwamini Yesu kama Bwana na Mwokozi wao binafsi kwa kuwashirikisha mistari ifuatayo: Warumi 3:23; Warumi 6:23; Yohana 3:16: Yohana 1:12, na Waefeso 2:8-9. Inaweza kuwa msaada mkubwa kama utawashirikisha mistari hii wanafunzi wako.

- Vile vile tumeona watu wengi wakipata uhakika wa wokovu baada ya kuwashirikisha simulizi au hadithi hii ya jinsi mtu mmoja alivyopata uhakika.

    ***Hadithi:*** Shetani alikuwa akimshambulia mara kwa mara mtu mmoja juu ya kwamba ameokoka au la. Kwa hiyo siku moja baada ya kusoma Yohana 5:24, mtu huyu alikwenda nyuma ya moja ya majengo yake na akachimbia nguzo ya mbao ardhini. Aliandika juu ya ile nguzo Yohana 5:24 na tarehe, kisha akapiga magoti na kuomba, “Bwana, sina uhakika kama nimeokoka, lakini kama sijaoko ka, ninajua nimetenda dhambi na ninajua kwamba Wewe ulikufa kwa ajili ya dhambi zangu. Niko tayari

kuacha dhambi zangu na kukugeukia Wewe na Wewe peke yako. Tafadhali nisamehe dhambi zangu na ingia katika moyo wangu kama Bwana na Mwokozi wangu sasa hivi. Bwana, kulingana na ukweli kwamba Wewe ni mwaminifu na siku zote unazitimiza ahadi Zako, ninasimama katika ahadi Yako katika Yohana 5:24. Ninajua kwamba sasa nimeokoka. Asante, Bwana". Baada ya zoezi hili, kila wakati Shetani alipojihudhurisha kujaribu kumfanya mtu huyu kuutilia shaka wokovu wake, mtu huyu alikwenda nyuma ya nyumba na kuonyesha kwenye ile nguzo, ikisema, "Shetani, ninasimama katika ahadi ya Mungu. Wokovu wangu ulikamilishwa siku ile nilipoandika juu ya nguzo hii."

***Maelezo: Sababu nyingine kwa nini ni muhimu kwetu sisi kusoma na kujadili "Mstari Ulionipa Amani***":

***Hadithi:*** SWakati mwingine tunafanya makosa kwa kufikiria kupita kiasi. Wakati fulani Marilyn alikuwa akimfundisha binti ambaye alikuwa amekaa muda mrefu akiwa mpweke (kapera) kanisani kwetu. Alikuwa ni kiongozi kwa asili, na wakati wote tungeweza kumtegemea. Walipokuwa wakipitia mafunzo ya Ushirika wa Mtu na Mungu, Marilyn aliamua kwamba japokuwa hakuwa kufanya hilo kabla, ataruka "Mstari Ambao Ulileta Amani" kwa kuwa binti huyu alionekana kuwa kama Mkristo mzuri. Kisha Marilyn akahisi katika roho yake kwamba hatakiwa kuruka sehemu hii, kwa hiyo alimtaka yule binti asome kwa sauti "Mstari Ambao Ulileta Amani." Alipokuwa akisoma, machozi yalianza kutiririka mashavuni mwake. Alisema, "Marilyn, sijawahi kufanya hili [kuzaliwa upya]. Nilipokuwa binti mdogo, nilimfuata kaka yangu kwenda madhabahuni, walijaza kadi kwa ajili yangu, na nilibatizwa pamoja na kaka yangu. Kuanzia wakati huo kila mtu alifikiri kwamba mimi nilikuwa Mkristo, lakini nimefahamika kwa miaka hii yote kwamba sikuwa nimeokoka." Marilyn na yule binti walipiga magoti wakiwa sebuleni kwetu, na aliamini katika Yesu na Yesu peke yake kama Bwana na Mwokozi wake. Jumapili iliyofuata alijisalimisha mwenyewe kanisani kwa ajili ya ubatizo wa mwamini.

- Uzoefu huu ulitufundisha mambo mawili:

    1. **Usidhanie au kufikiria tu** kwamba watu unaowafundisha ni waamini wa kweli.

    2. **Kamwe usiruke** kitu chochote katika kijitabu cha maelezo wakati unafundisha kwa sababu inaweza kuwa lile ni hitaji **maalumu kwa mtu fulani katika kundi**.

***Mwaliko:*** ABaada ya kuwa umemaliza kusoma, "Mstari Ulionipa Amani" ndani ya darasa, waalike wale ambao hawana hiyo amani kubaki baada ya darasa au kukupigia simu ili mzungumze jinsi gani wanaweza kuipata amani. Tunao ujasiri kwamba unaweza kuwasaidia watu wanaouitikia mwaliko wako kwa kushirikiana nao taarifa kutoka kurasa zilizotangualia, lakini kama unasita, fanya miadi na mmoja wa wachungaji wako au mtu yeyote unayemjua. Nenda pamoja na mtu huyo, na mwache mchungaji au rafiki yako kueleza kwa mwanafunzi jinsi anavyoweza kupata amani kupitia msamaha wa Mungu kwa kusimama katika ahadi Zake.

- Watu wengi wamempata Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi wao wakati wanapitia mafunzo ya *Ushirika wa Mtu na Mungu.*

***Maelezo:*** AWatu wengi wamempata Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi wao wakati wanapitia mafunzo ya Ushirika wa Mtu na Mungu:

***Kanuni***—*"Amini, amini, nawaambia, Yeye alisikiaye Neno langu na kumwamini Yeye aliyenipeleka yuna uzima wa milele; wala haingii hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia uzimani"* (Yohana 5:24 NKJV).

***Kanuni ya Msingi***—Amini na kusimamia katika kile Mungu anachosema.

***Swali***—Je Neno la Mungu (Biblia) ndio mamlaka katika maisha yako?

9. Soma/jadili Ubatizo (Kurasa 17-18).

***Maelezo:*** Moja ya matendo ya mwanzo ya utii kwa Mkristo mpya ni kubatizwa.

- Luka 6:46 (NLT) inasema, *"Kwa hiyo kwa nini mnaniita 'Bwana" wakati hamnitii?"*

  - Yesu ndiye aliyetoa maelekezo kwamba mwamini mpya anapaswa kubatizwa (Mathayo 28:19).

  - Kama Yesu ni Bwana na Mwokozi wetu, tunapaswa kuwa wazi kabisa kwamba lazima tuwe watii katika amri Yake na tubatizwe.

- Kwa kuwa ubatizo ni picha ya kile ambacho kilikwisha-tokea katika mioyo yetu na unatutambulisha sisi kama wafuasi wa Yesu, basi wale ambao walibatizwa kabla ya kumwamini Yesu kama Bwana na Mwokozi wao binafsi wanapaswa kuhamasishwa kubatizwa tena. Vinginevyo wanaweza wasipate amani kwani Neno la Mungu linatu-fundisha kwamba wokovu lazima uje kabla ya ubatizo.

10. Eleza jinsi ya kutumia **Changamoto za Kusoma Biblia Kila Siku Mwezi wa Kwanza** (Ukurasa 49).

    ***Maelezo:*** Kusoma Neno la Mungu kila siku ni sehemu ya mtindo wa maisha tunaojaribu kuwasaidia wanafunzi kuu-kuza au kuuendeleza.

- ***Andika***—maombi haya mafupi juu ya ukurasa wa 47-48. kisha kila asubuhi kabla ya kusoma Biblia, omba, "Bwa-na, tafadhali fungua ufahamu wangu ninaposoma Neno Lako asubuhi hii" (Luka 24:45 NKJV).

- ***Andika*** —tmaombi haya mafupi chini ya ukurasa wa 47-48. kisha kila asubuhi baada ya kuwa umesoma Biblia, omba, "Bwana, nakushukuru Wewe kwa muda nilio-kuwa na Wewe asubuhi hii" (M/Nyakati 29:13).

- Mathayo 4:4 (NKJV)—"*Lakini akajibu akasema, 'Ime-andikwa, Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu.*'"

- Yeremia 15:16 (NKJV)—"*Maneno yako yalionekana, nami nikayala; na maneno yako yalikuwa ni furaha kwangu, na shangwe ya moyo wangu; maana nimeitwa kwa jina lako, Ee Bwana, Mungu wa majeshi.*"

- Zaburi 34:8 (NKJV)—"*Onjeni mwone ya kuwa Bwana yu mwema; Heri mtu yule anayemtumaini!*"

- 2 Timotheo 3:16 (NKJV)—"*Kila andiko lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki...*"

11. Tafuta kupata usikivu wa wanafunzi kwa Kazi zao za Ziada (Kurasa 241-242).

    ***Soma darasani:*** Ruhusu muda wa kusoma ukurasa 241 kwa sauti darasani na hakikisha kwamba kila mmoja anaielewa kazi ya ziada.

12. Elezea jinsi ya kutumia karatasi ya Ufuatiliaji (Ukurasa 273):

    ***Maelezo***—Waambie wanafunzi: Kuanzia kipindi cha 2, utakuwa na karatasi ya ufuatiliaji kuijaza kabla ya kila kipindi. Katika kila kipindi kiongozi wako atakagua na kutia sahihi karatasi mpya ya Ufuatiliaji uliyoiandaa kwa ajili ya juma hilo. Utahitaji taarifa zifuatazo katika karatasi yako ya Ufuatiliaji kila juma:

    - Andika **Jina** lako.
    - **Tarehe ya Taarifa** ni siku mkutano wako unaofuata.
    - **Muda wa Kuanza** ni punde kabla hujaomba na kumwomba Mungu kuzungumza na wewe unaposoma mistari uliyopangiwa kila siku.
    - **Muda wa Kumaliza** ni pale unapoacha kufanya kazi yako ya ziada katika mafunzo ya Ushirika wa Mtu na Mungu kwa siku na umeomba na kumshukuru Mungu kwa ajili ya muda uliokuwa naye.

13. Funga kwa maombi.

## Mwongozo wa Kiongozi na Ujumbe wa Mwandishi........................Kipindi cha 2

1. Anza kwa maombi.

   ***Mfano**:* Waalike wanafunzi kupiga magoti pamoja na wewe mnapoomba pamoja na kuutoa muda kwa Mungu. Katika majuma machache yajayo utawataka wanafunzi kuomba wakiwa wamefungua macho yao wakiwa wanatembea, wamesimama, wanaendesha, n.k. lakini unawataka kuelewa kwamba ni muhimu kupiga magoti yao na kuomba kila wanapoweza kufanya hivyo.

2. Mtake kila mmoja kufungua katika karatasi ya **Ufuatiliaji** ambayo inahitajika siku hiyo. Kisha unaweza **kuzikagua na kuzisaini** (Ukurasa 273).

   ***Uwajibikaji**:* Ukaguzi na uwekaji sahihi karatasi zao za Ufuatiliaji kila juma huwafundisha wanafunzi katika kanuni ya uwajibikaji iliyofundishwa katika Warumi 14:12. Pia inakusaidia wewe kama kiongozi kuona kama wanafunzi wako:

   - Wanafanya kazi za ziada na kujijengea mtindo wa mai sha au
   - Wanahitaji kuhamasishwa au kutiwa moyo na wewe.

3. Hakiki au tathmini **Nadhiri Yangu katika Mafunzo ya Uanafunzi** (Ukurasa 11).

   ***Hamasisha**:* Watake wanafunzi kutia sahihi na tarehe kujiwekea nadhiri huko kama walikuwa hawajafanya hivyo bado.

   - Wanafunzi wana uwezekano wa kumaliza mafunzo ya *Ushirika wa Mtu na Mungu* kama watatia sahihi karatasi ya kujiwekea nadhiri.
   - Baraka kubwa zaidi ni kwa wanafunzi ambao wanashiriki katika madarasa yote na kumaliza kazi zao za ziada kila siku.

4. Soma **"Kwa kuwa Kusudi langu la dhati ni kwamba nimjue Yeye"** (Ukurasa 9).

   ***Andika na kujadili:*** Waombe wanafunzi kuandika upande wa juu kwenye ukurasa wa 9:

**Vikwazo** vya kumjua Yesu Kristo kwa kina, kwa undani na kibinafsi (Luka 8:14 LIV):

1. Wasiwasi(usumbufu)
2. Utajiri/mafanikio
3. Wajibu/majukumu
4. Anasa/starehe

***Uchunguzi:*** Wakati mwingine pale wanafunzi wanapoanza kuzifanyia mazoezi kanuni za kiroho kama vile kusoma Biblia, kujifunza Biblia, kushika maandiko, kutafakari, na maombi, wanakosea kwa kuanza kuziangalia kanuni kuliko kumwangalia Yesu, na Yesu peke yake. Matokeo yake ni kwamba baadhi yao wanaanguka njiani na kutokuwa na ufanisi kwa ajili ya Mungu. Kwa hiyo, tutautathmini mstari huu kila juma kwa sababu kuu tatu:

1. **Ili kuyafanya macho yetu yamwangalie Yesu** na ni Yesu peke yake na kutukumbusha kwamba **kusudi letu la dhati ni kumjua Yeye**.

2. Ili kutukumbusha kwamba **kanuni hizi siyo mwisho katika zenyewe. Hizi ni njia tu ambazo Mungu ametupatia kumjua Yesu** kwa kina, kwa undani au ukaribu na kibinafsi. Kwa hiyo, tunazifanyia kazi kanuni ili kwamba tuweze kumjua Yeye.

   ***Maelezo:*** Uzoefu wetu umetuonyesha kwamba kadri tunavyozifanyia mazoezi kanuni hizi za kiroho kufikia kusudi la kumjua Yeye, furaha ya kugundua huhamisha au kuyaondoa mawazo kama vile: *Ni lazima, Ninapaswa, au Ninawajibika kuifanyia kazi kanuni hii.*

3. **Ili kutafakari juu ya kweli yenye nguvu** katika mstari huu. Kuzihamisha kutoka kwenye ukurasa kwenda kwenye vichwa vyetu na kisha kwenda mioyoni kupitia kutafakari **ili kwamba Mungu aweze kuzitumia kutubadilisha sisi katika mfano wa Yesu**.

5. Jadili **Maswali ya Marudio ya Kazi ya Ziada** (Ukurasa 242).

   ***Maelezo:***

   - Watake watu mbalimbali katika kikundi kujitolea kusoma moja ya maswali na kushirikisha majibu yao.

- Baada ya mtu mmoja kusoma swali la 4 katika ukurasa 242 na kushirikisha uzoefu, wahamasishe wanafunzi kuzungumza kwa wengine juu ya Yesu na mambo anayowafundisha wao.

6. Soma/Jadili **Changamoto za Kutafakari** (Kurasa 75-78).

   ***Maelezo:***

- Kutafakari ni namna tunavyoihamisha kweli kutoka vichwani mwetu kwenda mioyoni mwetu. Kamwe kweli haitafanya kazi inavyopasa katika utekelezaji mpaka imeingia moyoni. Kwa hiyo, **kutafakari ni muhimu katika utekelezaji** (Yoshua 1:8).

- Ni muhimu kuelezea kwa wanafunzi kuwa wakati unawataka kutafakari, si kwamba tunataka waelezee kifungu kina maana gani.

  - Kutafakari ni jambo la kibinafsi zaidi likielezea tu maana ya kifungu. Kunahusisha **K**ufikiria kwa kina, **K**uvuta taswira, na **K**uomba (Kwa kifupi **KKK**) maombi ya kujitoa moja kwa moja kutoka moyoni mwako kwenda kwa Mungu.

  - Kutafakari ni kuihamishia kweli kwenda mioyoni mwetu ambako Mungu huitumia kweli hiyo kutubadilisha, kutufanya upya katika mfano wake na kutuweka huru.

- Wakati unapowataka wanafunzi kushirikisha taswira (picha) wanazoziona; siku zote watake kuanza kwa kusema, **"Hii ndio picha ninayoiona."**

  - Hivi karibuni mtu mmoja aliniuliza ikiwa wazo la kuvuta taswira lililofundishwa katika Agano la Kale limefundishwa pia katika Agano Jipya. Jibu ni ndiyo. Katika 1Timotheo 4:15, neno *tafakari* katika Kiyunani linamaanisha "kufikiri" ("Kamusi ya Kiyunani ya Agano Jipya" katika *Strong's Exhaustive Concordance of the Bible*, Ukurasa 47, namba 3191).

- Unapomwambia mmoja wa wanafunzi kuombea taswira au picha yake tena kwa Mungu kama ombi lake binafsi:

  - Kamwe usiseme, "Jinsi gani utayaombea (au kurudisha) tena kwa Mungu?"

- Siku zote sema, **“Ngoja tusikilize unapoomba tena kwa Mungu kama maombi yako binafsi”** Tunataka tu kusikiliza hasa pale mwanafunzi anapoomba.

*Kutafakairi Maandiko kunatusaidia kumjua Mungu.*

7. Soma/Jadili **Changamoto za Maombi** (Kurasa 81-82).

***Maelezo:***

- Efeso 6:18 (NLT):
    - **Jinsi ya kuondoa wasiwasi**—kama hujawahi kuombea hilo, usifikirie juu ya jambo hilo.
    - Omba popote, kila mahali na juu ya kila jambo.

        ***Hadithi:*** “Mhubiri” E. F. Hallock aliomba juu ya kila jambo – ikiwa ni pamoja na eneo la kuegesha gari. Siku moja Mhubiri aliendesha kwenda benki, na alipoikaribia benki, alimuomba Mungu kumpa eneo la kuegesha gari mbele ya benki. Hakuona eneo la kuegesha, kwa hiyo aliendesha kuzunguka jengo na akimwomba Mungu tena kwa ajili ya mahali pa kuegesha. Hili lilitokea mara kadhaa na hatimaye aliegesha huko mtaani. Mara tu mhubiri alipotoka kwenye gari lake na kuanza kutembea kando ya njia, alikutana na mtu aliyepotezana naye aliyekuwa akijaribu kumtafuta kwa majuma kadhaa. Pale njiani, katika muda mfupi tu, alimwongoza mtu huyu katika imani katika Kristo. Mungu alikuwa na mpango mzuri kwa ajili ya Mhubiri kuliko Mhubiri aliokuwa nao mwenyewe, na alikuwa tayari kupata maelekezo kwa upya kutoka kwa Mungu. “Walakini si kama nitakavyo mimi, bali kama utakavyo wewe” (Mathayo 26:39 NIV).

***Maelezo:***

- 1 Wathessalonike 5:17 (RSV)
    - *“Ombeni bila kukoma.”*
        - Jambo hili linaibua swali muhimu. Jinsi gani mnaweza kuomba bila kukoma wakati tunapaswa kufanya bidii katika mambo mengine katika wakati fulani?

- ***Kielelezo:*** Uthibitisho wa kwamba tunaomba "bila kukoma" unaweza kuonekana katika kielelezo rahisi. Fikiria juu ya akili yako kama raba bendi yenye nguvu. Wakati unakuwa makini katika mradi muhimu, akili yako inavutika. Swali la msingi ni kwamba pale mradi unapomalizika au unapokaa tu kupumzika kwa muda, je akili yako inarejea ghafla tena kwenye mawazo ya kusifu, kuabudu, na shukrani kwa Mungu? Je kuzungumza na Mungu katika maombi imekuwa jambo la kawaida linalochukua nafasi kubwa katika akili na moyo wako?

***Maelezo:***

- Kifupi cha maneno **K-K-K-K:**
  - Upande wa kushoto wa herufi "K" katika kuabudu (Ukurasa 82) andika neno "SURA" kwa sababu tunamwabudu Mungu kwa SURA yake, kwa jinsi Yeye alivyo:
    - Tunamwabudu Mungu kwa sababu Yeye ni Mtakatifu.
    - Tunamwabudu Mungu kwa sababu Yeye ni mwenye Haki.
    - Tunamwabudu Mungu kwa sababu Yeye ni Kweli.
    - Tunamwabudu Mungu kwa sababu Yeye ni Upendo.
    - Tunamwabudu Mungu kwa sababu Yeye ni Mwaminifu.

***Hadithi**:* Mmoja wa wachungaji wetu wa zamani alitumbia jinsi alivyokuwa akijisomea usiku moja, akijaribu kuandaa ujumbe kwa ajili ya Jumapili. Alikuwa kwenye chumba chake cha juu nyumbani kwake pale mtoto wake wa kike, aliyekuwa ndiyo anaanza kuongea, alipopanda ngazi na kuja hadi mlangoni kwake. Hakuwa na nguvu za kuweza kufungua kitasa lakini aliendelea kujaribu kuufungua mlango. Hatimaye aliweza kuufungua mlango na kuingia. Mchungaji wetu alikasirika kwa wakati huu kwa sababu kelele alizozipiga zilimfanya kuacha kusoma. Kwa hiyo akamgeukia kwa ukali na kusema, "Unataka

nini?” Yeye akamwendea tu, akampandia miguuni na kusema, **“Sikutaka kitu chochote, nilitaka tu kukuambia ninakupenda!”** Alijua jinsi ya kuonyesha namna ya kuabudu au kuadhimisha.

- Kushoto kwa herufi ***“K”*** katika *Kuungama* (ukurasa 82) andika maneno haya: *Ni wakati gani tunaungama dhambi?* Kisha andika jibu hili. *Ni wakati tunapopata ufahamu au kuzitambua dhambi zetu. Kwa nini? Ili kurejesha ushirika na Mungu kwa sababu dhambi inavunja ushirika wetu na Mungu.*

- Upande wa Kushoto kwa herufi ***K*** katika *Kushukuru* (Ukurasa 82) andika Neno *MKONO* kwa sababu tunamshukuru Yeye kwa yale aliyoyafanya, anayoyafanya, na atakayoyafanya.

    - Kwa siku nzima tunampa Mungu shukurani kwa ajili ya mambo yote, hata mambo ambayo tunayachukulia tu kama ni kawaida. Tunapaswa kuendeleza hali ya kushukuru na kujifunza kuonyesha shukrani zetu kwa Mungu pale tunapotembea au kuendesha, au katika hali yoyote. Tunataka kujifunza kuzungumza na Mungu siyo tu kama Bwana na Mwokozi wetu bali pia kama rafiki yetu wa karibu.

- Zingatia kwamba maombezi ni aina ya maombi. Ni kumwomba Mungu kwa niaba ya mtu mwingine.

8. Eleza jinsi ya kutumia **Kumbusho la Kufanya Maombi Kila Siku** (Kurasa 83-86).

    ***Maelezo****:*

    - Weka tarehe ya leo juu ya ukurasa panaposema: “Kutoka: _______ .”

    - Yesu anastahili ujasiri wetu mkuu tulio nao katika Yeye. Ni lazima tuamini kwamba Yeye atasikia na kujibu maombi yetu kwa wakati wake. Kadri tunavyomjua Yeye kwa undani zaidi, ndivyo tutakavyozidi kuwa na ujasiri katika Yeye.

    - Tunaomba mpaka Mungu ametupa amani. Tunaweza kuwa na amani miaka mingi kabla ya kuona jibu halisi.

Katika suala hilo, tunaendelea tu kuonyesha kuabudu na kushukuru kwetu kwa Mungu kwa ajili ya jibu hilo.

- Kwa sasa, weka tu jina la mwenzi wako wa maombi katika fomu hii na muombee kila siku. Tunaongeza tu majina na mambo mengine katika orodha zetu kama tunavyotaka au kama Mungu anavyotuongoza. Kisha tutaona kwamba kutumia orodha ya maombi litakuwa jambo ambalo tunataka kulifanya zaidi kuliko kitu kingine tunachopaswa kufanya.

***Hadithi:*** Hivi karibuni nilikuwa na furaha kumwona mtu akiomba kumpokea Kristo kama Bwana na Mwokozi wake ambaye nilikuwa nikimuombea kwa takribani miaka thelatini na saba kila siku. Usikate tamaa.

9. Soma/Jadili: Tabia Tatu Muhimu za Mwanafunzi wa Kweli (Ukurasa 19). Pata watu watatu wachague tabia mbalimbali na kisha wape nafasi ya **K**ufikiria kwa kina tabia hiyo. Sikiliza wanaposhirikisha **K**uvuta taswiri kwao. Sikiliza wakati wanapoziombea tabia hizo kurudisha kwa Mungu kama maombi yao binafsi katika **K**uabudu, **K**uungama, **K**ushukuru au **K**uomba kwa unyenyekevu.

***Maelezo**:*


- Kwa tafsiri, wanafunzi wote ni wafuasi na wanaojifunza, lakini katika Yohana 8:31 (AMP), **ni wafuasi watii na wanaojifunza tu ndio wanafunzi wa kweli**. Wale wanaorudi nyuma au kuanguka njiani na kamwe wasimfuate Yesu tena siyo wanafunzi wa kweli (Yohana 6:66; 1 Yohana 2:19 NKJV).

- Katika Luka 9:23, njia nzuri ya kuvuta taswira maana ya maneno *"na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake kila siku, na kunifuata"* ni kufikiria kwamba ndani ya mioyo yetu tunacho kiti cha enzi na msalaba. Hizi ni nafasi mbili za pekee katika mioyo yetu, na kuna nguvu mbili ambazo zinataka kutawala juu ya kiti cha enzi: utu wetu wa kale wa dhambi na Roho Mtakatifu. Pale tunapochagua kukiachia kiti cha enzi kwa Roho Mtakatifu, kwa hiyari, kama tendo la utashi wetu, kuna sehemu moja tu kwa utu wetu wa kale wa dhambi kuondoka, na huo ni msalaba. Tunapofanya hivyo, tumejikana wenyewe haki ya kuwa wasimamizi wa maisha yetu, na

tunaishi chini ya udhibiti wa Roho Mtakatifu. **Huu siyo uzoefu wa mara moja katika maisha bali ni lazima ufanyiwe mazoezi wakati wote kila siku.**

***Kielelezo*:**

***Sahihi*** ***Siyo Sahihi***




**RM = Roho Mtakatifu**
**UWKWD = Utu Wetu wa Kale wa Dhambi**

- Mathayo 11:29 (NKJV)—Nira ni kwa ajili ya kufanya kazi. Kwa hiyo, msemo *"Jitieni nira yangu, mjifunze kwangu"* inadokeza kwamba kujifunza na kukua kiroho ni kazi. Tunavuta taswira (Kupiga picha) ya nira, mahali ambapo wawili wanavuta pamoja; na mmoja anayevuta pamoja nasi ni Yesu. Anatubebea mzigo wetu. Tunapaswa kuwa tayari kulipa gharama ili kujifunza na kukua kiroho kwa sababu haya ndiyo mapenzi ya Mungu yaliyodhihirishwa na thawabu katika kutii ni kubwa.

10. Eleza jinsi ya kutumia **Notsi za kila siku katika Kusoma Biblia (NKSKB)** (Kurasa 62 -71) kwa kujadili mfano wa **Notsi za kila siku katika Kusoma Biblia (NKSKB)** (Ukurasa 64).

***Maelezo*:**

- Unapolisoma Neno la Mungu, Mungu anazungumza na wewe moja kwa moja na kukushirikisha kweli ambayo Anataka wewe kuitumia katika maisha yako. Neno la Mungu ni barua Yake ya upendo kwa watoto Wake. Kweli hizi kwa kawaida ni mambo ambayo yanajitokeza kadri unavyolisoma Neno Lake. Katika maeneo mengine ya maisha yako, unaposikia kitu fulani cha muhimu kabisa; kwa kawaida unakiandika ili kwamba usisahau. Je huoni ni muhimu kwamba pale Mungu anapoongea na wewe, unapaswa kuandika ili kwamba usikisahau kile

anachotaka ukikumbuke na kukitekeleza katika maisha yako?

**Mambo sita unayoweza kuyafanya** ili kuweza kufahamu zaidi katika usomaji wako wa Biblia:

1. **Muombe Mungu azungumze** nawe punde kabla hujaanza kusoma.

2. **Uwe makini katika kile unachosoma** na usiruhusu akili yako kutangatanga. Ni vizuri kuwa na kipande kingine cha karatasi ili kuandika mambo ambayo yatakuja akilini mwako ambayo usingetaka kuyasahau. Yanaweza kuwa mambo ya kuongezea katika orodha yako ya "mambo ya kufanya". Baada ya kuyaandika, unaweza kuweka tena umakini katika usomaji wako wa Biblia bila kuogopa kwamba utasahau kitu cho chote ambacho kinaweza kuwa cha muhimu.

3. Wakati unaposoma, **uwe hapo**. Jiweke mwenyewe katika mazingira unayosoma na ufikirie mwitikio wako.

4. **Fanya kuwa yako binafsi**. Vuta taswira kwamba Mungu ameketi karibu na meza uliyopo, akikuangalia machoni, akikuita kwa jina lako, na kusema, "Hili ni kwa ajili yako tu."

5. **Andika mambo ambayo yanajitokeza** kwako ili kwamba usiweze kusahau kile ambacho Mungu amesema.

6. **Tafakari juu ya kile ulichokiandika**.

*Kutafakari katika Notsi za kila siku katika Kusoma Biblia kunatusaidia kumjua Mungu.*

11. Vuta umakini wa wanafunzi katika **Kazi** zao **za Ziada** (Kurasa 243-244).

    ***Soma darasani:*** Ruhusu muda wa kusoma ukurasa 243 kwa sauti darasani na hakikisha kwamba kila mmoja ameielewa kazi ya ziada.

***Soma darasani:*** Sababu mbili za kuwa na muda wako wa utulivu mapema kila asubuhi:

1. **Yesu alituwekea mfano/kielelezo.**

   ***Hata alfajiri na mapema sana****, kukiwa bado kuna giza,* ***Yesu*** *akaondoka, akatoka nyumbani* ***na akaenda zake mahali pasipokuwa na watu akaomba huko*** (Marko 1:35 NIV).

2. **Maandiko yanasisitiza hilo.**

   Maneno ***"kutafuta"*** na ***"mapema"*** katika Isaya 26:9 na ***mapema*** katika Zaburi 63:1 yanatokana na neno la Kiebrania ***shachar***, ambalo linamaanisha **"Kutafuta kwa bidii mapema wakati wa asubuhi."** (*Strong's Exhaustive Concordance of the Bible*, "Hebrew and Chaldee Dictionary," Ukurasa 114, namba 7836)

   Kwa hiyo, mistari hii ingepaswa kutafsiriwa:

   > ***...Nitakutafuta Wewe kwa bidii mapema wakati wa asubuhi...*** (Isaya 26:9).
   >
   > ***...Ee Mungu, wewe ni Mungu wangu, nitakutafuta wewe kwa bidii mapema alfajiri...*** (Zaburi 63:1).

12. Funga kwa Maombi.

    ***Mfano:*** Waalike wanafunzi kupiga magoti pamoja nawe mnapoomba pamoja na kumshukuru Mungu kwa kukutana nawe na kipekee kuzungumza na kila mmoja wenu.

## Mwongozo wa Kiongozi na Ujumbe wa Mwandishi........................Kipindi cha 3

1. Anza kwa maombi.

   ***Mfano**:* Waalike wanafunzi kupiga magoti pamoja na wewe mnapoomba pamoja na kuutoa muda kwa Mungu. Katika majuma machache yajayo utawataka wanafunzi kuomba wakiwa wamefungua macho yao wakiwa wanatembea, wamesimama, wanaendesha, n.k. lakini unawataka kuelewa kwamba ni muhimu kupiga magoti yao na kuomba kila wanapoweza kufanya hivyo.

2. Mtake kila mmoja kufungua kwenye karatasi ya **Ufuatiliaji** ya siku hiyo. Kisha **kazikagua** na **kuzisaini** (Ukurasa 274).

   ***Uwajibikaji**:* Ukaguzi na uwekaji sahihi karatasi zao za Ufuatiliaji kila juma huwafundisha wanafunzi katika kanuni ya uwajibikaji iliyofundishwa katika Warumi 14:12. Pia inakusaidia wewe kama kiongozi kuona kama wanafunzi wako:

   - Wanafanya kazi za ziada na kujijengea mtindo wa maisha au
   - Wanahitaji kuhamasishwa au kutiwa moyo na wewe.

3. Soma **"Kwa kuwa Kusudi langu la dhati ni kwamba Nimjue Yeye"** (Ukurasa 9-10). Mtake mtu mmoja kushirikisha Kuvuta taswira kwake sehemu moja ya mstari huu na kumsikiliza pale anaporudisha Maombi yake kwa Mungu kama maombi binafsi ya **K**uabudu, **K**uungama, **K**ushukuru au **K**uomba kwa unyenyekevu.

   ***Andika*** nukuu hii katika ukurasa wa 9:

   > "Uzoefu wa kiwango cha juu katika maisha ni kumjua Mungu."
   >
   > —Billy Graham

   ***Maelezo**:* Waonyeshe wanafunzi Ukurasa wa 10, na tambua umakini wao jinsi msitari ulivyogawanyika katika sehemu nne:

   - Wahamasishe kuchukua sehemu moja kati ya nne za mstari kuitafakari kila siku.

- Kisha sikiliza mmoja wa wanafunzi **A**napofikiria kwa kina, **V**uta taswira na **K**uombea sehemu moja ya mstari tena kwa Mungu.

4. Jadili **Maswali ya Marudio ya Kazi ya Ziada** (Ukurasa 244).

   ***Maelezo**:*

   - Watake watu mbalimbali katika kundi kujitolea kusoma moja ya maswali na kushirikisha majibu yao.

   - Baada ya mtu mmoja kuwa amesoma swali la 6 katika ukurasa 244 na ameshirikisha uzoefu, wahamasishe wanafunzi kuzungumza kwa wengine juu ya Yesu na mambo aliyowafundisha.

5. Soma/jadili **Baadhi ya Sifa ambazo Mwanafunzi wa Kweli Anapaswa Kuziendeleza katika Maisha yake** (Ukurasa 20). Watake watu wanne kuchagua sifa mbalimbali, na kisha watake kuzifikiria kwa kina sifa hizo. Wasikilize watakapo shirikisha kuvuta taswira kwao. Sikiliza wanapoombea tena sifa zao kuzielekeza kwa Mungu kama maombi yao binafsi ya **K**uabudu, **K**uungama, **K**ushukuru au **K**uomba kwa unyenyekevu.

   ***Maelezo**:*

   - Mathayo 22:37 (NKJV)—Haya ni maneno ya Yesu. Anazungumzia juu ya kumpenda Mungu kwa moyo wote. Tunapaswa kumpenda Yeye kwa utu wetu wote na tena kuliko mtu yeyote au kitu kingine cho chote katika maisha. Tunapaswa kujitoa na kujiachalia kikamilifu kwa Mungu.

     ***Hadithi**:* Kwa miaka mingi tumekuwa na mbwa wengi, lakini hakuna aliyeonyesha upendo na furaha kama mmoja wao mwenye asili ya Uingereza. Mara kwa mara aliketi dirishani kwetu akitusubiri tu apate kuniona, bwana wake. Mara aliponiona mimi, alianza kukwaruza kwaruza kwa kucha na meno yake kuonyesha furaha kamili. Kusingekuwa na namna ambavyo ungekosea kwamba alinipenda kwa dhati. Moyo wake ulinielekea mimi.

    - Mungu anastahili kutoka kwetu tumpende kwa mioyo yetu yote. Inapaswa kudhihirika kwa kila mtu kwamba mioyo yetu ni mali ya Mungu.

- Mdo 17:11 (RSV)—Hapa tunaona kundi la watu wakiwa na shauku ya kuijua kweli na walio radhi kuitumia na kuigundua kweli wao wenyewe. Walikuwa wazi na walikuwa tayari kufundishwa.

- Mathayo 11:28 (AMP)—Maneno, *"Njoni kwangu"* ni mwaliko wa upendo wa kuja kwa Yesu. Sasa ni wakati kwa ajili yetu kuitikia na kupatikana na kuukubali mwaliko wake.

- Mathayo 11:29-30 (AMP)—inajumuisha baadhi ya maneno na misemo inayovutia:

    - *Nira*—Nira ni kwa ajili ya kuwaunganisha wanyama ili kwamba kazi iweze kufanyika, lakini mpaka pale mnyama anapokuwa amevunjwa kwa nira, hatakuwa na manufaa kwa Bwana wake. Ikiwa tunataka Mungu kututumia, ni lazima tukubali wenyewe kuwepo kujifunza, na ni lazima tuwe na utayari kuvunjwa kwa nira. Mtoa hoja mmoja anasema, "Nira ni laini na si nzito kwa sababu inakubaliana na upendo wa Mungu."

    - *"Jifunzeni kutoka kwangu"*—Katika mstari wa 28 tumeaambiwa tumwendee Yesu na hapa katika mstari wa 29 tumeambiwa kwa nini. Sababu inayotufanya kwenda kwake ni kukaa miguuni Pake na kujifunza kutoka Kwake.


    - *Mpole*—Neno *mpole* katika mstari 29 halimaanishi "udhaifu." Katika nyakati za wafalme na makasiri pale wanaume walipopigana juu ya mgongo wa farasi, farasi dume mwenye nguvu waliyemwendesha aliitwa mpole kwa sababu neno mpole lilimaanisha "nguvu iliyo chini ya udhibiti". Yule mmiliki wa farasi alikuwa ameshika hatamu. Na Bwana wetu Yesu, naye ameshika hatamu ya maisha yetu, tuwe wanaopatikana kwake ili kwamba aweze kutufundisha na kututumia kama apendavyo mwenyewe.

- Luka 9:23—Kama mtu hayuko tayari kujikana mwenyewe, hatakuwa tayari kujitoa ili kujifunza.

    ***Marudio:*** Njia nzuri ya kuvuta taswira ya nini kifungu hiki kilimaanisha *"...na ajikane mwenye na kuubeba msalaba wake kila siku na anifuate Mimi"* ni kufikiria kwamba katika moyo wako unacho kiti cha enzi na msalaba. Hizo ndizo nafasi mbili pekee katika moyo wako, na kuna nguvu mbili ambazo zinataka kutawala juu ya kiti cha enzi: Utu wako wa kale wa dhambi na Roho Mtakatifu. Pale unapochagua, kukiachia kiti cha enzi kwa Roho Mtakatifu kwa hiyari, kama tendo la utashi wako, kuna sehemu moja tu kwa ajili ya utu wako wa kale wa dhambi kwenda, na hapo ni msalabani. Pale unapofanya hili, umejikana mwenyewe haki ya kuwa msimamizi katika maisha yako mwenyewe, na unaishi chini ya udhibiti wa Roho Mtakatifu. **Huu si uzoefu wa mara moja katika maisha yako bali ni lazima ufanyiwe mazoezi wakati wote kila siku.**

***Kielelezo:***

***Sahihi*** ***Siyo Sahihi***




**RM = Roho Mtakatifu**
**UWKWD = Utu Wetu wa Kale wa Dhambi**

6. Hakiki au tathmini **Changamoto za Kutafakari** (Kurasa 75-78).

    ***Marudio:*** Kutafakari ni namna tunavyoihamisha kweli kutoka vichwani mwetu kwenda mioyoni mwetu. Kamwe kweli haitafanya kazi inavyopaswa katika utekelezaji mpaka inapofika moyoni. Kwa hiyo, **kutafakari ni muhimu katika utendaji** (Yoshua 1:8).

- Wakati mwingine Wakristo wanakuwa inchi kumi na mbili mbali na kuyaishai maisha ya Kikristo yenye

mafanikio—umbali kati ya kichwa na moyo. Kwa nini? Kweli nyingi tunazofikiri tumejifunza zipo tu akilini mwetu na hazijawahi kuhamia kwenda mioyoni mwetu kupitia kutafakari. Kwa hiyo, hatufurahii au kuona tunda ambalo huja kutokana na utendaji pale kweli inapokubalika na kupokelewa katika mioyo yetu kwa njia ya kutafakari.

- ***Kwa Mfano:*** Daudi alikuwa bingwa katika kuyatumia maandiko na kuyaombea kwa kuyarudisha tena kwa Mungu kama maombi yake binafsi, ambayo ni sehemu ya muhimu katika kutafakari. Maombi binafsi kutoka katika moyo wa Daudi katika Zaburi 60:10-12 yanaakisi **K**ufikiria kwa kina na **K**uvuta taswira kwake kile Mungu alichokuwa akisema naye katika Yoshua 7:12.

*Kutafakari maandiko kunatusaidia kumjua Mungu.*

7. Kuhakiki au Kutathmini **Changamoto za Maombi** (Kurasa 81-82).

***Wakumbushe*** Wanafunzi:

- 1 1Wathesalonike 5:16-18 (RSV) inaelezea angalau sehemu ya mapenzi ya Mungu kwetu kuhusiana na maombi:
    - Furahini siku zote.
    - Ombeni bila kukoma.
    - Mshukuruni Mungu kwa kila jambo.
- Maombi yanatakiwa kuwa jambo la kawaida kama ilivyo kupumua au kula.
- Kila mwanafunzi wa kweli wa Yesu anapaswa kuwa na maisha ya maombi yenye ufanisi.

***Maelezo:*** Kusudi mojawapo la kutumia herufi hizi **K-K-K-K** ni kutusaidia kutambua jinsi maisha yetu ya maombi yanavyoweza kuwa nje ya uwiano na kutuonyesha jinsi ya kuyaweka katika uwiano. Yamkini 99% ya maombi yetu ni sala au kumwomba Mungu kwa ajili ya kitu fulani. Biblia inatuambia tuombe, lakini pia inatufundisha kuonyesha kuabudu kwetu na kumshukuru Mungu, vile vile kukubaliana na Mungu kwamba tumetenda dhambi na h ivyo tunapaswa kuungama dhambi zetu. Jinsi gani unafikiri Mungu ataitikia ikiwa zaidi ya nusu ya maombi yetu ni kuonyesha kuabudu kwetu na kumshukuru Yeye?

***Kielelezo:*** Mzazi anaweza kuvunjika moyo ikiwa mtoto wake siku zote anamwomba kwa ajili ya jambo fulani lakini kamwe haonyeshi upendo au shukrani kwa mzazi.

8. Jadili **Notsi za kila siku katika Kusoma Biblia (NKSKB)** (Ukurasa 65-72) walizofanya wanafunzi kwa juma hili lililopita. Watake baadhi yao:

    a. **Kushirikisha** moja ya Notsi zao.

    **b. Kufikiria kwa kina** juu ya notsi.

    **c. Kuvuta taswira ya** notsi hizo.

    > **Wakumbushe** wanafunzi kwamba kuvuta taswira ya notsi hakumaaminishi kuzielezea notsi. Watake wanafunzi waanze kwa kusema: **"Hii ndiyo picha ninayoiona."**

    d. **Ombea** notsi hizo kwa Mungu kama maombi binafsi katika **K-K-K-K**. Baada ya wanafunzi ku**maliza kushirikisha, uwe mhamasishaji/mtia moyo**.

    *Kusoma Neno la Mungu, kutengeneza notsi na kutafakari katika notsi hizo hutusaidia kumjua Mungu.*

9. Soma/jadili **Dondoo za Kukusaidia** (Ukurasa 63).

    ***Maelezo:*** Itakuwa busara kwa wanafunzi kukumbuka maswali haya manne kwenye ukurasa wa 61 akilini mwao wanaposoma Neno la Mungu, kwa hiyo, wahamasishe kufungua nyuma na kurejea ukurasa huu mara kwa mara.

10. Soma/jadili Changamoto za Kujifunza Biblia Kila Siku (Ukurasa 89-90).

    ***Wakumbushe*** wanafunzi kwamba kuanzia kesho wataanza **Kujisomea** sehemu ya kijitabu kidogo cha Mwanafunzi katika muda wao wa utulivu.

    - Taarifa tunazozipata kutoka kwenye kujifunza Biblia ni maarifa tu ya kichwani au ridhaa ya akili (weledi) mpaka tunapotafakari juu ya kweli tuliyoigundua.
    - Kutafakari ni kwa muhimu katika utekelezaji. Kupitia kutafakari Mungu anatubadilisha na kutuweka huru.

    *Kutafakari juu ya kweli tunazozipata katika kujifunza au kujisomea Biblia hutusaida kumjua Mungu.*

11. Soma/jadili na kutafakari juu ya **(KKK)** kweli katika **Unapata Wapi Heshima na Umuhimu Wako**? (Kurasa 44-46)

***Maelezo:*** Pale tunapoelewa kwa nini tuna uthamani na umuhimu, ni rahisi kudumisha mtazamo wa Mungu katika maisha yetu.

***Hadithi:*** Mchungaji mmoja huko Amerika alikua bila kuelewa nini kilimfanya yeye wa muhimu. Alipokuwa mtoto wa miaka mitano, baba yake na wajomba zake walipenda kumwangalia akicheza muziki. Walijikusanya kumzunguka, na ili mradi alicheza, walirusha pesa sakafuni kwa ajili yake. Halikuonekana kama ni jambo lenye madhara, lakini mapema katika maisha alianza kufikiria kwamba alikuwa na umuhimu pale tu alipofanya onyesho, na hili likawa tatizo kwake baadaye katika maisha.

- ***Maelezo:***
    - Miaka elfu mbili iliyopita kabla hatujazaliwa na wala hatukuwa na namna yoyote ya kufanya kuthibitisha uthamani wetu, Yesu alikufa msalabani kwa ajili ya dhambi zetu na kuthitibitisha kwamba sisi ni watu wa muhimu Kwake.
    - Hapa tunaiona picha nzuri. Tunajua kwamba ndani yetu na sisi wenyewe hatuna stahili, thamani au umuhimu., lakini kama tendo la upendo, neema na rehema, **Mungu alipendezwa** kwamba tuwe na stahili, thamani na umuhimu. Kisha **Akalithibitisha** hilo kwa kuchukua nafasi yetu pale msalabani na kufa kwa ajili ya dhambi zetu. Jinsi gani Mungu alivyo wa ajabu!

        ***Kielelezo:*** Karatasi ambayo pesa inachapishwa ni ya thamani ya chini, lakini pale thamani inapokuwa imeongezewa na watu walio na mamlaka, inakuwa na thamani. Kwa namna hiyo hiyo Mungu, ambaye anamiliki nguvu na mamlaka yote, hutuongezea thamani. Hiyo humfanya kila mmoja wetu kuwa mtu anayefaa, wa thamani na wa muhimu.

***Muhtasari*** wa kwa nini sisi ni wa muhimu:

- **Mungu alipendezwa na hilo**—Mungu alipendezwa au kukusudia kwamba tuwe watu wa muhimu tangu mwanzo.

    - Efeso 1:4 (WEY—*Agano Jipya katika Lugha ya Kisasa* na Richard Francis Weymouth) – *"Alituchagua sisi tuwe watu wake katika Kristo kabla ya kuumbwa ulimwengu..."*

    - 2 Wathesalonike 2:13 (NIV)—"*Kwa kuwa Mungu amewachagua tangu mwanzo mpate wokovu, katika kazi ya kutakaswa ya Roho, na kupitia kuiamini kweli.*"

- **Mungu analithibitisha hilo—**katika nyakati tatu (wakati uliopita, uliopo na ujao).
    - **Uliopita**—Miaka 2000 iliyopita Mungu alithibitisha kufaa, thamani na umuhimu wetu kwa kumruhusu Mwanaye, Yesu Kristo, kufa juu ya msalaba kwa ajili ya dhambi zetu.

        - Yohana 3:16 (NKJV)—"*Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanaye wa pekee, ili kila amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele."*

    - **Wakati uliopita, uliopo na ujao**—Mungu anathibitisha umaana, uthamani, na umuhimu wetu katika njia ya upendo ambayo anatuonyesha katika Neno Lake.

        - Isaya 43:4 inathibitisha kwamba Mungu anaongezea umaana, uthamani na umuhimu kwetu na kwamba anatupenda:

            - *"Kwa kuwa ulikuwa na thamani machoni pangu, na mwenye kuheshimiwa, nami nimekupenda."* (RHM— Rotherham)
            - *"Kwa sababu ya thamani yako machoni pangu, umeheshimiwa na kupendwa nami..."* (BBE—*Bible in Basic English*)
            - *"Umethaminiwa sana, umeheshimiwa sana, umependwa sana..."* (Knox)

- Kumbukumbu ya Torati 7:6 inathibitisha kwamba Mungu huongeza umaana, thamani, na umuhimu kwetu kwa kututambulisha kama:
    - *"Miliki yake ya thamani"* (Moffatt)
    - *"Watu wake aliowathamini"* (TOR—*Torati: Vitabu Vitano vya Musa*)
- **Wakati uliopita, uliopo na ujao**—Mungu anathibitisha umaana, uthamani na umuhimu wetu katika ukweli kwamba anayo mipango mizuri kwa ajili ya maisha yetu:
    - Yeremia 29:11 (LIV)—*"Maana nayajua mawazo ninayowawazia ninyi, asema Bwana, ni mawazo ya amani wala si ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho."*

12. Vuta umakini wa wanafunzi kwa **Kazi** zao **za ziada** (Kurasa 245-246).

    ***Soma darasani:*** Ruhusu muda wa kusoma ukurasa 245 kwa sauti darasani na hakikisha kwamba kila mtu anailewe kazi ya ziada.

    - ***Wahamasishe kuwa waaminifu kwa Mungu na kukutana Naye kila siku katika muda wao wa utulivu.***

13. Funga kwa maombi.

    ***Kielelezo:*** Waalike wanafunzi kupiga magoti pamoja nawe wakati unaomba na mshukuru Mungu kwa ajili ya kukutana nao na kipekee kuzungumza na kila mmoja wenu.

## Mwongozo wa Kiongozi na Ujumbe wa Mwandishi........................Kipindi cha 4

1. Anza kwa Maombi.

    ***Mfano**:* Waalike wanafunzi kupiga magoti pamoja na wewe mnapoomba pamoja na kuutoa muda kwa Mungu. Katika majuma machache yajayo utawataka wanafunzi kuomba wakiwa wamefungua macho yao wakiwa wanatembea, wamesimama, wanaendesha, n.k. lakini unawataka kuelewa kwamba ni muhimu kupiga magoti yao na kuomba kila wanapoweza kufanya hivyo.

2. Mtake kila mmoja kufungua katika karatasi ya **Ufuatiliaji** ambayo inahitajika siku hiyo. Kisha unaweza **kuzikagua na kuzisaini** (Ukurasa 275).

    ***Uwajibikaji**:* Ukaguzi na uwekaji sahihi karatasi zao za Ufuatiliaji kila juma huwafundisha wanafunzi katika kanuni ya uwajibikaji iliyofundishwa katika Warumi 14:12.

3. Soma **"Kwa kuwa Kusudi langu la dhati ni kwamba Nimjue Yeye"** (Ukurasa 8-9). Mtake mtu mmoja kushirikisha Kuvuta taswira kwake sehemu moja ya mstari huu na kumsikiliza pale anaporudisha Maombi yake kwa Mungu kama maombi binafsi ya **K**uabudu, **K**uungama, **K**ushukuru au **K**uomba kwa unyenyekevu. Wakumbushe wanafunzi kuweka mtazamo wao kwa Yesu (Waebrania 12:2).

    - Watake wanafunzi **kuandika** mawazo haya katika ukurasa wa 9:

        - Kutoka 33:13—Musa alidhamiria kumjua Mungu.

        - Yohana 10:14 (NIV)—Yesu alisema, *"Kondoo wangu wananijua Mimi."*

    - ***Hadithi**:* Kusudi la dhati la Paulo lilikuwa kumjua Yesu. Nini mtazamo wetu juu ya kumjua Yesu leo? Ninapofikiria juu ya hili, inanikumbusha akilini mwangu mbwa watatu wawindaji wakongwe. Waliokuwa tofauti kabisa. Kwangu mimi, wanawakilisha **mitazamo** mitatu **tofauti** kati ya mingi ambayo Wakristo wanayo leo juu ya kumjua Yesu, kukua kiroho na kumtumikia Yeye.

Mbwa mmoja alikuwa kiashirio ambaye wakati wote **alinitazama mimi kutoka mbali**. Hatukuufurahia ushirika wa karibu kwa sababu hakuvutiwa nami katika kuwa na ushirika naye, mimi bwana wake. Alikuwa na ajenda yake, na haikunijumuisha mimi isipokuwa nimemchukua kwenda kuwinda, hilo ndilo jambo alilotaka kulifanya. Je huyu anaweza kulingana na baadhi ya Wakristo?

Mbwa wa pili alikuwa wa Kijerumani mwenye kiashirio cha manyoya mafupi, na alipenda kuwa karibu nami kwa muda mfupi lakini muda wake mwingi aliutumia nje ya upeo wangu. Ningeweza kumpapasa mara moja au mara mbili na alikuwa ameshaondoka. Hakuvutiwa na chochote isipokuwa aina ya ushirika wa "kuingia na kutoka". Hata huko nyuma ya nyumba ambako tungelikuwa na muda kwa ajili yetu kufahamiana, hakuvutiwa kabisa. Kwa hiyo ushirika wetu ulikuwa kidogo na usio na maana sana. Je huyu haonekani kama baadhi ya Wakristo?

Mbwa wa tatu alikuwa mdogo wa Kiingereza wa kuwindia, na alikuwa akifurahishwa sana nasi. Alituletea furaha kubwa kwa sababu siyo tu alitaka kunitumikia mimi kwa moyo wa hiyari tulipokuwa tukiwinda pamoja, tena mara kwa mara alionyesha upendo wake kwangu na kwa familia nzima. Alisimama mlangoni akinitazama tu, na pale aliponiona, alisisimuka sana hata asingeweza kusimama kimya. Aliishi kwa ajili ya muda wetu wa pamoja, na tulikuwa na ushirika mzuri. Ninafurahi kusema kwamba maisha yetu yameguswa na baadhi ya Wakristo ambao walionyesha aina hii ya upendo na kujitoa kwa Kristo.

Mungu anatupenda na anautamani ushirika wetu, lakini hataweza kulazimisha ushirika huo juu yetu. Ni muda muafaka kwetu sisi kuukubali ushirika huo.

***Marudio**:* Waonyeshe wanafunzi ukurasa 10, na tafuta kujua umakini wao wa jinsi mstari ulivyogawanyika katika sehemu nne:

- Wahamasishe kuchukua moja ya sehemu hizo nne ya mstari kuutafakari kila siku.
- Kisha msikilize mmoja wa wanafunzi Akifikiria kwa kina, Akivuta taswira, na Akiombea sehemu moja ya mstari kwa Mungu**.**

***Uchunguzi:*** Wakati mwingine pale wanafunzi wanapoanza kutendea kazi kanuni za kiroho kama kusoma Biblia, Ku-

jifunza Biblia, Kushika maandiko, kutafakari na kuomba, wanakosea na kuanza kuweka mtazamo katika kanuni hizo kuliko Yesu na Yesu pekee yake. Matokeo ni kwamba baadhi yao huanguka njiani na kutokuwa na ufanisi kwa ajili ya Mungu. Kwa hiyo, tutahakiki au tutauchunguza mstari huu kila juma kwa sababu kuu tatu:

1. **Ili kuyaweka macho yetu kumwelekea Yesu** na Yesu pekee yake na kutukumbusha kwamba **kusudi letu la dhati ni kumjua Yeye**.
2. Ili kutukumbusha kwamba **kanuni zenyewe zilivyo siyo mwisho. Ni njia tu ambazo Mungu ametupatia ili tumjue Yesu** kwa kina, kwa undani na kibinafsi. Kwa hiyo, tunafanya mazoezi ili kwamba tuweze kumjua Yeye.
3. **Kutafakari juu ya kweli zenye nguvu** katika mstari huu ili kwamba ziweze kuhama kutoka kwenye ukurasa kwenda vichwani mwetu na kisha kwenda mioyoni mwetu **ili kwamba tuweze kubadilishwa katika mfano wa Yesu, aliye kioo kinachoakisi mng'aro wa utukufu wa Bwana**.

4. Jadili **Maswali ya Marudio ya Kazi za Ziada** (Ukurasa 246).

   ***Maelezo:***

   - Tumia swali la 4 katika ukurasa wa 246 kuwahamasisha wanafunzi kuzungumza juu ya Yesu na mambo anayowafundisha.
   - Mtake mmoja katika kundi kueleza uzoefu wa juma lililopita pale alipoongea na mtu fulani juu ya Yesu au kushirikisha jambo fulani ambalo Mungu anamfundisha yeye.

5. Jadili **Notsi za kila siku katika Kusoma Biblia (NKSKB)** (Kurasa 65-72) walizoziandaa wanafunzi juma lililopita. Watake baadhi yao:

   a. **Kushirikisha** moja ya notsi zao.

   b. **Kufikiria kwa kina** juu ya notsi hizo.

c. **Kuvuta taswira ya notsi hizo**.

***Wakumbushe*** wanafunzi kwamba kuvuta taswira ya notsi hakumaanishi kuzielezea notsi. Waambie waanze tu kwa kusema, **"Hii ni picha ninayoiona."**

d. **Kuombea** notsi hizo kwa Mungu kama maombi binafsi ya **K-K-K-K.** Baada ya wanafunzi kumaliza kushirikisha, uwe mhamasishaji (Mtiaji moyo)**.**.

***Waeleze*** wanafunzi kwamba hawatakiwi kukuambia nini *wata*kiombea lakini wanapaswa kuomba *hasa* na kukuruhusu wewe na wanaobaki kwenye kundi kumsikiliza pale wanapoongea na Mungu.

*Kutafakari katika Notsi zetu za Usomaji wa Biblia kila Siku hutusaidia kumjua Mungu.*

6. Soma/jadili kwa kina mafunzo ya **Kumruhusu Yesu Kristo kuwa Kitovu na Bwana wa Maisha Yangu** (Kurasai 91-96). Kadri unavyosoma na kujadili, mara kwa mara simama na kuwapa wanafunzi fursa ya **K**ufikiria kwa kina, **K**uvuta taswira na **K**uomba.

***Ukurasa 91:***

- ***Andika*** juu kwenye ukurasa—*Mambo mawili magumu zaidi katika maisha ya Kikristo*:

  1. ***Uwiano—****Ufunguo wa uwiono ni Kristo kuwa Kitovu kwako.*

     ***Elezea—***Watu wengi wanafikiri kuwa uwiano ni kuugawanya muda wao vizuri kati ya familia, kazi, kanisa, burdani, n.k. Kwa Mungu, uwiano unajitokeza pale Kristo anapokuwa kitovu cha maisha yetu na kila kitu katika maisha yetu kimhusishe Yeye.

     ***Kielelezo***—Miaka kadhaa iliyopita ulipolipeleka gari lako kusawazisha matairi, mafundi walitoa tairi nje ya gari na kuliweka kwenye mashine. Kitu cha kwanza walichotakiwa kufanya kabla hawajasazawazisha tairi lilikuwa kuliweka tairi katikati ya mashine. Ndivyo ilivyo katika maisha ya Ukristo. Hakuna tumaini kamwe la usawa na uwiano katika maisha

yetu isipokuwa tunaanza kwa kumruhusu Yesu Kristo kuwa kitovu cha maisha yetu na katika yeye vitu vingine vyote vinahusishwa. Wakati familia zetu, kanisa, kazi, burdani na jambo lingine lolote katika maisha yetu linahusishwa kwa karibu na Yesu, basi tuko kwenye njia sahihi kupata uzoefu wa uwiano (usawa) kama Mkristo.

2. ***Ulinganifu—****Ufunguo wa kuwa na ulinganifu ni kutawaliwa na Kristo.*

   ***Elezea—***Ulinganifu unatokea pale tunapojifunza **kujiachilia** katika udhibiti wa Roho Mtakatifu na **kukaa** (kuishi) chini na uongozi Wake.

   ***Fikria juu ya hilo***—Wakati Yesu alipoishi hapa duniani, alikuwa thabiti na hakufanya dhambi, na anapokuwa katika udhibiti wa maisha yetu, sisi pia hatutatenda dhambi. Maisha yetu ni vioo amabavyo kupitia hivyo ama ni utu wetu wa dhambi wa asili au Kristo anaakisiwa, kutegemea na nani yupo kwenye udhibiti.

   - Paulo anaelezea matatizo yetu kwa uthabiti kwa kushirikisha uzoefu wake binafsi:

     - Warumi 7:15 (NIV)—*"Maana sijui nifanyalo, kwa sababu lile nilipendalo, silitendi; bali lile nilichukialo ndilo ninalolitenda."* Paulo anasema kwamba Kristo anapokuwa siyo mdhibiti, haiwezekani kumuakisi Kristo na kuishi maisha ya Ukristo yenye uthabiti.

   - Tatizo letu ni kwamba tunaendelea kukwapua udhibiti wa maisha yetu kutoka mikononi mwa Mungu baada ya kuwa tumeuachia udhibiti huo kwa Mungu. Katika tendo hilo tu, tunafanya dhambi, ambayo huharibu ushirika wetu na Mungu na kutufanya kutokuwa madhubuti katika mwenendo wetu wa Kikristo.

     - Tutalizungumza zaidi juu ya hili baadaye.

*Ukurasa 92:*

- Maneno yasemayo “Nijiachilie kwa hiyari katika udhibiti wa Mungu” katika mstari wa kwanza wa kifungu (para) cha kwanza inatufanya sisi kukabiliana na uamuzi wa muhimu: Nani nitamruhusu kuwa msimamizi au mtawala katika maisha yangu leo—Mungu au mimi mwenyewe?

- Watake wanafunzi kuandika rejea hizi zenye nguvu zinazokubaliana (unga mkono) licha ya Wakolosai 1:15-19 (LIV):

  - Yohana 5:23; Tito 2:13; Wafilipi 2:6; Yohana 20:28; Wakolosai 2:9; Yohana 10:30; Yohana 1:3.

**Kwa nini nimruhusu Yesu Kristo kuwa Kitovu na Bwana wa maisha yangu?** (Kurasa 92, sehemu II Ukurasa 97)

*Ukurasa 93:*

- Baada ya mtu mmoja kuwa amesoma kwa sauti sehemu ya C katika ukurasa huu, simulia hadithi ifuatayo:

  ***Hadithi:*** 1 Wakorintho 6:20 (NLT)—*“...Mungu alikununua kwa gharama kubwa...”* Hii ni hadithi ya mvulana mdogo aliyeishi katika kijiji ukingoni mwa ziwa kubwa. Mvulana huyu mdogo alitengeneza kimtumbwi kidogo na kwa furaha kubwa akakichukua kwenda ziwani na kukiweka juu ya maji kukiangalia kikielea. Wakati alipokuwa akiangalia kiliteleza kukatisha maji, dhoruba kubwa ikaja, ikabeba matanga, na kukichukua kimtumbwi katikati ya ziwa na asikoweza kukiona. Yule mvulana mdogo alivunjika moyo.

  Siku chache baadaye alipokuwa akitembea kijijini kwake alipita kwenye duka na kuona kimtumbwi chake dirishani. Kwa furaha kubwa, alikimbia kuingia ndani na kusema kwa mwenye duka, “Bwana, huu ni mtumbwi wangu uliopo dirishani! Niliutengeneza mtumbwi huo!”

  Mwenye duka alisema, “Samahani, lakini nilimlipa mvulana mwingine mdogo kiasi cha pesa kwa ajili ya mtumbwi huo, kwa hiyo kama unautaka, utatakiwa kunilipa mimi.”

Yule mvulana mdogo alikimbia nyumbani na kuvunja kibubu chake. Pesa mkononi, alirudi kwenda dukani na kuweka fedha iliyotakiwa mezani. Mwenye duka alikwenda dirishani kuuchukua ule mtumbwi na kumpa yule mvulana mdogo. Mvulana mdogo kwa upendo aliuchukua mtumbwi mikononi mwake, na alipokuwa akitoka mlangoni, alisema hivi, "Sasa wewe ni wangu mara mbili. Nilikutengeza na nikakununua."

Hii ni picha nzuri ya kile Yesu alifanya kwa ajili yetu. **Alituumba na Akatununua.**

***Ukurasa 94:***

- Watake wanafunzi **kuandika** maandiko ya rejea yenye nguvu yanayosaidia:
    - Licha ya Isaya 45:22 (NKJV), **andika** rejea hii, K/Torati 7:9 (NKJV), ambayo linasema, *"...Bwana Mungu wako, Ndiye Mungu."*
    - Licha ya Yohana 10:30 (NKJV), **andika** rejea kutoka Tito 2:13 (NKJV), ambayo linasema, *"..... Mungu wetu mkuu na Mwokozi Yesu Kristo."*

***Ukurasa 95:***

- Baada ya kusoma ukurasa huu na kuruhusu baadhi ya wanafunzi, **K**ufikiria kwa kina, **K**uvuta taswira na **K**uomba tena kwa Mungu baadhi ya maandiko haya:
    - Waombe wanafunzi **kuandika** yafuatayo kulia katika sehemu ya notsi pembeni ambako uliijaza sehemu iliyo wazi kwa neno *MTAWALA* chini yake 1 Timotheo 6:15 (JBP):

        Mungu ni mdhibiti mwenye nguvu katika mambo yote; kwa hiyo, hakuna kinachogusa maisha yetu isipokuwa kile kinachoruhusiwa na Mungu. Kama Mungu atakiruhusu, basi ameahidi kwamba kwa kuwa tunampenda Yeye na tumeitwa kwa kusudi lake; Atahakikisha kwamba mambo yote yanafanya kazi kwa ajili ya kutupatia mema (Warumi 8:28).

***Ukurasa 96:***

- Waombe wanafunzi **kuandika** pembeni mwa 2 Timotheo 2:13 (NKJV) maneno yafuatayo:

    *Mungu lazima atatimiza ahadi Zake.*

    - Sehemu ya tabia ya maadili ya Mungu ni kwamba ni mwaminifu. Hawezi kutokuwa mwaminifu kwa sababu hawezi kujikana mwenyewe jinsi alivyo. Kwa hiyo, ni lazima atatimizia ahadi. Tarajia hilo.

        - Fikiria juu ya baraka ambazo ni zetu kwa sababu Mungu ni mwaminifu. Tunajua kwamba kama tuna uaminifu kwa 99.99%, hii inamaanisha hatuna uaminifu. Uaminifu unamaanisha 100% na hilo linamaanisha kwamba Mungu siku zote atafanya kile Alichoahidi kufanya. Tarajia hilo.

- Waombe wanafunzi **kuandika** maelezo haya chini ya ukurasa huu:

    *Kwa hiyo, kujiachilia katika Utawala Wake, kukaa ndani Yake na kumruhusu Yeye kuwa msimamizi katika maisha yako.*

***Ukurasa 97:***

- Waombe wanafunzi **kuandika** maelezo haya pembeni mwa herufi D:

    *Haya ni maisha ya imani, kumwamini Mungu na kuishi chini ya udhibiti wa Roho Mtakatifu.*

- Waombe wanafunzi **kuandika** maswali haya sehemu ya chini ya ukurasa huu:

    1. Je, utamruhusu Yesu kuwa kitovu na Bwana wa maisha yako leo?

    2. Je, utamruhusu Yesu kuwa mtawala wa maisha yako leo?

*Kutulia ili kutafakari juu ya kweli tulizojifunza katika Mafunzo yetu ya Biblia kunatusaidia kumjua Mungu.*

7. Soma/jadili na kutafakari juu ya Kweli za (**KKK**) katika **Jitie Nguvu katika Bwana** (Kurasa 33-36). Wakumbushe

**K**ufikiria kwa kina na **K**uvuta taswira juu ya kweli hizi (**KKK**) mara kwa mara.

***Maelezo:*** Baada ya kuwa umesoma nukuu ya Charles Swindoll kwenye ukurasa wa 36, simulia hadithi ifuatayo:

***Hadithi:*** Miaka kadhaa iliyopita kiwanda cha viatu kilimpeleka mfanyakazi wa idara ya masoko kwenda Afrika. Mfanyakazi huyu alishuka kutoka kwenye mashua na kuona kwamba hakuna mtu aliyevaa viatu, mara moja aliwasiliana na kampuni yake na kusema, "Nitumieni fedha ili nirudi nyumbani, hakuna mtu hapa anayevaa viatu". Mfanyakazi huyu wa idara ya masoko aliona mazingira yasiyowezekana au hali isiyowezekana.

Muda mfupi baadaye kampuni hiyo hiyo ilimpeleka mfanyakazi mwingine wa masoko kwenda Afrika. Mfanyakazi wa pili aliposhuka mashuani na kuona kwamba hakuna mtu aliyevaa viatu; ghafla aliwasiliana na kampuni yake na kusema, "Nitumieni mashua iliyojaa viatu, hapa hakuna mtu anayevaa viatu." Mfanyakazi wa pili aliona fursa kubwa.

Wafanyakazi wote wawili waliona jambo linalofanana, lakini mmoja aliona kutokuwezekana na mwingine aliona fursa kubwa.

- Je, tunayaona maisha yetu yamejaa hali ya kutokuwezekana au kujaa kwa fursa kubwa?
- Sisi wote tunahitaji kutiwa moyo katika maisha yetu katika nyakati fulani, kwa hiyo, "Jitie Nguvu katika Bwana" hii imetolewa ili kwamba:
    - Tuweze kutiwa moyo kwa kuchunguza au kuhakiki na kutafakari katika kweli hizi pale tunapohitaji kutiwa moyo.
    - Tunaweza kushirikisha maandiko haya na kuwapa hamasa rafiki zetu na wengine ambao wamevunjika moyo au kukata tamaa.

***Changamoto:*** : Jitie Nguvu! Kila mahali karibu nasi kuna fursa nyingi kubwa zilizojigeuza kama hali zisizowezekana.

*Ikiwa tutarudia mara kwa mara kuzifakari kweli hizi za kutia moyo, zitatusaidia Kumjua Mungu.*

8. Watie moyo wanafunzi kuzitafuta fursa ili kuzungumza juu ya Yesu na kushirikisha nini Mungu anawafundisha.

   ***Maelezo:*** Tunataka kuwasaidia wanafunzi kuwa na hali ya utulivu katika kuzungumza juu ya Yesu katika mazingira na hali yoyote.

9. Vuta usikivu wa wanafunzi katika **kazi** zao **za ziada** (Kurasa 247-248).

   ***Kusoma darasani:*** Toa muda wa kusoma ukurasa 247 kwa sauti darasani na hakikisha kwamba kila mmoja anaelewa kazi ya ziada.

   ***Watie moyo wanafunzi wako kukutana na Mungu mapema kila asubuhi kwa ajili ya muda wao wa utulivu***.

   > ***...Ee Mungu, Wewe ni Mungu wangu, nitakutafuta Wewe kwa bidii mapema...*** (Zaburi 63:1). (*Strong's Exhaustive Concordance of the Bible*, "Hebrew and Chaldee Dictionary," Ukurusa 114, namba 7836)

10. Funga kwa maombi.

    ***Mfano:*** Waalike wanafunzi kupiga magoti pamoja na wewe mnapoomba pamoja na mshukuru Mungu kwa kukutana na wewe na kipekee kuzungumza na kila mmoja wenu.

## Mwongozo wa Kiongozi na Ujumbe wa Mwandishi........................Kipindi cha 5

1. Anza kwa maombi.

   ***Mfano**:* Waalike wanafunzi kupiga magoti pamoja na wewe mnapoomba pamoja na kuutoa muda kwa Mungu. Katika majuma machache yajayo utawataka wanafunzi kuomba wakiwa wamefungua macho yao wakiwa wanatembea, wamesimama, wanaendesha, n.k. lakini unawataka kuelewa kwamba ni muhimu kupiga magoti yao na kuomba kila wanapoweza kufanya hivyo.

2. Mtake kila mmoja kufungua katika karatasi ya **Ufuatiliaji** ambayo inahitajika siku hiyo. Kisha unaweza **kuzikagua na kuzisaini** (Ukurasa 276).

3. Chunguza/Hakiki **Nadhri Yangu katika Mafunzo ya Uanafunzi** (Ukurasa 11).

   ***Hamasisha**:* Watake wanafunzi kutia sahihi na tarehe kujiwekea nadhiri huko kama walikuwa hawajafanya hivyo bado.

   - Wanafunzi wana uwezekano wa kumaliza mafunzo ya *Ushirika wa Mtu na Mungu* ikiwa wataweka sahihi karatasi ya kujiwekea nadhiri kwao.

   - Baraka kubwa ni kwa wanafunzi ambao wanashiriki katika madarasa yote na kumaliza kazi zao za ziada kila siku.

4. Soma **"Kwa kuwa Kusudi langu la dhati ni kwamba Nimjue Yeye"** (Ukurasa 9-10). Mtake mtu mmoja kushirikisha Kuvuta taswira kwake sehemu moja ya mstari huu na kusikiliza pale anaporudisha Maombi yake kwa Mungu kama maombi binafsi ya **K**uabudu, **K**uungama, **K**ushukuru au **K**uomba kwa unyenyekevu. Wakumbushe wanafunzi kuweka mtazamao wao kwa Yesu (Waebrania 12:2).

   ***Mradi:*** Kabla mwanafunzi mmoja hajasoma ukurasa wa 9 kwa sauti, watake wanafunzi wote kufanya yafuatayo:

   - Kuzungushia maneno ***Yeye*** na ***Yake*** kila wakati wanapoyaona katika Wafilipi 3:10 (AMP).

- Sasa mtake mmoja wa wanafunzi kusoma Wafilipi 3:10 (AMP) kwa sauti, akibadilisha jina la Yesu kwa *Yeye* au *Yake*.

- Kisha mtake mmoja wa wanafunzi **K**ufikiria kwa kina, **K**uvuta taswira, na **K**uomba tena kwa Mungu baadhi ya sehemu za mstari huu.

5. Jadili **Maswali ya Marudio ya Kazi ya Ziada** (Ukurasa 248).

   ***Maelezo:***

   - Tumia swali la 4 katika ukurasa wa 248 kuwatia moyo wanafunzi kuzungumza kwa wengine juu ya Yesu na mambo aliyowafundisha wao.
   - Ruhusu yeyote katika kundi kuzungumza juu ya uzoefu unaotokana na somo la juma lililopita pale alipozungumza na mtu yeyote habari za Yesu au kushirikisha kitu chochote ambacho Mungu anamfundisha Yeye.

6. Jadili Notsi za kila siku katika Kusoma Biblia (NKSKB) (Kurasa 65-72) wanafunzi walizofanya juma lililopita. Watake baadhi yao:

   a. **Kushirikisha** moja ya notsi zao.

   b. **Kufikiria kwa kina** juu ya notsi hizo.

   c. **Kuvuta taswira** ya notsi hizo.

      ***Wakumbushe*** wanafunzi kwamba kuvuta taswira ya notsi hakumaanishi kuzielezea notsi. Waambie kuanza kwa kusema, **"Hii ndiyo picha ninayoiona."**

   d. **Ombea** notsi hizo kwa Mungu kama maombi binafsi katika **K-K-K-K.** Baada ya kumaliza, uweze kuwatia moyo.

      ***Eleza*** kwa wanafunzi kwamba hawatakiwi kukuambia wewe kile watakachoombea. Wanachotakiwa kufanya ni kuruhusu wewe na wanakikundi wengine kusikiliza wanapozungumza na Mungu.

*Kutafakari Notsi zetu za Usomaji wa Biblia Kila Siku kunatusaidia kumjua Mungu.*

7. Soma/Jadili kwa kina mafunzo ya **Jinsi gani ninaweza kumruhusu Yesu Kristo kuwa kitovu na Bwana wa maisha yangu?** (Kurasa 98-106). Unaposoma na kujadili, mara kwa mara simama na kutoa fursa kwa wanafunzi **K**ufikiria kwa kina, **K**uvuta taswira, na **K**uomba.

***Ukurasa 98:***

***Kanuni ya Muhimu Sana:*** Inapatikana katika Mathayo 6:11 na ni kanuni ya kujifunza *kuishi siku moja kwa wakati*.

**Kwa nini** Yesu alitufundisha sisi kuomba *"Utupe leo riziki yetu"*? Kwa nini hakufundisha kuomba riziki ya juma, mwezi, mwaka au maisha yote?

***Jibu:***

- Mungu anatutaka kuelewa kwamba Anatupenda na anatutaka tumwamini Yeye kwa kila kitu kila siku. Yeye pekee yake ndiye anayeweza kukidhi mahitaji yetu yote.

- Mungu anataka ushirika nasi kila siku, na anaelewa kwamba wengi wetu kamwe tusingetafuta ushirika na Yeye katika mazungumzo yetu, kama angetupatia kila kitu tunachokihitaji kwa ajili ya maisha yetu. Tungeukosa kabisa uzima tele hapa duniani, ambao unahusisha kumwamini Yesu kwa kila kitu kila siku.

- Siyo tu kwamba Mungu anapenda kututoa sisi kutoka hatua A kwenda hatua B au kutoka pale tulipo kwenda ukomavu (utu uzima). Bali Alituumba sisi ili tufurahie kila ushirika na yeye hatua kwa hatua pale tunapojihusisha katika mchakato wa kuhama kutoka mahali tulipo kwenda ukomavu (utu uzima). Huu ni ushirika wa siku kwa siku, wakati wote.

***Kielelezo:*** Jinsi gani unamla tembo? Unakata kidogo kidogo kwa wakati mmoja.

- Je unaishije maisha ya Kikristo? Ni siku moja kwa wakati.

***Thibitisha:*** Hakuna lisilowezekana kwa wale ambao wanamwamini Mungu, kuishi chini ya udhibiti wake na kutekeleza kanuni Zake.

- Ni lazima tujifunze kuyagawa maisha yetu katika vyumba vidogo vya siku moja na kisha kuishi kila siku kwa ajili ya Yesu.

**Chini ya ukurasa** katika kijisanduku chenye fomula **kuna maneno muhimu mawili ya** kutafakari:

1. ***Maelekezo:***

    - Maelekezo yanayozungumzwa hapa sio kama maelekezo yanayotolewa na Polisi wa Usalama Barabarani ambaye anaelekeza na kusema, "Nenda hapa, na unakwenda pale". Wala sio kama ya mwagiza teksi ambaye anampigia simu dereva kupitia redio kumwambia kwenda katika eneo fulani.

    - Aina hii ya maelekezo yanayozungumzwa hapa ni kama yale ambayo yanatolewa na kiongozi wa uwindaji au muongoza watalii ambaye anatoa maelekezo kwa kwenda na wewe na kukaa na wewe.

    - Yesu anatuelekeza kwa kukaa pamoja nasi. Kamwe hatuachi au kukupungukia (Isaya 41:10).

2. ***Mafanikio:***

    - Hakuna mafanikio makubwa kuliko **kuwa katika kitovu cha mapenzi ya Mungu leo, wakati wote (hatua kwa hatua)**.

***Ukurasa 99:***

- Katika ukurasa huu tunaona moja ya kanuni za muhimu sana zilizofundishwa katika Neno la Mungu:

  ***Kanuni****—"Mwenye haki ataishi kwa imaini."*

  - *"...na kila tendo lisilotoka katika imani iliyoridhiwa na Mungu ni dhambi"* (Warumi 14:23 AMP).

    - Tunapaswa kuishi maisha yetu kwa ushawishi kwa sababu tunajua Mungu anayakubali pale tunapoyakita mawazo, mitazamo na matendo yetu katika kanuni kutoka katika Neno Lake.

  - Pale Biblia inapotaja kanuni mara moja, hiyo inamaanisha kwamba ni ya muhimu sana. Katika ukurasa huu tunaona Biblia inataja kanuni hii mara nne, kwa hiyo, ni lazima itakuwa na umuhimu wa kipekee kwa Mungu kwamba tuielewe kanuni hii.

***Ukurasa 100:***

- Baada ya mtu mmoja kushirikisha majibu yatokanayo na Yohana 15:4-5 (NKJV), pendekeza kwamba jibu pasipo linatuelekeza kwenye ukweli kwamba pasipo Yesu hatuwezi kufanya lolote lenye maana kwa umilele. Tunaweza kuwavutia wanadamu—lakini siyo Mungu.

***Ukurasa 101:***

- Baada ya kuwa umesoma Yohana 10:28, na kujaza majibu katika kisanduku, ambayo ni W O K O V U simulia hadithi hii:

  ***Hadithi:*** Mvulana mdogo alikuwa akivuka kukatiza katikati ya mto, ndani ya maji ambayo yalikuwa yanamfikia kiunoni tu hivi. Kulikuwa na mvua kubwa katika eneo hilo, na kutokana na mvua maji yalianza kutiririka kutoka mashambani kwenda mtoni, yakisababisha kina cha maji kuongezeka kwa haraka. Kabla mvulana mdogo hajafikia ukingoni, maji yalikuwa juu ya kichwa chake, na hakuweza kuogelea. Mvulana mkubwa ukingoni alimuona

kwamba mvulana mdogo alikuwa katika shida na akaogelea ili kumuokoa. Akiwa amemshikilia kijana mdogo kwa mkono mmoja, alianza kuogelea kurudi ukingoni. Lakini kwa sababu maji yalikuwa yanakuja kwa kasi kubwa na kina kikazidi kupanda, mvulana mkubwa asingeweza kuogolea wakati anamshikilia yule mvulana mdogo. Kwa hiyo aliushika mkono wa mvulana mdogo na kumwambia, "Jishikilie kwenye mkanda wangu wakati ninakuvuta kuelekea ukingoni." Ilimgharimu mvulana mkubwa nguvu zake zote kuogolewa, na alipofika ukingoni na kugeuka nyuma ili kumchukua mvulana mdogo, alikuwa amekwenda. Mawimbi makubwa yalimchukua mvulana mdogo chini ya mto, na akawa amekufa kwa kuzama majini.

- Nakushukuru, Bwana, kwamba wokovu wangu hautegemei katika uwezo wa kukushikilia wewe, lakini kwamba umeahidi kwamba Wewe una nguvu za kutosha kunishikilia salama katika kiganja cha mkono wako.
- Ni jinsi gani Mungu tuliye naye alivyo na uweza na nguvu kwa sababu pale tulipokuwa tunazama katika dhambi zetu, naye Alikuja kutuokoa sisi, Wala hakutuambia, "masumbufu, shida, na matatizo katika maisha yatayafanya kuwa magumu, bali nishikilie mimi na nitajaribu kukuokoa."
  - Yesu alisema, "Nami nawapa uzima wa milele; wala hawatapotea kamwe; wala hakuna mtu atakayewapokonya katika mkono wangu." (Yohana 10:28).
  - Ili kitu fulani au mtu fulani asiondoke mkononi mwa Mungu, kina au anapaswa kuwa na nguvu zaidi ya ile ya Mungu, na tunajua kwamba hakuna kitu chenye nguvu kuliko Mungu.

***Swali:*** Nini tofauti kati ya kuwa na uzima na kuwa na uzima tele?

***Maelekezo:***

- Chini ya kisanduku cha jibu ambako ulijaza neno W O __ O V __, anzia kwenye ukingo

wa kushoto wa ukurasa na chora mstari ulionyooka ukatishe mpaka ukingo wa upande wa kulia wa ukurasa.

- Upande wa kulia wa ukurasa, juu ya mstari uliouchora, andika maneno haya:

***Mstari wa Yohana 10:10***

- Upande wa kulia mwa ukurasa chora mshale kuelekea juu kutoka mstari huo na mshale unaoelekea chini kutoka kwenye mstari.


- Juu ya mshale unaoelekeza juu, andika neno

***UZIMA***

- Chini ya mshale unaoelekea chini, andika maneno

***UZIMA TELE***

***Mfano***:




***Maelezo:***

- Yesu alisema, *"Mimi nalikuja ili wawe na uzima na kisha wawe nao tele"* (Yohana 10:10).

- Wale wanaomwamini Yesu Kristo kwa ajili ya wokovu wanao **uzima**.

- Wale wanaomwamini Yesu Kristo kwa kila kitu, kila siku wanao **uzima tele**. Wanamwamini Yesu kila siku kwa ajili ya wokovu, ukombozi, nguvu, faraja, mahitaji, maelekezo, na msamaha.

- Wakristo wanaomwamini Yesu kwa ajili ya **wakovu katika nyakati zote tatu:**
    - **Wakati uliopita—Tuliokolewa** kutokana na adhabu ya dhambi.
    - **Wakati uliopo—Tunaokolewa** kutokana na nguvu ya dhambi kadri tunavyomwamini Yesu kila siku na kuuachilia udhibiti wa maisha yetu Kwake.
    - **Wakati Ujao—Tutaokolewa** hata kutokana na uwepo wa dhambi pale tutakapokwenda mbinguni.

***Ukurasa 102:***

- Baada ya kuwa umesoma Wafilipi 4:19, watake wanafunzi kuzungushia neno wote/yote katika mstari. Kisha simulia hadithi hii.

    ***Hadithi**:* Gary Smalley alisumbuliwa na hasira kwa miaka miwili kabla hajapata ushindi dhidi ya hasira. Aliomba kwa bidii sana juu ya dhambi hii, na hatimaye Mungu alimwonyesha sababu ya tatizo lake. Alikuwa akitarajia mtu fulani au kitu fulani kuliko Mungu kutimiza mahitaji yake, na pale mahitaji yake yaliposhindwa kufikiwa, alipata hasira. Mungu aliweka mpango katika akili yake juu ya namna ya kushughulika na dhambi hii, na kutoka wakati huo alianza kuutekeleza mpango wa Mungu. Sasa anao ushindi dhidi ya hasira. Wakati alipotambua kwamba anakuwa na hasira, anaomba tu maombi haya:

    ***Maombi***—"Bwana, ninakushukuru Wewe kwamba ninatambua kuwa nina hasira. Nilikuwa nikitarajia mtu mwingine anitimizie mahitaji yangu kuliko kukutumaini wewe tu."

    - Jambo la ajabu kuhusu maombi haya ni kwamba yanaweza kutekelezeka kwa mambo mengi, kwa hiyo, kama hasira siyo tatizo kwako, unachotakiwa kufanya ni kubadilisha neno lingine kwenye *hasira*. Kama unasumbuliwa na hofu, upweke, uchungu, kukataliwa au dhambi nyingi yoyote au

tatizo, badilisha tu neno hilo kwenye *hasira* katika maombi yako.

***Ukurasa 103:***

***Maelezo:***

- Kwa miaka mingi mwandishi mwenza wa mafunzo ya *Ushirika wa Mtu na Mungu* alisoma Luka 17:5-9 na kushangazwa kwa nini Yesu hakulijibu swali hili muhimu ambalo lilitoka moyoni mwa wanafunzi. Ndipo siku moja alielewa kwamba Yesu alilijibu swali lao katika simulizi aliyowasimulia juu ya mtumishi aliyekuja kutoka shambani.

  ***Vuta Taswira***—Mtumishi anarudi kutoka shambani, ni joto, amechoka, mchafu, na ana njaa na kiu. Ana mahitaji mengi kwa ajili yake mwenyewe, lakini kabla hajajihudumia mahitaji yake, anaandaa chakula cha bwana wake na kumhudumia.

  ***Jibu liko wazi kabisa***—Kama tunataka imani zaidi, ni lazima **siku zote tumweke Mungu kuwa wa kwanza** na imani yetu itakua.

***Ukurasa 105:***

- Baada ya kuwa umesoma kifungu cha kwanza sehemu ya III D, Soma hadithi hii:

  ***Hadithi****:* Dhambi sicho kikwazo pekee kikubwa katika"Kumruhusu Yesu Kristo kuwa kitovu na Bwana wa Maisha yangu," l**akini siku zote gharama yake ni kubwa zaidi ya vile tunavyotarajia**. Mhuburi mkubwa Dr. R. G. Lee anasimulia hadithi hii katika ujumbe wake maarufu "Siku fulani ya Malipo". Wakati Dr. Lee alipokuwa mchungaji huko New Orleans, alihubiri redioni. Baada ya kila ujumbe alipokea simu, katika simu hizo, mpiga simu mmoja alimshambulia Dr Lee kwa maneno yasiyo na adabu na yenye kumkufuru Mungu. Kisha akamalizia simu yake kwa kusema, "Huyu ni mfalme wa mahakama teule isiyo rasmi."

  Usiku mmoja Dr. Lee akiwa tayari amekwenda kulala, alipokea simu kutoka hospitali. Muuguzi

alimuomba Dr. Lee ikiwa ataweza kwenda hospitali. Alisema, “Kuna kijana wa kiume hapa anayekaribia kufa, na ametuomba tukupigie wewe. Kitu pekee alichoweza kutuambia ni kwamba yeye ni hakimu wa mahakama isiyo rasmi”. Dr. Lee aliamka, na kwenda mara moja hospitali.

Alipofika, muuguzi alimwambia Dr. Lee, “Usimguse mtu huyu, kwa sababu hatujajua ni aina gani ya ugonjwa alio nao.”

Dr. Lee alipokuwa akikikaribia kitanda, kijana yule alipunga mkono ili amsogelee karibu kwa sababu angeweza kuzungumza tu kwa kunong’ona. Alisema, “Dr. Lee, Je wewe si unakwenda maeneo yote ya nchi hii na kuzungumza na vijana kuhusu habari za Yesu?”

Dr. Lee alisema, “Ndiyo”

Yule kijana, katika hali ya kunong’ona kiasi cha kutosikika vizuri, akasema, “Waambie vijana kwa niaba yangu kwamba shetani analipa kwa fedha bandia”. Kwa maneno hayo ya mwisho, kijana alikufa na kwenda kwenye umilele, pasipo Kristo na pasipo tumaini.

***Kielelezo:*** Kuungama dhambi na kuachilia udhibiti

- Dhambi isiyotubiwa katika maisha yetu humzuia Mungu kuwa mdhibiti katika maisha yetu. Kwa hiyo **jambo la kwanza tunalopaswa kufanya ni kuungama dhambi zetu**.
    - Kwa nini tuungame dhambi zetu? Dhambi huvunja uhusiano wetu na Mungu.

      ***Maelezo***: Hapa ni mahali pazuri la kuelezea tofauti kati ya uhusiano na Mungu na ushirika na Mungu.

        - Mara tunapoweka imani yetu katika Kristo Yesu kama Bwana na Mwokozi wetu binafsi, Mungu anatushikilia kwa usalama, na hakuna mtu anayeweza kutondoa mikononi mwake (Yohana 10:28). Tunakuwa katika uhusiano na Mungu milele (Yohana 1:12). Hakuna nguvu katika ulimwengu yenye uwezo wa kutosha kutuondoa mikononi

mwa Mungu kwa sababu Mungu ndiye mwenye nguvu zaidi huko mbinguni na hapa duniani (Mathayo 28:18). **Kwa hiyo katika uhusiano, Mungu ndiye anayetushilikilia sisi** tangu pale tunapookoka (Yohana 5:24).

- **Katika Ushirika, tunashikamana na Mungu**. Pale tunapotenda dhambi, tunajitenga wenyewe mbali na Mungu, na ushirika wetu na Mungu unavunjika (Isaya 59:2). Kumbuka, Mungu ndiye *"aliyekuita wewe [sisi] katika ushirika na Mwanaye Yesu Kristo Bwana wetu..."* (1 Wakorintho 1:9 NIV). Yeye hapendi kuona ushirika huu unavunjika, kwa hiyo, tunapotenda dhambi, ni lazima mara moja tuungame dhambi hiyo (1 Yohana 1:9) na kuachilia udhibiti wa maisha yetu kwa Mungu tena (Warumi 6:13).

***Kielelezo:*** Fikiria kwa makini Mungu akiwa amekunjua mikono yake miwili. Mkono wa Mungu wa kulia unawakilisha uhusiano wetu na Mungu na mkono wa Mungu wa kushoto unawakilisha ushirika wetu na Mungu. Katika mkono wake wa kulia tunajiona tukipumzika kwa amani na usalama kwa sababu tunajua kwamba hakuna anayeweza kutuondoa mikononi mwake. **Uhusiano wetu uko salama kwa sababu anatushikilia sisi**. Katika ushirika tunauuona mkono wake wa kushoto umenyooshwa, na tunajiona kama mtoto aliyeshikilia kidole cha Mungu. Pale tunapotenda dhambi, tunaachilia na ushirika unavunjika. **Ushirika wetu na Mungu hauko salama kama ulivyo uhusiano wetu na Mungu kwa sababu tunawajibika kwa ajili ya ushirika wetu, na wakati mwingine tunashindwa**.

***Mifano:***

- Tunao watoto wawili wa kiume. Wanaweza kuamua kwamba hawatataka mimi kuwa baba yao na kwenda mahakamani ili kubadilisha majina yao. Au wanaweza kusema kwamba mimi siyo baba yao. Lakini mimi ndiyo baba yao, hakuna kinachoweza kuub-

adilisha ukweli huu. Hata yule mwana mpotevu bado alikuwa ni mtoto wa baba yake (Luka 15:11-32). Kwa namna hiyo hiyo, **mara tunapofanyika wana wa Mungu, siku zote tutakuwa wana** (Yohana 5:24). Huu ni mfano wa uhusianao.

    - **Uhusiano** kati ya mimi na watoto wangu wawili hauwezi kuvunjika, lakini walipoasi, ushirika wetu ulivunjika. Hata hivyo, msamahasiku zote unafuatiwa na kuungama kwao (1 Yohana 1:9). Kwangu mimi, baba yao, japokuwa dhambi zao zinaweza kuwa kama rangi nyekundu, pale walipoungama na kusamehewa, walikuwa waupe kama theluji (Isaya 1:18). Ushirika wetu ulirejeshwa. **Huu ni mfano wa ushirika**.

- **Uhusiano** kati ya mimi na watoto wangu wawili hauwezi kuvunjika, lakini walipoasi, ushirika wetu ulivunjika. Hata hivyo, msamaha siku zote unafuatiwa na kuungama kwao (1 Yohana 1:9). Kwangu mimi, baba yao, japokuwa dhambi zao zinaweza kuwa kama rangi nyekundu, pale walipoungama na kusamehewa, walikuwa waupe kama theluji (Isaya 1:18). Ushirika wetu ulirejeshwa. **Huu ni mfano wa ushirika**.

- Jambo lingine tunalopaswa kulifanya ni kuachilia udhibiti wa maisha yetu kwa Mungu. Ninalifanya hili namna hii, Katika muda wangu wa utulivu kila asubuhi navuta taswira mwenyewe nikiwa nimekaa juu ya gari linalovutwa na farasi. Nilianza siku yangu nikiwa kwenye kiti cha dereva nikiwa nimeshikilia hatamu mikononi mwangu. Yesu ameketi pembeni yangu, na ninamkabidhi lijamu na kusema, "Bwana, sasa hivi ninakupa lijamu, udhibiti kamili wa maisha yangu, kwa kipindi chote kilichobakia kwa leo. Tafadhali uwe msimamizi katika maisha yangu leo." Unaweza kuvuta taswira mwenyewe ukiwa kwenye gari au ukiongoza roketi. Kitu cha muhimu hapa ni kwamba kwa uchaguzi wako wa hiyari, unaamua kumruhusu Mungu kuwa msimamizi katika maisha yako kwa siku hiyo. Pia ninavuta taswira nikiachilia udhibiti wa maisha yangu kwa Mungu kila siku kwa kufikiria kwamba ndani ya moyo wangu kuna kiti cha enzi na msalaba. Hizi ndizo nafasi

mbili za pekee ndani ya moyo wangu, na huko kuna nguvu mbili ambazo zinataka kutawala katika kiti cha enzi. Utu wangu wa kale wa dhambi na Roho Mtakatifu. Ninafikiria kwamba kila asubuhi pale ninapoamka, utu wangu wa kale wa dhambi upo kwenye kiti cha enzi. Kisha ninavuta taswira kwamba ninatoka kwenye kiti cha enzi na kusema, "Bwana, sasa hivi ninakupa udhibiti kamili wa maisha yangu kwa muda wote uliobakia leo. Tafadhali uwe msimamizi katika maisha yangu leo." Wakati huo Roho Mtakatifu, Roho wa Yesu, anachukua nafasi yake kwenye kiti cha enzi. Pale ninapochagua kwa hiyari yangu, kama tendo la utashi wangu, nachagua kukiachilia kiti cha enzi kwa Roho Mtakatifu, kuna nafasi moja tu kwa ajili ya utu wangu wa kale wa dhambi kwenda, na hapo ni msalabani. Pale ninapofanya hivyo, nimejikana mwenyewe haki ya kuwa msimamizi katika maisha yangu mwenyewe; na ninaishi chini ya udhibiti wa Roho Mtakatifu. Hivi ndivyo inavyomaanisha katika Luka 9:23 pale inaposema, *"Akawaambia wote, Mtu yeyote akitaka kunifuata na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake kila siku anifuate."*

- Sasa ni lazima tushughulike na swali lingine. Nilianza siku kwa kutoa udhibiti wa maisha yangu kwa Mungu, lakini nini kinatokea pale ninapotenda dhambi katika siku hiyo? **Pale ninapotenda dhambi, nakwapua umiliki, udhibiti, kutoka mikononi mwa Mungu na kukirudisha tena kwangu kiti cha enzi, nikidai kwamba mimi ndiye msimamizi. Kwa hiyo, ni lazima nifanye mambo mawili**:

    1. **Niungame dhambi zangu mara moja.**
    2. **Niachilie udhibiti tena kwa Mungu.**

    - Ni lazima tukumbuke kwamba siyo tu tunataka kusamehewa dhambi zetu, bali tunataka pia Mungu kuwa mdhibiti wa maisha yetu kila wakati na kila siku; na Anaweza kufanya hivyo kwa mwaliko wetu.

*Kutafakari juu ya kweli katika mafunzo haya ya Biblia kunatusaidia sisi Kumjua Mungu.*

8. Soma/jadili na kuzitafakari kweli (**KKK**) katika **Kumbusho la Kujitoa Kila Siku** (Kurasa 31-32).

*Maelezo:* Katika ukurasa 104 ulihamasishwa kuamua **kujiwekea Nadhiri Kikamilifu maishani** ili kumruhusu Yesu Kristo kuwa kitovu na Bwana wa maisha yako. Kisha ulihamasishwa kurudia kujiwekea nadhiri huko kikamilifu maishani kila siku. Unaweza kuyafanya marudio haya ya kujiwekea nadhiri sehemu muhimu ya maisha yako ya kila siku ikiwa utafanya mambo mawili:

1. Baada ya kuhakiki **Kumbusho la Kujitoa Kila Siku** darasani, tafuta dakika chache ukiwa nyumbani ambapo unaweza kutafakari: **K**ufikiria kwa kina, **K**uvuta taswira, na **K**uombea kweli hizi tena kwa Mungu kama maombi yako binafsi.

2. Kila asubuhi katika muda wako wa utulivu unaposoma ukurasa 31, utakumbushwa juu ya wema wa Mungu na upaji wake wa kila siku. Wakati unasoma ukurasa 32, rudisha maombi kwa Mungu kama maombi yako binafsi ya kujitoa tena.

*Mfano:* Ndani ya darasa soma kwa sauti ukurasa 31 na toa maoni juu ya wema na upaji wa Mungu kwa ajili yetu. Kisha ruhusu darasa kusikiliza, wakati wewe kama kiongozi, unasoma na kuomba tena kwa Mungu Ukurasa 32 kama maombi yako binafsi ya kujiwekea nadhiri kwa Mungu tena.

*Kutafakari katika kweli hizi hutusaidia kumjua Mungu.*

9. Jadili **Changamoto za Kusoma Biblia Kila Siku Kwa mwezi wa Pili** (Ukurasa 50). Watie moyo wanafunzi kuanza katika changamoto hii baada ya kuwa wamekamilisha siku zote 30 za **Changamoto za Usomaji Biblia Mwezi wa Kwanza.**

   *Maelezo:* Hapa ndipo mahali hasa pa kuanzia kwa wanafunzi juu ya mradi wa maisha yote wa kusoma Biblia yote mara moja kwa mwaka kwa kipindi chote cha maisha kilichobakia.

   *Kujiwekea nadhiri wenyewe kulisoma Neno la Mungu angalau mara moja kwa mwaka na kutafakari juu ya kile ulichosoma hutusaidia kumjua Mungu.*

10. Jadili Kalenda ya Usomaji Biblia Kila Siku na jinsi ya kuitumia (Kurasa 51-62). Wanafunzi wataanza kutumia kalen-

da hii baada ya kuwa wamemaliza siku zote thelathini za Mwezi wa Kwanza wa Changamoto za Usomaji wa Biblia**.**

***Maelezo:***

- Hii ni nyenzo tutakayowahamasisha wanafunzi kutumia ili kuisoma Biblia yote mara moja kwa mwaka kwa kipindi chote cha maisha yao.

  - Kwa kusoma sehemu ya Neno la Mungu kila siku, inatufanya tuwepo au tupatikane kwa Mungu ili kuzungumza nasi.

  - Asubuhi inayofuata katika muda wako wa utulivu, baada ya kusoma mistari yote ya zaburi 119, tutaanza usomaji wetu wa Bibilia katika **Kalenda ya Kujisomea Biblia Kila Siku**. Ikiwa tutamaliza Zaburi 119 tarehe 10, tunaanza usomaji wetu wa Biblia katika Kalenda ya Usomaji wa Biblia Kila Siku tarehe 11.

11. Jadili umuhimu ya kujisomea sura moja katika Mithali kila siku.

***Maelezo:***

- Kitabu cha Mithali kimejaa hekima ya Kimungu.
- "Mithali inatoa maelekezo ya kina ya Mungu kwa ajili ya watu ili kushughulika kwa ufanisi katika utendaji wa kila siku wa maisha: jinsi ya kuhusiana na Mungu, wazazi, watoto, majirani, na serikali." (Imenukuliwa kutoka *The Open Bible* notes)

*Kusoma sura moja kila siku katika Mithali na kutafakari juu ya kile tulichosoma kunatusaidia kumjua Mungu.*

12. Wahamasishe wanafunzi kutafuta fursa za kushirikisha kile Mungu anachowafundisha wao.

***Maelezo:*** Tunataka kuwasaidia wanafunzi kupata utulivu wa kuzungumzia juu ya Yesu katika kila eneo la maisha yao.

13. Vuta usikivu wa wanafunzi katika **Kazi** zao **za ziada** (Kurasa 249-250).

***Soma darasani:*** Ruhusu muda ili kusoma ukurasa 249 kwa sauti darasani na hakikisha kwamba kila mmoja anaielelwa kazi ya ziada.

- ***Watie moyo wanafunzi kuwa waaminifu kwa Mungu ili kukutana Naye kila siku katika muda wao wa utulivu.***

14. Funga kwa maombi.

    ***Mfano:*** Waalike wanafunzi kupiga magoti pamoja na wewe wakati mnapoomba pamoja na kumshukuru Mungu kwa ajili ya kukutana nanyi na kipekee kuzungumza na kila mmoja wenu.

## Mwongozo wa Kiongozi na Ujumbe wa Mwandishi.......................Kipindi cha 6

1. Anza kwa maombi.

   ***Mfano:*** Waalike wanafunzi kupiga magoti pamoja nawe mnapoomba pamoja na kuukabidhi muda kwa Mungu.

2. Mtake kila mmoja kufungua katika karatasi ya **Ufuatiliaji** ambayo inahitajika siku hiyo. Kisha unaweza **kuzikagua na kuzisaini** (Ukurasa 277).

   ***Uwajibikaji:*** Ukaguzi na uwekaji sahihi karatasi zao za Ufuatiliaji kila juma huwafundisha wanafunzi katika kanuni ya uwajibikaji iliyofundishwa katika Warumi 14:12. Pia inakusaidia wewe kama kiongozi kuona kama wanafunzi wako:

   - Wanafanya kazi za ziada na kujijengea mtindo wa maisha au

   - Wanahitaji kuhamasishwa au kutiwa moyo na wewe.

3. Soma **"Kwa kuwa Kusudi langu la dhati ni kwamba Nimjue Yeye"** (Ukurasa 9-10). Mtake mtu mmoja **kushirikisha kuvuta taswira** kwake sehemu moja ya mstari huu na kusikiliza pale anaporudisha Maombi yake kwa Mungu kama ombi lake binafsi. **Wakumbushe wanafunzi kuweka mwelekeo wao kwa Yesu** (Waebrania 12:2).

   Watake wanafunzi kuandika mawazo hayo katika ukurasa wa 9:

   - Yeremia 9:23-24 (NKJV)—*"...Bali kwa kuwa ananifahamu na kunijua Mimi..."*

   - 2 Timotheo 1:12—*"...maana namjua niliyemwamini..."*

   ***Kumbusho:*** Tunahakiki Wafilipi 3:10 (AMP) kila juma kwa sababu kuu tatu:

   1. **Ili kuyafanya macho yetu yamwelekee Yesu** na Yesu pekee yake na kutukumbusha kwamba **kusudi letu la dhati ni kumjua Yeye.**

2. Ili kutukumbusha kwamba **kanuni kama zilivyo siyo mwisho wa mambo. Hizo ni njia tu ambazo Mungu ametupatia ili kumjua Yesu** kwa kina, kwa undani, na kibinafsi.

3. **Ili kutafakari juu ya kweli zenye nguvu** katika mstari huu ili kwamba ziweze kuhama kutoka kwenye ukurasa kwenda kichwani na kisha kwenda mioyoni mwetu **ili kwamba tuweze kubadilishwa katika mfano wa Yesu**.

4. Jadili **Maswali ya Marudio ya Kazi ya Ziada** (Ukurasa 250).

***Maelezo:***

- Tumia swali la 5 kwenye ukurasa 250 ili kuwahamasisha wanafunzi kuzungumza kwa wengine habari za Yesu na mambo ambayo Anawafundisha.
    - Ruhusu mtu mmoja katika kundi kusimulia juu ya uzoefu wake wa majuma ya nyuma wakati alipozungumza na mtu fulani habari za Yesu au kushirikisha kitu chochote ambacho Mungu anamfundisha.

5. Jadili matumizi ya **Fomu za Notsi za Mahubiri au Somo** (Kurasa 21-24).

***Kwa nini*** ni muhimu kutengeneza notsi pale tunaposikiliza mafundisho na mahubiri ya kibiblia?

***Maelezo:***

- Wengi wetu tumesikia kweli ya kutosha (Neno la Mungu) likihubiriwa na kufundishwa ili tuwe Wakristo bora ambao wamewahi kuishi (kuwepo), lakini kwa sababu hatuandiki notsi na kuzitafakari (*K*ufikiria kwa kina na *K*uvuta taswira ya notsi hizi na kisha *K*uziombea tena kwa Mungu kama maombi binafsi), Shetani ametuibia ukuaji wetu wa kiroho ambao tungepaswa kuwa nao.

- ***Hadithi:*** Mnenaji mhamasishaji kwa ajili ya mashirika alishirikisha jinsi gani wakati mwingine tunavyokuja bila kujiandaa kwa kutumia nafasi ya fursa tulizo nazo. Alizungumzia juu ya kutembelea kanisa ili kusikiliza mahubiri. Alisema kwamba alikaa na kujiandaa kusikiliza ujumbe akiwa na kalamu na karatasi mkononi,

tayari kwa kuchukua notsi juu ya ujumbe huo. Ghafla alitambua kuwa hakuna mtu karibu yake aliyekuwa na kalamu na karatasi. Wazo hili lilifunga ufahamu wake. *Yawezekana hawatarajii jambo kubwa.*

- **Tunapaswa kuhudhuria ibada tukitarajia Mungu kuzungumza nasi**. Pale anapoongea, tunapaswa kujiandaa kuandika kile anachokisema. Mara tunapokiandika, basi tunaweza kuzitunza notsi mpaka tutakapokuwa na fursa ya kutafakari juu ya kweli hizo. Pale tunapotafakari (**K**ufikiria kwa kina, **K**uvuta taswira na **K**uziombea kweli hizo tena kwa Mungu kama maombi yetu binafsi), tunazihamisha kweli hizi kutoka vichwani mwetu kwenda mioyoni mwetu, ambako zinafanya kazi yake katika utekelezaji/utendaji.

*Pale tunaposikia Neno la Mungu likihubiriwa, kutengeneza notsi na kutafakari juu ya kile Mungu anachosema nasi, inatusaidia kumjua Mungu.*

6. Jadili **Notsi za kila siku katika Kusoma Biblia (NKSKB)** (Kurasa 65-72) walizozitengeneza wanafunzi juma lililopita. Waombe watu wawili au watatu:

   a. **K**ushirikisha moja ya jumbe zao.

   b. **K**ufikiria kwa kina notsi hizo.

   c. **K**uvuta taswira ya notsi hizo.

      - Wakumbushe wanafunzi kwamba kuvuta taswira ya notsi hakumaanishi kuzielezea notsi. Watake kuanza tu kwa kusema, **"Hii ni picha yangu ninayoiona."**

   d. Ombea notzi hizi kwa Mungu kama maombi binafsi (**K-K-K-K**). Baada ya kuwa wamemaliza, watie moyo.

      - Waambie wanafunzi kwamba hawatakiwi kukueleza wewe kile wanachotaka kuombea, bali wanapaswa kuomba na kuruhusu tu wewe na wanakikundi wengine kusikiliza pale wanapozungumza na Mungu.

   *Pale tunaposikiliza katika kile ambacho Mungu anasema nasi wakati tunasoma Neno Lake, kuchukua notsi na kisha kutafakari katika notsi hizo, inatusaidia sisi kumjua Mungu.*

7. Soma/jadili kwa kina mafunzo ya **Kuyajaza Maisha Yangu kwa Neno la Mungu** (Kurasa 107-119). Pale unaposoma na kujadili, mara kwa mara tulia na kuwapa wanafunzi fursa ya **K**ufikiria kwa kina, **K**uvuta taswira na **K**uomba.

    ***Ukurasa 107:***

    ***Fafanua*** nguvu ya Neno la Mungu ukurasa wa 107 kwa kusimulia hadithi hizi baada ya kuwa umezisoma:

    ***Hadithi #1:*** Don Milam, baba wa mwandishi mwenza, alikuwa muasi asiyeamini alipokuwa shule ya sekondari. Usiku mmoja alikuwa akitoka kwenda kupata kinywaji (kunywa) na kusherehekea. Mama yake alikuwa Mkristo mzuri, na alisimama mlangoni na kumsihi asiende. Akajilaza kwenye mlango wa mbele, akamsihi asitoke usiku ule wa dhambi, lakini Don alimpitia tu juu yake na kuelekea kwenye starehe.

    Alipokuwa akitembea mtaani, alipita karibu na duka la vitabu, na jicho lake liliangukia juu ya Biblia iliyokuwa wazi kwenye dirisha la duka. Alivutiwa na kusoma Mithali 1:22-33. *[Angalizo: Mtake mmoja wa wanafunzi kusoma kifungu hiki kwa sauti darasani.]* Mara aliposoma kifungu hiki, Mungu aliutia hatia moyo wake. Akaitikia na akaokolewa palepale mtaani, kwa kusoma Neno la Mungu.

    Baadhi ya marafiki waliokuwa naye walikuja karibu naye na kusema, "Vipi, Don. Hebu twende tukasherehekee."

    Lakini Don alisema, "Hapana, mimi nakwenda nyumbani."

    Alipokwenda nyumbani na kuingia kwenye mlango wa mbele, aliweza kumsikia mama yake chumbani kwake, ghorofani, akiomba kwa ajili yake. Muda mfupi baada ya tukio hili au uzoefu huu, Mungu alimwita Don katika huduma kama mchungaji na mwinjilisti.

    Ni hadithi nzuri ya kuvutia mno kuhusu nguvu ya Neno la Mungu na kuomba! Don J. Milan alifariki mwaka 1995 akiwa na umri wa miaka 85. miaka 65 kati ya hiyo aliiwekeza katika huduma kama mchun-

gaji, mwinjilisti na mchungaji wa muda baada ya kustaafu.

***Hadithi #2:*** Msichana mdogo aliyeitwa Gloria alituambia hadithi hii. Katika kijiji kilichoko mpakani mwa Texas na Mexico, kulikuwa na mafuriko mabaya sana. Hakukuwa na Mkristo hata mmoja katika kijiji kile, lakini baada ya mafuriko mvulana mdogo wa Kimexico aliipata Biblia ambayo maji ya mafuriko yaliibeba na kuiacha. Hakukuwa na mtu wa kumsaidia kukielewa kile alichokisoma kwenye Biblia, lakini kwa kusoma tu Biblia aliweza kujisikia hatia ya dhambi zake na kumpokea Yesu moyoni mwake kama Bwana na Mwokozi wake binafsi. Alitaka kuwa mmishenari kwa watu wake, kwa hiyo baada ya kumaliza Sekondari ya juu, alikwenda chuoni na kisha akaenda Seminari. Baada ya kumaliza alirudi katika kijiji kile kuwa mmishenari kwa watu wake mwenyewe, na wengi walimjua Kristo kupitia huduma yake. Gloria alisema, "Ninajua hadithi hii ni ya kweli, kwa sababu mvulana huyo mdogo ni baba yangu." Hii ni hadithi nyingine ya ajabu kuhusu nguvu ya Neno la Mungu.

## **Kwa nini Niyajaze maisha yangu katika Neno la Mungu** (Ukurasa 108, sehemu II Ukurasa 119)

***Ukurasa 109:***

- Isaya 40:8—*"Majani yakauka, ua lanyauka, bali neno la Mungu wetu litasimama milele."*
    - Mstari huu unaibua swali la muhimu sana. Kitu gani ni cha milele na kitadumu milele? Mambo matatu yametajwa katika Biblia:

        1. Neno la Mungu ni la Milele na litadumu milele.
            - Isaya 40:8—*"...Neno la Mungu wetu litasimama milele."*
            - 1 Petro 1:25—*"BALI NENO LA BWANA HUDUMU HATA MILELE. Na neno hilo ni neno lile jema lililohubiwa kwenu."*
            - Zaburi 119:89 (NIV)—*"Neno lako, Bwana ni la Milele..."*

2. Mungu ni wa milele na atadumu milele.

    - K/Torati 33:27 (NKJV)—*"Mungu wa milele ndiye kimbilio letu..."*

    - Zaburi 48:14—*"Kwa maana ndivyo alivyo Mungu, Mungu wetu milele na milele..."*

    - Tito 2:13 (NKJV)—*"...Mungu wetu mkuu na Mwokozi wetu Yesu Kristo..."*

    - Waebrania 13:8 (NKJV)—*"...Ni Yeye Yule jana leo na hata milele."*

    - Ufunuo 15:7 (NKJV)—*"...Mungu, anayeishi milele na milele."*

3. Nafsi za watu ni za milele na zitaishi milele.

    - Yohana 3:16 (NIV)—*"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanaye wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele."*

    - Mathayo 25:46 (NIV)—*"Na hao watakwenda zao kuingia katika adhabu ya milele, bali wenye haki watakwenda katika uzima wa milele."*

- Isaya 40:8 pia inasisitiza ufupi wa maisha duniani.

    - Zaburi 90:10 (NKJV)—*"Siku za maisha yetu ni…… zinapita upesi na tukatokomea mara."*

    - Zaburi 102:11—*"Siku zangu ni kama kivuli cha jioni, Nami ninanyauka kama majani."*

    - Zaburi 103:15-16—*"Mwanadamu siku zake zi kama majani, kama ua la kondeni ndivyo astawivyo. Maana upepo hupita juu yake, kumbe haliko; na mahali pake hapatalijua kamwe."*

    - Yakobo 4:14 (NIV)—*"...Uzima wenu ni nini? Maana ninyi ni mvuke uonekanao kwa muda mfupi tu, kisha hutoweka."*

- Kwa hiyo hapa zipo kweli zifuatazo:

- Maisha yetu hapa duniani yanapita haraka sana.
- Tutaishi milele ama katika adhabu ya milele, kufa milele yote lakini kamwe hakuna kufa, au katika uzima wa milele, milele na Bwana na waamini wa kweli mbinguni, ambako hakuna maumivu tena na huzuni tena.
- Wakati tupo hapa duniani, ni lazima tufanye mambo mawili muhimu ambayo yatatuathiri sisi na wengine wengi kwa ajili ya umilele.

  1. Ni lazima tuchague kati ya adhabu au hukumu ya milele na uzima wa milele. Madhara ya uamuzi huendelea milele.
  2. Ni lazima tuchague kati ya kutumia maisha yetu katika yale ambayo ni ya kitambo (matamanio yetu binafsi) au kuwekeza maisha yetu katika yale ambayo ni ya milele. Kumbuka kile Biblia inachotuambia ni umilele. (au cha milele):
     - **Neno la Mungu ni la Milele**—tunapaswa kuyakinaisha maisha yetu katika Neno lake.
     - **Mungu ni wa milele**—Tunapaswa kumjua Mungu kwa kina, kwa undani na kibinafsi.
     - **Nafsi za wanadamu ni za milele—**Tunatakiwa kuwafikia wanaume na wanawake kwa ajili ya Kristo na kuwafundisha kuwa wanafunzi wa kweli.

***Kielelezo:*** Maisha yako hapa duniani ni kama nukta juu ya mstari ambao hauna mwisho. Nukta hiyo inawakilisha muda tunaoishi hapa duniani. Mstari unawakilisha umilele. Tunao muda mfupi sana hapa duniani, lakini tunaweza kufanya kitu tofuati kwa ajili ya umilele ikiwa tutabakia katika mwelekeo na kujiwekea sharti kwa lile ambalo ni la milele.

Katika safu ya notsi upande wa kulia wa herufi G upande wa chini ya ukurasa wa 109, chora mstari kutoka ukingo wa kushoto wa safu ya notsi upande wa ukingo wa kulia wa karatasi, na juu ya mstari huo weka nukta moja ndogo. Kisha fikria kwamba mstari unakwenda nje ya ukurasa na hauna mwisho. Nukta

hii ni kama kufumba na kufumbua macho ukilinganisha na umilele. Bila shaka maisha hapa duniani ni maandalizi tu kwa ajili ya umilele. Muda hapa duniani ni mfupi sana, kwa hiyo, ni muhimu kwetu sisi kubakia katika mwelekeo na kujiwekea sharti katika yale ambayo ni ya milele, vinginevyo hatutaweza kulitimiza kusudi la Mungu katika maisha yetu.

***Mchoro:*** Kwenye karatasi itaonekana kama hivi:



***Angalizo:*** Ni lazima uongoze mstari ukingoni upande wa kulia mwa ukurasa na kisha fikiria kwamba unaendelea milele, bila kikomo.

***Ukurasa 112:***

- 1 Petro 2:2—*"Kama watoto wachanga waliozaliwa sasa yatamanini maziwa ya akili yasiyoghoshiwa, ili kwa hayo mpate kuukulia wokovu."*

  ***Hadithi:*** Mmishenari aliyekwenda kwa Wazawa au wenyeji katika nchi ya Marekani alimuongoza kwa Bwana Chifu aliyekuwa mzee. Takribani mwaka mmoja baadaye mmishenari alirudi kumwona chifu. Mmishenari yule alimtaka chifu kumueleza kuhusu maisha yake tangu alipokuwa Mkristo.

  Chifu alijibu, "Ni kama mbwa mweusi na mbwa mweupe wanapigana ndani yangu bila kukoma."

  Mmishenari akasema, "Vizuri chifu, ni yupi anashinda?"

  Chifu akajibu, "Ni yule ninayemlisha zaidi."

  - Ndani ya kila mmoja wetu kuna vita vya kiroho visivyokoma kati ya utu wa kale wenye asili ya dhambi na utu wetu mpya. Ni lazima tuulishe utu wetu mpya kwa kuendelea kuyajaza maisha yetu kwa Neno la Mungu, au la sivyo tutashindwa katika vita vya kiroho tunavyokabiliana navyo kila siku.

***Ukurasa 113:***


***Kielelezo:*** Mchoro katika ukurasa 113 unaonyesha jinsi Mungu anavyolitumia Neno lake katika maisha yetu.

Unaonyesha kwamba hata pale tunapotoka nje ya njia ya Mungu, kama tutakaa katika Neno Lake, ataongea nasi kwa maneno ya kukemea na kurekebisha kutupata sisi tena katika njia Yake.

***Angalizo:*** Ni wajibu wetu kuona kwamba hatutoki nje ya njia ya Mungu. Tubakie katika Neno la Mungu kila siku ili kwamba aweze kukutana nasi wakati wa uhitaji wetu kwa mafundisho, maonyo, marekebisho na maelekezo kuhusu jinsi ya kubakia kwenye njia.

- Pale tunapotoka nje ya njia ya Mungu, ufunguo wa haraka wa kuturejesha ni kurudi katika Neno Lake na kuzitendea kazi kanuni ambazo tulijifunza katika kipindi cha 5. Kanuni hizi ni:
    - Kutubu dhambi zetu mara moja.
    - Kuachia umiliki wa maisha yetu tena kwa Mungu mara moja kufuatia ungamo la dhambi zetu.
- Kama tutatekeleza kweli hizi rahisi, nyakati zetu za kutoka katika njia ya Mungu kutokana na dhambi kutakuwa ni kwa kipindi kifupi na kutatokea mara chache.

***Kuchora:*** Kwenye karatasi itaonekana kama hivi:



- Watake wanafunzi kuchora mchoro uliopo hapo juu katika vijitabu vyao vidogo katika ukurasa wa 113 katika safu ya notsi upande wa kulia wa 2 Timotheo 3:16. kisha watake kuandika mambo haya matatu chini ya kile walichokichora:

1. **Kaa katika Neno la Mungu kila siku.**
2. **Ungama dhambi zako mara moja.**

3. **Achilia udhibiti wa maisha yako tena kwa Mungu mara moja kufuatia ungamo la dhambi zako.**

***Ukurasa 116:***

***Maelezo:*** Yoshua 1:8 ni sehemu nzuri katika kusisitiza kwamba kutafakari ni kwa muhimu katika utekelezaji. Ikiwa tunataka kutekeleza maandiko, ni lazima kwanza tuyatafakari. Kutafakari kunamaanisha **K**ufikiria kwa kina kile Mungu anachokisema kwetu, kisha **K**uvuta taswira ya kile anachokisema kwetu na kisha **K**uombea kile alichokisema kwetu kurudisha tena Kwake kama maombi binafsi. Ule ukweli kwamba tunayo maarifa vichwani, hakutakuwa na utekelezaji wa kweli ambao unamletea Mungu utukufu. Ni pale tu kweli hizi zinapoingia kwenye mioyo yetu kupitia kutafakari tutaweza kuziona zikitenda kazi kwa usahihi kutoka mioyoni mwetu katika utekelezaji.

***Kurasa 117-118:*** Mithali 2:1-10 (LIV) na kanuni vinapaswa kuwa vya msaada mkubwa kwa wanafunzi. Ni kifungu kinachopendwa na wengi. Hapa tunaona orodha ya baraka zilizoahidiwa kwa wale wanaolichunguza Neno la Mungu kwa bidii, kumsikiliza Mungu na kutii kile anachotufundisha. Hii ni ahadi yenye masharti. Ikiwa tutafanya kile Mungu anasema, siku zote tutaweza kupata kile alichoahidi.

***Maelezo:*** Tunapaswa kuwa katika Neno la Mungu kila siku, tukichunguza na kutarajia Mungu kuzungumza nasi. Tunapaswa kuchunguza Neno kwa bidii kama vile tunavyotafuta pesa iliyopotea au hazina iliyositirika.

***Kielelezo:*** Kama tungekuwa na ramani inayotuonyesha wapi hazina kubwa imefichwa, kitu pekee ambacho tungetakiwa kufanya ni kuchukua ramani na kuichimba hazina ili kwamba iweze kuwa yetu, ninajua kwamba:

- Tungekwenda haraka na kuichimba hazina, na hakuna ambacho kingeweza kutuzuia.
- Tungekwenda kwa msisimko na matarajio makubwa.
- Tungetoa kafara za kila aina ili kupata hazina mara moja kwa sababu hiki ndicho kingekuwa kipaumbele chetu cha juu.

- Ikiwa tutafanya hilo kwa ajili ya hazina ya duniani ambayo ni ya muda, hatupaswi kufanya kwa msisimko zaidi juu ya hazina ya kiroho, ambayo ni ya milele? Fikiri juu ya hilo!

***Tafsiri:***

- *Hekima ya Kimungu*, ambayo ni # 1 katika ukurasa wa 118,imetafsiriwa katika Mithali 4:11 (AMP) kama *"Ufunuo wa kiwango cha juu katika njia na makusudi ya Mungu."*
- *Uelewa au ufahamu* ((# 8 katika ukurasa wa 118), ), kama ilivyotafsiriwa katika Mithali 4:7, inamaanisha, kushughulikia kwa hekima ambako ni kujua jinsi ya kutumia hekima ya Kimungu. ("Hebrew Dictionary of the Old Testament" in *Strong's Exhaustive Concordance of the Bible*, Ukurasa 20, namba 995).

***Habari za Kusisimua:***

- Mithali 2:9 (LIV)—*"Yeye (Bwana) huonyesha jinsi ya kupambanua yaliyo ya haki kutoka kwa yasiyo ya haki, jinsi ya kupata uamuzi ulio sahihi kila wakati."*
    - Hii inaonekana ni nzuri sana kuweza kuwa kweli. Je, hili linawezekanaje? Jibu ni katika Mithali 2:10 (LIV)—*"Maana hekima na kweli vitaingia katika kilindi cha moyo wako, vikiyajaza maisha yako kwa furaha"*
        - Yesu ndiye kweli katika mwili. Yohana 14:6 (NIV)—*"Yesu akajibu, Mimi ndimi njia na kweli na uzima. Mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya Mimi."*
        - 1 Wakorintho 1:30 (NIV)—*"...Kristo Yesu, ambaye amefanyika kwetu hekima kutoka kwa Mungu..."*
        - Yesu ndiye furaha ndani ya mwili. Roho Mtakatifu anazungumza nasi kupitia mwimba Zaburi ili kutufundisha kwamba Mungu mwenyewe ndiye furaha—*"Hivyo nitakwenda madhabahuni kwa Mungu, kwa Mungu aliye furaha yangu na shangwe yangu…"* (Zaburi 43:4 NIV).

- Kwa hiyo nini ufunguo wa kuweza kupambanua jema na baya, kufanya maamuzi sahihi kila wakati, na kupitia maisha yaliyojaa furaha? Jibu ni rahisi kabisa. Hekima na kweli lazima viingie kwenye kilindi cha moyo wako" Yesu ndiye hekima, kweli, na furaha katika mwili." Kwa hiyo, pale tunapotekeleza kweli kutoka katika Neno la Mungu na kujiachilia udhibiti wa maisha yetu kwa Yesu, anakuwa kitovu cha maisha yako ambaye kwa Yeye kila kitu katika maisha yako kinahusika. Pale anapokuwa kitovu cha maisha yako, katika udhibiti wa maisha yako, utaweza kupambanua lilo jema na baya, kufanya maamuzi sahihi kila wakati, na kupata maisha yaliyojaa furaha.
- Fikiri juu ya hilo
    - Wakati Yesu alipoishi hapa duniani, siku zote aliweza kupambanua kati ya mema na mabaya na kufanya maamuzi sahihi kila wakati. Pale anapokuwa katika udhibiti wa maisha yetu, Atafanya vivyo hivyo kwa ajili yetu.

      ***Hitimisho:*** Jambo la pekee lenye maana ni kuchunguza Neno la Mungu kwa bidii, kumsikiliza Mungu, kumtii, na kupokea baraka alizo nazo kwa ajili yetu. Matokeo siyo maisha pasipo matatizo bali ni maisha yaliyojaa furaha hata nyakati za matatizo (katikati ya matatizo).

      ***Mfano: Tunalichunguza Neno la Mungu na kugundua kanuni ambayo inatufundisha sisi kwamba tunapaswa kumruhusu Yesu Kristo awe kitovu na Bwana wa maisha yetu na kwamba tunapaswa kuachilia udhibiti wa maisha yetu Kwake. Tunamtii Mungu na kwa matendo ya hiyari yetu tunaanza kuachilia udhibiti wa maisha yetu Kwake kila siku. Kisha tunagundua***

***kwamba pale Mungu anapokuwa mdhibiti wa maisha yetu, tunaweza kutofautisha kati ya mema na mabaya na kufanya maamuzi sahihi. Pale anapokuwa siyo mdhibiti, tunatenda dhambi, tunashindwa, tunapungukiwa na tunashindwa kulenga shabaha na baraka alizo nazo kwa ajili yetu***.

- Maisha yetu yamejawa na furaha pale mioyo yetu inapokuwa imejazwa kwa Roho Mtakatifu, pale tunapokuwa tumeuachilia udhibiti wa maisha yetu kwa Mungu
- Kule kudhibitiwa na Roho Mtakatifu na kujazwa furaha hakumaanishi kwamba kamwe hatutapata matatizo. Tunakuwa na furaha kwa sababu tunaye Yesu, na Yesu ndiye furaha iliyofanyika mtu. Siyo tu tutajawa na furaha, bali tutaweza kupambanua mema na mabaya na kufanya maamuzi sahihi kila wakati.

*Tunamjua Mungu vizuri pale tunapotafakari juu ya kweli tunayoipata katika Kujifunza Biblia.*

8. Chunguza au hakiki **Makusudi ya Maisha kwa ujumla** (Kurasa 12-13).

   ***Maelezo:*** Kiongozi anapaswa kuchunguza au kuhakiki notsi za mwandishi katika somo hili kwenye kipindi cha 1 cha Mwongozo huu wa Kiongozi. Kisha awashirikirishe wanafunzi kile anachofikiri kinahitaji kufanyiwa uchunguzi au uhakiki. Hutakuwa na muda wa kutosha, kwa hiyo, unaweza kuchagua kuuliza maswali machache ambayo yataleta usikivu wao tena kwenye **Makusudi ya Maisha kwa Ujumla**, ambayo ni ya muhimu sana.

9. Chunguza au hakiki **Tabia tatu Muhimu za Mwanafunzi wa Kweli** (Ukurasa 19).

   ***Maelezo:*** Kiongozi anapaswa kuchunguza au kuhakiki notsi za mwandishi wa somo hili katika Kipindi cha 2 cha Mwongozo huu wa Kiongozi. Kisha atachunguza au kuhakiki na wanafunzi kile unachofikiri kinahitaji kutiliwa mkazo. Huta-

kuwa na muda wa kutosha. Unaweza kutaka kuuliza maswali kama hili: *Ni kitu gani Mungu alikitilia makazo kwako wakati mlipozungumza kuhusu tabia hizi darasani?*

10. Chunguza au hakiki kitu cho chote mlichokijadili mpaka hapo mlipofikia ambacho unafikiria wanafunzi wanahitaji msaada au kutiwa moyo.

    ***Maelezo:*** Unaweza tu kuuliza kama wanayo maswali juu ya masomo ambayo tayari wamejifunza mpaka walipofikia.

11. Wahamasishe wanafunzi kutafuta fursa ili kushirikisha kile ambacho Mungu anawafundisha wao.

    ***Maelezo:*** Tunataka kuwasaidia wanafunzi kuwa watulivu wanapozungumzia habari za Yesu katika kila eneo la maisha yao.

12. Vuta usikivu wa wanafunzi kwenye **kazi** zao **za ziada** (Kurasa 251-252).

    ***Soma:*** Ruhusu muda ili kusoma ukurasa 251 kwa sauti darasani na hakikisha kwamba kila mmoja ameielewa kazi ya ziada.

    ***Soma darasani:*** Sababu mbili za kuwa na muda wako wa utulivu kila siku mapema alfajiri:

    1. **Yesu alionyesha mfano katika hilo.**

       ***Hata alfajiri na mapema sana,*** *wakati pakiwa giza bado,* ***Yesu aliamka,*** *akatoka nyumbani,* ***na akaenda zake mahali pasipokuwa na watu, ambako aliomba*** (Marko 1:35 NIV).

    2. **Maandiko yanalisisitiza hilo.**

       Maneno ***kutafuta*** na ***mapema*** katika Isaya 26:9 na ***mapema*** katika Zaburi 63:1 yanatokana na neno la Kiebrania ***shalchar***, ambalo linamaanisha **"ni kutafuta kwa bidii alfajiri na mapema."** (*Strong's Exhaustive Concordance of the Bible*, "Hebrew and Chaldee Dictionary," Ukurasa namba, number 7836)

       Kwa hiyo, mistari hii inapaswa kutafsiriwa hivi:

***..Nitakutafuta Wewe kwa bidii alfajiri na mapema...*** (Isaya 26:9).

***...Ee Mungu, Wewe ni Mungu wangu, nitakutafuta wewe kwa bidii alfajiri na mapema ...*** (Zaburi 63:1).

13. Funga kwa maombi.

    ***Mfano:*** Waalike wanafunzi kuungana nawe kupiga magoti mnapoomba pamoja na kumshukuru Mungu kwa ajili ya kukutana nanyi na kipekee kuzungumza na kila mmoja wenu.

## Mwongozo wa Kiongozi na Ujumbe wa Mwandishi........................Kipindi cha 7

1. Anza kwa maombi.

   ***Mfano:*** Waalike wanafunzi kupiga magoti pamoja nawe mnapoomba pamoja na kuukabidhi muda kwa Mungu.

2. Mtake kila mmoja kufungua katika karatasi ya Ufuatiliaji ambayo inahitajika siku hiyo. Kisha unaweza kuzikagua na kuzisaini (Ukurasa 278).

   ***Uwajibikaji:*** Ukaguzi na uwekaji sahihi karatasi zao za Ufuatiliaji kila juma huwafundisha wanafunzi katika kanuni ya uwajibikaji iliyofundishwa katika Warumi 14:12. Pia inakusaidia wewe kama kiongozi kuona kama wanafunzi wako:

   - Wanafanya kazi za ziada na kujijengea mtindo wa maisha au
   - Wanahitaji kuhamasishwa au kutiwa moyo na wewe.

3. Soma **"Kwa kuwa Kusudi langu la dhati ni kwamba Nimjue Yeye"** (Ukurasa 9-10). Mtake mtu mmoja kushirikisha Kuvuta taswira kwake sehemu moja ya mstari huu na kumsikiliza pale anaporudisha Maombi yake kwa Mungu kama ombi lake binafsi. **Wakumbushe wanafunzi kuweka mwelekeo wao kwa Yesu** (Waebrania 12:2).

   ***Kumbusho:*** Tanaichunguza au kuhakiki Wafilipi 3:10 (AMP) kila wiki kwa sababu kuu tatu:

   1. **Ili kuyafanya macho yetu yamwelekee Yesu** na Yesu peke yake na kutukumbusha kwamba **kusudi letu la dhati ni kumjua Yeye zaidi.**
   2. Ili kutukumbusha kwamba kanuni zenyewe haziwi mwisho. Bali **ni njia tu ambazo Mungu ametupatia ili tumjue Yesu** kwa kina, kwa undani na kibinafsi. Kwa hiyo tunafanya mazoezi ya nidhamu ili tupate kumjua Yeye.
   3. **Ili kuzifakari kweli zenye nguvu katika mstari huu**; Ili kuzihamisha kutoka kwenye ukurasa, kwenda vichwani mwetu, na kisha kwenda mioyoni

mwetu kupitia kutafakari **ili kwamba Mungu aweze kuitumia kutubadilisha katika mfano wa Yesu**.

4. Mtake mtu mmoja kushirikisha kisha **K**ufikiria kwa kina, **K**uvuta taswira na **K**uombea tena kwa Mungu **Notsi** zake **za Mahubiri au Somo** (Ukurasa 21-24).

   ***Marudio:***

   - Tunapaswa kuhudhuria ibada za kuabudu tukitarajia Mungu kuzungumza nasi. Pale anapozungumza, tunapaswa kuwa tumejiandaa kuandika kile Anachokisema. Mara tunapoandika, basi tunaweza kuzitunza notsi mpaka tunapokuwa na fursa ya kutafakari kweli hizo. Pale tunapotafakari (**K**ufikiria kwa kina, **K**uvuta taswira, na **K**uombea kweli tena kwa Mungu kama maombi binafsi), tunazihamisha kweli kutoka vichwani kwetu kwenda mioyoni mwetu ambako zinaweza kufanya kazi kwa namna yake katika utekelezaji.

   *Pale tunapotulia kutafakari juu ya notsi tunazozitengeneza huku tunasikiliza Mungu anapozungumza nasi katika mahubiri, inatusaida kumjua Yeye.*

5. Jadili **Maswali ya Marudio ya Kazi za Ziada** (Ukurasa 252).

   ***Maelezo:***

   - Tumia swali la 4 kwenye ukurasa 252 kuwatia moyo wanafunzi ili kuzungumza na wengine kuhusu Yesu na mambo ambayo amewafundisha.

     - Mruhuusu mtu mmoja katika kundi kusimulia kuhusu uzoefu unaotokana na juma lililopita wakati alipozungumza na mtu kuhusu Yesu au kushirikisha kitu fulani ambacho Mungu amemfundisha.

6. Soma/Jadili kwa kina mafunzo ya **Jinsi gani naweza kuyajaza maisha yangu kwa Neno** (Kurasa 120-128) Unapoendelea kusoma na kujadili, mara kwa mara simama na kuwapa wanafunzi fursa ya **K**ufikiria kwa kina, **K**uvuta taswira, na **K**uomba.

   ***Ukurasa 120:***

   - Elezea kielelezo cha Mkono—Hii inaonyesha jinsi ya

kulishika Neno la Mungu. Kinaonyesha jinsi ya *"... Kuyashika mafundisho na kuishi kulingana na **yanavyo-fundisha**"* (Yohana 8:31 AMP).

- Kinaonyesha jinsi tunavyotumia njia nne za kupata Neno la Mungu katika nia zetu: kusikia, kusoma, kujifunza, na kushika.

- Kisha kinatuonyesha jinsi kidole gumba, kutafakari, kilivyo kitu cha muhimu ili kupata Neno la Mungu pale linapofanya kazi kwa kusikia, kusoma, kujifunza na kushika. Pasipo kidole gumba kutafakari, kulipata Neno la Mungu kikamilifu kunakuwa kidogo au kunakosekana kabisa.

- Mara ile kweli inapoingia katika nia zetu, inahamia kwenye mioyo yetu kwa njia ya kutafakari ili kwamba tuweze *"kuishi kulingana na lilivyo"* ikimaanisha kuitumia hiyo kweli.

- Jinsi ya kuonyesha kielelezo cha mkono:

    1. Shika Biblia yako katika mkono wako wa kulia. Fungua mkono wako wa kushoto, weka kiganja chako wazi, egesha uzito wa Biblia kwenye kidole kidogo cha mkono wa kushoto, ambacho kinawakilisha kusikia, kisha ondoa Biblia kwenye kidole na onyesha kuwa hiki kidole hakiwezi kuishika Biblia.
    2. Kutoka hapo, weka sasa Biblia kwenye vidole vinavyowakilisha kusikia, na kusoma, na uivute bila kipingamizi, uonyeshe kwamba bado kunakuwa hakuna ushikaji wa Neno la Mungu.
    3. Kisha weka Biblia kwenye vidole vinavyowakilisha kusikia, kusoma, na kujifunza na uivute hapo bila kipingamizi, uonyeshe kwamba bado hakuna ushikaji wa Neno la Mungu.
    4. Kutoka hapo weka Biblia kwenye vidole vinavyowakilisha kusikia, kusoma, kujifunza, na kushika na uivute hapo, uonyeshe kwamba hakuna ushikaji wa Neno la Mungu.
    5. Sasa rudi kupitia hatua hizi kwa kuanzia kidole kile kidogo, lakini onyesha nini kinatokea pale unapoweka dole gumba, kinachowakilisha kutafakari, ukivitendea kazi vile vidole.

6. Halafu onyesha nini kinatokea pale vidole vyote na kidole gumba vinapofanya kazi pamoja kwa kushika Neno la Mungu.

*Tunapoyajaza maisha yetu kwa Neno la Mungu kwa njia ya kusikia, kusoma, kujifunza, kukariri na kulitafakari bila kuacha tunaanza kulishika Neno la Mungu.*

***Kurasa 120-127:***

- Unapowaongoza wanafunzi kupitia kurasa hizi, tulia kidogo ili kuwapata nafasi kutafakari kila wakati muda unapopatikana. Kwenye kila ukurasa jaribu kumtaka angalau mwanafunzi mmoja kuchagua sehemu ya mstari na kisha **K**ufikiria kwa kina, **K**uvuta taswira, na **K**uuombea mstari huo tena kwa Mungu kama maombi yake binafsi wakati wewe na wanafunzi wengine mkisikiliza.

  ***Wakumbushe*** wanafunzi kwamba kuvuta taswira ya notsi hakumaanishi kuzifafanua notsi. Waombe kuanza kwa kusema, **"Hii ndio picha ninayoiona."**

***Ukurasa 125, sehemu B:***

- Wasisitize wanafunzi umuhimu wa kujitoa mwenyewe kuwa lengo la maisha yote kuitawala Biblia.

  ***Hadithi:*** Rafiki yetu mpendwa, E. F Hallock "Mhubiri", akiwa bado kijana, alijiwekea kuwa na lengo la kuitawala Biblia, lakini muda si mrefu alibaini kwamba Biblia ndio ilikuwa inamtawala yeye.

  - Pale Neno la Mungu linapoanza kututawala, litatugeuza nia zetu na mioyo yetu.
  - Mungu anatumia Neno lake kutufinyanga nia zetu toka ndani.

***Kurasa 125-126, sehemu C:***

- **Bila kuwa na nidhamu, hakuna tumaini kubwa ambalo litatufanya kuwa wanafunzi wa kweli ambao Mungu anatutarajia kuwa.**

- 1 Wakorintho 9:24-27 (LIV) inaongea juu ya maisha ya nidhamu ya Kikristo na kutoa mwongozo kwa ajili ya Mkrito wa kweli:

- Mstari 24—*"...Pigeni mbio namna hiyo ili mpate."* Ni lazima kujikana kila siku sehemu ya utu wetu ili tuweze kuwa wanafunzi bora wanaopaswa, pasipo kuzuiliwa na chochote.
- Mstari 25—*"...ni lazima ujinyime nafsi yako vitu vingi ambavyo vinaweza kukuzuia usiweze kufanya yaliyo mazuri....."* Ni lazima tujikumbushe kwamba wengine wanaweza, lakini tunaweza tusiweze – kama tunataka kuwa wanafunzi bora tunaweza kuwa hivyo kwa njia ya Kristo.
    - *"...Tunafanya kwa ajili ya thawabu ya mbinguni ambayo haichakai."*
        - Hivyo tutazifanyia nini hizi thawabu huko mbinguni? Tutaziweka miguuni pa Yesu. *"Ndipo hao wazee ishirini na wanne huanguka mbele zake yeye aketiye juu ya kile kiti cha enzi, na humsujudia yeye aliye hai hata milele na milele, nao hutupa taji zao mbele ya kile kiti cha enzi, wakisema, Umestahili wewe, Bwana wetu na Mungu wetu, kuupokea utukufu na heshima na uweza; kwa kuwa wewe ndiwe uliviumba vitu vyote, na kwa sababu ya mapenzi yako vilikuwako, navyo vikaumbwa"* (Ufunuo 4:10-11 NKJV).
    - Huku ni kuwekeza kwa ajili ya umilele.
- Mstari 26—*"Hata mimi napiga mbio vivyo hivyo, si kama asitaye, napigana ngumi vivyo hivyo, si kama apigaye hewa."* Hili anasema nasi juu ya kuishi maisha ya uanafuzi wenye nidhamu, yaliyojaa kusudi na ari ya kumjua, kumpenda, na kumtumikia Mungu.
- Mstari 27—*"...ninauadhibu mwili wangu, nikiuburuza, naupatia mafunzo ili kufanya yale unaopaswa kuyafanya siyo yale unayotaka wenyewe kuyafanya..."*
    - Hii ina maana kwamba Paulo asingependa mwili wake uendeshe maisha yake. Bali aliweka nafasi ya kazi hiyo kwa ajili ya Roho Mtaktifu.

      ***Kielelezo:*** Ikiwa miili yetu itayadhibiti maisha yetu, hatutaweza kamwe kuamka asubuhi na

mapema na kuwekeza muda wetu mzuri na Mungu kwa ajili ya muda wetu wa utulivu. Kwa nini? Kwa sababu miili yetu inaweza kutuambia, "Zima kengele ya saa, rudi ulale; nahitaji kupumzika zaidi."

**Andika** kwenye safu ya notsi jinsi tafsiri ya J.B. Philips inavyohitimisha 1 Wakorintho 9:24-27 kama ifuatavyo:

1. **Weka lengo lako ushinde**
2. **Jifunze kwa bidii**
3. **Pania**
4. **Ifanyie mazoezi kanuni ya kujikana mwenyewe.**

***Ukurasa 127, sehemu D:***

- Hii ni moja ya kanuni muhimu sana zinazofundishwa na Neno la Mungu: Ishi siku moja kwa wakati. Hakikisha umepata kiasi cha Neno la Mungu moyoni mwako leo.

    - Hila zake Shetani za hukuambia uongo ili useme baadaye. Yeye ni mwerevu sana na hututaka tuone kuliweka Neno la Mungu mioyoni mwetu ni upuuzi. Anataka tuwe na mwitikio hasi katika hilo. Yeye anachofanya ni kutunong'oneza masikioni mwetu, "Wazo hili ni sawa, ni murua kabisa, ila kwa leo unayo mambo mengi mno ya kufanya na tayari umeshachelewa. Kwa nini usisubiri mpaka kesho? Hebu fikiria juu ya hilo!

*Kuzitafakari kweli tunazojifunza katika kujisomea Biblia hutusaidia kumjua Mungu.*

7. Jadili **Notsi za kila siku katika Kusoma Biblia (NKSKB)** (Kurasa 65-72) wanafunzi walizozitengeneza juma hili. Waombe watu wawili au watatu:

    a. Kushirikisha moja ya notsi zao

    b. **K**ufikiria kwa kina notsi hizo.

    c. **K**uvuta taswira ya notsi hizo.

    d. Kuombea notsi hizo kwa Mungu kama maombi binafsi ya **K-K-K-K**. Baada ya wao kumaliza, uwe mhamasishaji au mwenye kutia moyo.

*Tunaposikiliza kile Mungu anachosema nasi tunaposoma Neno Lake, tunatengeneza notsi, na kisha kutafakari notsi hizo, inatusaidia kumjua Mungu.*

8. Soma/Jadili **Changamoto za Kushika Maandiko** (Ukurasa 235).

   ***Maelezo:*** Wanafunzi wanapokuwa wanashika na kutafakari maandiko haya, watakua na kuimarika katika maeneo yafuatayo:

   - Kumtegemea Mungu katika kila jambo
   - Kukaa ndani ya Kristo
   - Ushuhudiaji
   - Kulithamini Neno la Mungu
   - Kujiwekea sharti au kujitoa kwa Mungu
   - Kutiwa Moyo
   - Kuachia udhibiti kwa Mungu

   *Tunapotafakari maandiko haya ambayo tumeyakariri, yanatusaidia kumjua Mungu.*

9. Soma/Jadili **Mpango wa Kushika Maandiko** (Ukurasa 236).

   ***Maelezo:*** Ikiwa utaufanyia kazi mpango huu, mpango nao utakutendea kazi pia.

   - Kushika maandiko haya huyawezesha kuingia akilini. Kutafakari maandiko huyafanya yaingie mioyoni mwetu, na mara yanapokuwa mioyoni mwetu, tunaweza kuyatumia katika maisha yetu.

   ***Hadithi:*** Huko nyuma nilikuwa nashangaa kwa nini nashika mstari halafu wiki moja baadaye siukumbuki. Nilitambua kwamba ufunguo wangu ulikuwa kifungu cha 2f kwenye ukurasa 2136 ambacho kinatuhamasisha kuurudia ule mstari mara moja baada ya kuushika kwanza kwa kunukuu maandiko yaliyotajwa, mstari, maandiko yaliyotajwa mara 30. Kitu kingine kinachosaidia ni kunukuu ule mstari kila mara wakati unapowashirikisha wengine. Kwa mistari tunayoitumia ama tunayoipoteza.

10. Jadili **Udhuru na Mwitikio wa Maandiko** (Ukurasa 237).

*Maelezo:*

- Hii ni mistari bora kuishika kwa sababu ina mwitikio wa kimaandiko au ni mistari ambayo unaweza kuwashirikisha watu waliopotea pale wanapotoa udhuru yakini wa kutokuwa Wakristo.
- Nafasi za wazi zimeachwa kwa lengo kwamba mwanafunzi apate kuzijaza:
  - Udhuru, ambao haujaorodheshwa bado, unaweza kumsikia mtu asiyeamini akiutoa, yaani kinachomfanya yeye asiwe Mkristo.
  - Mwitikio wa kimaandiko, mstari ambao wanaukuta ndani ya Biblia unaotoa jibu kwa udhuru ulio yakini (wazi).
- Kuna mwitikio wa kimaandiko, mstari, kwa kila udhuru ambao mtu anaweza kuutoa wa yeye kutokuwa Mkristo.
  - Dawson Trotman, ambaye ndiye mwanzilishi wa Navigatora Ministry, aliwahi kumpa Mungu ahadi kwamba kamwe asingeweza kubambwa kwenye udhuru ule ule mara mbili. Mara tu aliposikia udhuru, aligundua jibu la udhuru huo ndani ya Biblia na kuushika ili kwamba awe na mstari, mwitikio wa kimaandiko, ili kuweza kushirikisha wakati mwingine baadaye anaposikia udhuru.

11. Jadili **Mlolongo wa Mistari Iliyoshikwa (iliyokaririwa)** (Ukurasa 238).

*Maelezo:*

- Waombe wanafunzi kuandika tarehe walipoanza kushika kwenye safu ya “Tarehe Uliposhikwa/kaririwa” baada ya kushika na kunukuu andiko rejea, mstari, maandiko rejea mara 30.
- Inachukua dakika tano au nane tu kunukuu andiko rejea, mstari, maandiko rejea mara 30 pindi mstari unapokuwa umeshikwa.
  - Ni wekezo lenye busara la muda wetu kushika mistari hii ili kwamba wakati wowote, Mungu anapotuletea kwenye kumbukumbu au akilini mwetu ipate kutubariki na pia iwabariki wengine.

  - Moja ya mistari hii inaweza kuwa tu ni kitu ambacho wewe au rafiki yako anahitaji kukiona au kukipata ili kushinda wakati wa majaribu.

12. Waonyeshe wanafunzi jinsi ya kuweka **Yohana 5:24** na **Yohana 10:28** kwenye kadi ya maandiko.

*Maelezo:*

- Fungua mfuko ulioko nyuma ya jarida la kijitabu kidogo, na uchukue kadi iliyo wazi kwa kila mstari utakaoukariri juma hili.
- Andika ile rejea ya Yohana 5:24 katikati ya kadi ya maandiko.
  - Andiko rejea ni kama anwani.
- Shikilia hiyo kadi kati ya kidole gumba na kidole chanda, halafu ikunje na iandike huo mstari upande mwingine wa kadi.
- Unapaswa kuwa na andiko rejea upande mmoja na mstari uliochapwa ama kuandikwa upande mwingine ili kwamba uweze kuutazama huo mstari na kuuona kama unaweza kunukuu hilo andiko rejea—ama kutazama kwenye andiko rejea na kuona ikiwa unaweza kunukuu huo mstari.
- Rudia zile hatua ukiwa na kadi nyingine kwa kutumia Yohana 10:28.
- Pindi unapokuwa umeshika mstari na kunukuu andiko lake rejea, mstari, andiko rejea mara 30, weka ile tarehe uliokashikwa/kaririwa upande ule ule wa kadi wa rejea ya andiko.

*Muhimu:*

- Chukua muda kuandika mistari hii kwenye kadi darasani ili wanafunzi waweze kuondoka nayo kwa juma zima na kuishika wakiwa katika kumngojea mtu, katika mapumziko, n.k. Kama hutafanya hivi darasani, Shetani ataweka vikwazo vingi kwa wanafunzi na kufanya iwe vigumu kwao kuipata mistari iliyokaririwa kabla hamjakutana tena.

- Kumbuka kushika mstari huuingiza kwenye akili zetu. Kutafakari huuhamisha kwenda mioyoni mwetu. Kwa hiyo tunashika mistari hii mapema iwezekanavyo katika juma hilo ili kuwa na muda wa kutafakari zaidi mistari hii kabla hatujakutana tena. Kwa nini tuitafakari? Tunataka Mungu aitumie mistari hii katika maisha yetu ili itubadilishe tuwe katika mfano wake.

*Kutafakri kweli tunazojifunza kutoka kwenye Biblia, hutusaidia kumjua Mungu.*

13. Wahamasishe wanafunzi kutafuta fursa za kuwashirikisha wengine mafundisho ya Neno la Mungu.

    ***Maelezo:*** Tunataka kuwasaidia wanafunzi kuwa na utulivu katika kuzungumza habari za Yesu katika maeneo yote ya maisha yao.

14. Tafuta kupata umakini wa wanafunzi kwa ajili ya **Kazi za Ziada** (Kurasa 253-254).

    ***Soma darasani:*** Ruhusu mmoja wao asome kwa sauti kazi uliyowapatia, na hakikisha kila mmoja ameelewa kazi ya ziada katika ukurasa 253.

    - ***Wahamasishe wanafunzi kuwa waaminifu kwa Mungu na kukutana Naye kila siku kwa ajili ya muda wao wa utulivu.***

15. Funga kwa Maombi.

    ***Mfano:*** Waalike wanafunzi kuungana nawe kupiga magoti mnapoomba pamoja na kumshukuru Mungu kwa ajili ya kukutana nanyi na kipekee kuzungumza na kila mmoja wenu.

## Mwongozo wa Kiongozi na Ujumbe wa Mwandishi........................Kipindi cha 8

1. Anza kwa maombi.

   ***Mfano:*** Waalike wanafunzi kupiga magoti pamoja nawe mnapoomba pamoja na kuukabidhi muda kwa Mungu.

2. Mtake kila mmoja kufungua katika karatasi ya **Ufuatiliaji** ambayo inahitajika siku hiyo. Kisha unaweza **kuzikagua na kuzisaini** (Ukurasa 279).

   ***Uwajibikaji: U****kaguzi na uwekaji sahihi karatasi zao za Ufuatiliaji kila juma huwafundisha wanafunzi katika kanuni ya uwajibikaji iliyofundishwa katika Warumi 14:12.*

3. Soma **"Kwa kuwa Kusudi langu la dhati ni kwamba Nimjue Yeye"** (Ukurasa 9). Mtake mtu mmoja kushirikisha Kuvuta taswira kwake sehemu moja ya mstari huu na kumsikiliza pale anaporudisha Maombi yake kwa Mungu kama ombi lake binafsi. **Wakumbushe wanafunzi kuweka mwelekeo wao kwa Yesu** (Waebrania 12:2).

   ***Kumbusho:*** Moja ya sababu kuu zinazotufanya tutathmini Wafilipi 3:10 (AMP) kila juma ni:

   - **Ili kuyaelekeza macho yetu kwa Yesu** na Yesu pekee yake na ili kutukumbusha kwamba **Kusudi letu la dhati ni kumjua Yeye**.

4. Mwombe mtu mmoja kushirikisha kisha **K**ufikiria kwa kina, **K**uvuta taswira, na **K**uombea tena kwa Mungu **Notsi za Mahubiri au Somo lake** (Kurasa 21-24).

   ***Rudia:***

   - Tunapaswa kuhudhuria ibada za kuabudu tukitarajia Mungu kuzungumza nasi. Pale anapozungumza nasi, tunapaswa kuwa tayari kuandika kile anachosema. Mara tunapokiandika, basi tunaweza kuutunza notsi mpaka tunapopata fursa ya kuzitafakari kweli hizo. Pale tunapotafakari (**K**ufikiria kwa kina, na **K**uombea kweli hizo tena kwa Mungu kama maombi), tunazihamisha kweli hizo kutoka vichwani mwetu kwenda mioyoni mwetu ambako zinaweza kufanya kazi kwa namna yake katika utekelezaji.

*Pale tunapotulia ili kutafakari juu ya notsi tulizozitengeneza wakati tunasikiliza Mungu anaposema nasi katika mahubiri, inatusaidia kumjua Yeye.*

5. Jadili **Maswali ya Marudio ya Kazi za Ziada** (Ukurasa 254).

   ***Maelezo:***

   - Tumia swali la 4 katika ukurasa 254 kuwahamasisha wanafunzi kuzungumza kwa wengine habari kuhusu Yesu na mambo ambayo Anawafundisha.
     - Mruhusu mmoja wao katika kundi kusimulia juu ya uzoefu unaotokana na juma lililopita wakati alipozungumza na mtu fulani kuhusu Yesu au kushirikisha kitu chochote ambacho Mungu amemfundisha.

6. Kusoma/Kujadili kwa kina mafunzo ya **Kuyajaza Maisha yako kwa Maombi** (Kurasa129-135). Unaposoma na kujadili, mara kwa mara tulia kidogo na kutoa nafasi kwa wanafunzi **K**ufikiria kwa kina, **K**uvuta taswira, na **K**uomba**.**

   **Kwa nini niyajaze maisha yangu kwa maombi?** (Ukurasa 130, Sehemu II)

   ***Ukurasa 130:***

   - Yeremia 33:3 (NKJV) inasema, *"Niite, nami nitakuiitikia, nami nitakuonyesha mambo makubwa magumu usiyoyajua."*

     ***Hadithi**:* Nilikuwa namfundisha mchungaji na kundi dogo la wanaume kutoka kanisani kwake huko Romania. Siku moja mchungaji aliniuliza kama nitapenda kusikia jinsi gani Mungu ameanzisha kanisa jipya kwa sababu lilihusisha mmoja wa wanaume ndani ya kanisa letu, ambaye tutamwita Joe. Nilikuwa na shauku ya kusikia, kwa hiyo alinisimulia hadithi.

     Siku moja Joe aliitwa na rafiki aliyekata tamaa, mtu asiyemwamini Mungu tutakayemwita Mike. Huko nyuma, Mike hakujali chochote kuhusu Mungu na alimdhihaki Joe na imani yake, lakini leo alikuwa

amebanwa. Mike alikuwa amepoteza sanduku lake dogo na lilikuwa na taarifa kuhusu watu ambazo zingesababisha matatizo makubwa kama taarifa hizo zingefahamika kwa umma. Alikuwa ametafuta karibu siku nzima hilo sanduku lake dogo lakini bila mafanikio. Hatimaye alimwita Joe, na kwa pamoja walitembea tena katika maeneo yale yale ambayo Mike alikuwa amepita siku nzima. Giza liliingia, kwa hiyo wakaacha, na Mike alikuwa amefadhaika. Mike alimuomba Joe kama angeweza kuomba kabla hawajaachana ili kwamba Mungu aweze kumsaidia kupata sanduku lake dogo. Joe alisema ataomba kwa ajili ya Mike ikiwa Mike atamuahidi kwenda naye kanisani kama Mungu atamrudishia tena sanduku lake dogo. Mike alikubali na alikwenda nyumbani, ambapo ilikuwa kama mwendo wa saa moja kutoka Bucharest ambako alikuwa amepoteza sanduku lake dogo.

Joe aliomba usiku ule kwamba Mungu amwezeshe Mike kuliona sanduku lake dogo. Baadaye siku iliyofuata asubuhi mwanamke aligonga mlangoni kwa Mike akiwa na sanduku lake dogo mkononi. Alisema kwamba alikuwa Bucharest mapema asubuhi ile na aliliona lile sanduku dogo limewekwa kando ya njia yenye shughuli nyingi. Bucharest ni jiji lenye karibu watu milioni tatu, mitaa imejaa watu kwa maelfu, na wazururaji au vibaka wanajulikana vizuri kwa kuiba chochote wanachokiona. Joe na Mike walikuwa wamepita mara kadhaa eneo hili ambako sanduku dogo lilipatikana, na halikuwepo pale usiku wa nyuma yake. Mungu alikuwa amefanya muujiza na kulirudisha sanduku dogo kwa Mike.

Mike alitunza ahadi yake na alikwenda kanisani na Joe. Mike alikuwa ameokoka na alianza kuwaleta watu kanisani pamoja naye kutoka kwenye mji aliokuwa akiishi. Aliendelea kuwaalika na kuwaleta watu pamoja naye mpaka siku moja aliposema, “Mchungaji sijui nifanye nini. Tunajaa magari mawili kuja kanisani kutoka kwenye mji wangu, na karibu tutahitaji gari jingine.” Mchungaji alimwambia Mike kwamba kanisa lao lilikuwa tayari kuanzisha kanisa jingine na kwamba tayari

wamelitambua hilo lakini kwa hilo wataahirisha kuanzisha kanisa hilo na kuanzisha moja katika mji wake. Walibadilisha mipango yao na kuanzisha kanisa mahali ambapo Mungu tayari alikuwa kazini. Wakati tunaondoka Romania, kanisa lilikuwa limeanza kwa takribani mwaka mmoja. Walikuwa wamebatiza watu kumi na nne na walikuwa na takribani watu hamsini wanaohudhuria kanisani.

*Kwa nini tuyayajaze maisha yetu kwa maombi? Mungu anafanya mambo makubwa pale tunapoomba.*

***Ukurasa 130:***

***Maelezo****:* Yohana 14:14 (NKJV) inasema, *"Kama mkiniomba neno lolote kwa jina langu nitawapa."*

- Je, maneno haya yanamaanisha nini: *Kwa jina langu*?
    - Kuomba kwa jina la Yesu hakumaanishi kumalizia tu maombi yetu kwa kutumia maneno "kwa jina la Yesu"—japokuwa hakuna ubaya wowote katika kusema maneno hayo ikiwa yanatoka moyoni. Ninaamini tunaomba kwa jina la Yesu pale tunapotambua kwamba hatustahili kuwa na mwingiliano wa moja kwa moja na Baba, lakini tumepewa upendeleo maalumu kwa sababu Yesu alikufa juu ya msalaba kwa ajili ya dhambi zetu. Kwa hiyo, hatuwezi kumwendea kwa majina yetu wenyewe lakini kwa jina la Mwanaye, tukikumbuka nini Yesu alikifanya kwa ajili yetu juu ya msalaba.

      ***Kielelezo:*** Kati ya mifano hii miwili ni upi unaonyesha hali ambayo ungependa kuhusika nayo kuhusu kusaidia?

      ***Mfano #1***—Ukiwa mtaani, mtu fulani anakuja kwako na kukuomba kiwango kikubwa cha pesa.

      ***Mfano #2***—Mtu mwingine anakuja kwako na kusema, "Mimi ni rafiki wa mwanao. Nina tatizo kubwa, na nimemwambia mtoto wako juu ya hili. Ameniambia kwamba kama nikija kwako na kukushirikisha tatizo langu, utanisaidia."

Ni yupi kati ya watu hawa wawili unafikiri utavutiwa naye zaidi katika kumsaidia? Ni yule aliyekuja kwako kwa jina la mwanao.

***Ukurasa 131:***

***Maelezo****:* Wafilipi 4:6 (JBP) inasema, ***"Msijisumbue kwa neno lolote;*** *mweleze Mungu kila kipengele cha mahitaji yako kwa bidii na maombi ya shukurani."*

- Hapa tunaona kanuni ya muhimu san—**Usijisumbue kwa jambo lolote; omba juu ya kila kitu**.
    - Kuwa na wasiwasi ni dhambi kwa sababu inaakisi upungufu wa imani na ujasiri kwa Yesu.
    - Wakati mwingi mambo tunayojisumbua nayo yamejengwa katika mtazamo potofu katika akili zetu.

***Hadithi***: Mara nyingi wakati wa kipupwe, ndege wekundu walio katika jozi huja kujenga kiota nyuma ya nyumba yetu. Wakati mwingine dume, ambaye ndiye mmiliki mkuu, huweza kuiona taswira yake kwenye kioo chetu kikubwa dririshani na mara kwa mara hulishambulia dirisha, akijaribu kufukuza kwenye himaya yake ile taswira yake mwenyewe anayoiona. Mwaka mmoja ndege huyu dume alikuwa na wasiwasi sana na akazidiwa na hofu mpaka akajiua mwenyewe kwa kujipigiza kwenye kioo. Mwaka ule ndege mwekundu dume alishambulia dirisha alfajiri wakati wa mapambazuko. Anarudia tena kufanya mashambulizi kwenye dirisha siku nzima na kisha anarudi tena kwa shambulizi moja la mwisho kabla ya giza kuingia. Hofu hii ilisababishwa na mtazamo wake potofu, kwa hakika iligharimu maisha yake. Ni wakati wa kipupwe, na anapaswa, na anaweza kufurahia ulimwengu mzuri wa Mungu. Wasiwasi mwingi umejengwa katika mtazamo potofu. **Usiruhusu wasiwasi kuharibu maisha yako. Usijisumbue kwa jambo lolote; omba katika kila jambo**. Mungu anakupenda, na Yeye ndiye mdhibiti.

***Maelezo:*** 1 Wathesalonike 5:18 inasema, *"Shukuruni kwa kila jambo, maana hayo ni mapenzi ya Mungu kwenu katika Kristo Yesu."*

- Sasa angalia maneno ambayo takribani yanakaribiana na kifungu cha maneno hayo katika vifungu vifuatavyo katika ukurasa 132.

***Ukurasa 132:***

- Efeso 5:20 (RSV) inasema, *"Na kumshukuru Mungu Baba siku zote kwa mambo yote, katika jina lake Bwana wetu Yesu Kristo."*

  ***Msisitizo:*** 1 Wathesalonike 5:18 ukurasa 131 inasema, *"**katika** kila jambo"* na Efeso 5:20 (RVV) kwenye ukurasa 132 inasema *"**kwa** mambo yote"* shukuruni.

  - Wote tunaweza kufikiria hali ambazo zinaweza kuwa ngumu sana katika maisha. Kwa hiyo kwa nini Mungu alitake hilo kwetu?

  - 1 Wathesalonike 5:18 inasema *"..... maana haya ni mapenzi ya Mungu."*
  - 1 Petro 1:6-7 (NIV) inaseama, "*...ijapokuwa sasa kwa muda mfupi, ikiwa ni lazima, mmehuzunishwa kwa majaribu ya namna mbalimbali; ili kwamba kujaribiwa kwa imani yenu, ambayo ina thamani kuu kuliko dhahabu ipoteayo, ijapokuwa hiyo hujaribiwa kwa moto—kuonekane kuwa kwenye sifa na utukufu na heshima, katika kufunuliwa kwake Yesu Kristo."*

  - Mwamini wa kweli kamwe hakosi TUMAINI kwa sababu Yesu ndiye tumaini letu (Zaburi 71:5), na Aliahidi kwamba kamwe hatatuacha au kutupungukia (Waebrania 13:5). Kupitia Bwana wetu Yesu Kristo tunao ushindi hata dhidi ya mauti (1 Wakorintho 15:55-57).

  - 1 Wathesalonike 4:13-14; 17-18 (JBP) inasema, *"Sasa, ndugu, hatutaki msijue habari zao 'waliolala' mauti, ama msije mkahuzunika kama na wengine wasio na matumaini. Hata hivyo, ikiwa tunaamini ya kwamba Yesu alikufa akafufuka kutoka kwa wafu, vivyo hivyo na hao 'waliolala' katika Yeye...Na*

*baada ya hayo tutakuwa pamoja na Bwana milele. Kwa hiyo kwa namna yoyote tumieni ujumbe huu kufarijiana ninyi kwa ninyi."*

***Ukurasa 133:***

- Yakobo 5:16 (NKJV) katika ukurasa huu inasema, *"... Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana akiomba kwa bidii."* Maombi yenye bidii ni yapi?

  ***Maombi ya aina mbili tofauti yenye bidii:***

  ***Hadithi #1***—Wakati kijana wetu, Steve, alipokuwa na miaka mitano hivi, mchungaji wetu alikuwa na tatizo la mgongo kwa muda mfupi. Kwa karibu majuma matatu hakuweza kusimama wima na alihitaji mkongojo ili kutembea. Jumamosi moja usiku tulipokuwa tumepiga magoti pembeni ya kitanda cha Steve tukiomba, Steve alimuomba Mungu kumponya mchungaji wake. Yalikuwa ni maombi mafupi ya kimyakimya bila msisimko. Asubuhi iliyofuata tulitembea kuelekea kwenye ukumbi wa kanisa letu, tulimuona mchungaji amesimama wima amenyooka na akitembea bila mkongojo. Steve alisema neno moja tu: "Angalia!" Steve alikuwa ameomba maombi ya kumaanisha na kweli kutoka moyoni mwake na aliamini kwamba Mungu atajibu, kwa hiyo hakushangazwa pale alipoona kwamba Mungu amejibu maombi yake. Tunaamini maombi ya Steve yalikuwa ni maombi ya bidii.

  ***Hadithi #2***—Miaka kadhaa baadaye wakati kijana wetu mdogo, Don, akiwa na miaka mitano au sita hivi, alikuwa na samaki wake mdogo aliyemfuga. Bakuli la kufugia lilihitaji kusafishwa, lakini Marilyn alikuwa na haraka na aliamua kulisafisha kwa haraka haraka tu, kwa hiyo akaliweka bakuli la samaki chini ya bomba kwenye sinki la bafuni na akayaacha maji kutiririka moja kwa moja kwenye bakuli. Maji ya zamani yalikuwa yakilazimishwa kutoka kupitia juu ya bakuli na kumwagika chini kwenye mfereji. Kila kitu kilikuwa vizuri mpaka samaki yule alipozidiwa na maji na kutokea juu na kuanza kuzolewa kuingia kwenye mfereji. Marilyn aliitikia kwa haraka kwa kuvuta kifuniko ili kufunga mfereji, lakini samaki alikanaswa kwenye kizibo. Samaki alijikunza katika umbo la *L*, akiwa amepoteza uhai.

Wakati huu huo Don aliingia bafuni. Alipoona kile kilichotokea, alianza kulia kwa sauti kubwa, “Umemuua samaki wangu mdogo! Umemuua samaki wangu mdogo! Na alikuwa sahihi. Don aliendelea kulia na kumsihi Mungu asiruhusu samaki wake kufa. Tena na tena alimsihi Mungu katika maombi, “Mungu, tafadhali usiruhusu samaki wangu kufa.”

Hatimaye, ilikuwa ni wakati wa kwenda kulala na Marilyn alimrudisha tena samaki ndani ya bakuli ili tu kumridhisha Don. Don alikuwa amechanganyikiwa kabisa na aliendelea kulia na kumsihi Mungu, “Tafadhali usiruhusu samaki wangu mdogo kufa.” Lakini samaki alikuwa amejikunja kwenye umbo la *L*, asiye na uhai na akielea juu ya maji tumbo lake likiwa juu (dalili kwamba samaki amekufa). Wote tulikwenda kulala, japokuwa Don alikuwa bado analia na kumsihi Mungu.

Asubuhi iliyofuata wakati tulipoamka, samaki mdogo wa Don hakuwa tena kwenye umbo la *L* na hakuwa mfu tena. Alikuwa akiogolea akizunguka ndani ya bakuli kama vile hakuna kitu kilichotokea! Maombi haya kutoka kwenye moyo wa Don yalikuwa ya sauti kubwa na yenye hisia kali. Tunaamini maombi ya Don yalikuwa pia yenye bidii.

> ***Kulinganisha:*** Ombi moja lilikuwa na hisia kali na moja halikuwa na hisia, lakini yote mawili yalikuwa ya kumaanisha na yalikuwa maombi ya kweli kutoka kwenye mioyo ya vijana walioamini kwamba Mungu anaweza kusikia na kujibu maombi yao. Kwa hiyo wote wawili walikuwa na maombi yenye bidii.

*Kutafakari juu ya kweli tulizojifuna katika Usomaji wa Biblia kunatusaidia kumjua Mungu.*

7. Wewe, Kiongozi, shirikisha **Notsi za kila siku katika Kusoma Biblia (NKSKB)** (Kurasa 65-72) ulizozitengeneza katika juma hili lililopita:

    a. **S**hirikisha notsi zako, moja au mbili.

    b. **F**ikiria kwa kina juu ya notsi zako.

    c. **V**uta taswira ya notsi zako.

***Kumbuka*** kwamba kuvuta taswira ya notsi hakumaanishi kuzielezea notsi. Kwa hiyo, pale unaposhirikisha kuvuta taswira kwako, anza kwa kusema, **“Hii ndiyo picha ninayoiona.”**

d. **O**mbea notsi zako kwa Mungu kama maombi yako binafsi ya **K-K-K-K**.

***Unapoomba***—Ruhusu wanafunzi kusikiliza unaporudisha maombi yako kwa Mungu kama maombi yako binafsi ya **K**uabudu, **K**uungama, **K**ushukuru au **K**uomba kwa unyenyekevu.

***Maelezo:***

- Leta ukurasa wa Notsi zako za **NKSKB** darasani, na soma notsi zako, moja au mbili.
- Kuonyesha jinsi ya kufanyia mazoezi hili katika maisha yako mwenyewe kunaweza kuwasaidia wanafunzi kuona au kuelewa jambo fulani ambalo hawakuelewa ulipolielezea mara ya kwanza jinsi ya kulifanya.

***Ushuhuda****:* Hili ni eneo nzuri kwako, kiongozi, kuwashirikisha msisimko wako juu ya jinsi usomaji wa Neno la Mungu kila siku, kutengeneza notsi, na kutafakari juu ya notsi hizo kunafanya kitu cha tofauti katika maisha yako mwenyewe.

***Kutengeneza notsi siyo mwisho wa mambo***, ni chombo cha kukukumbusha kile Mungu alichosema kwetu ili kwamba tuweze kutafakari juu ya kweli hizo na kumjua Mungu.

8. Muombe kila mmoja kwa kunukuu Yohana 5:24 (**KKK**).
9. Muombe kila mtu kunukuu Yohana 10:28 (**KKK**).
10. Kurudia **Mpango wa Kushika** (Ukurasa 236).

***Marudio:*** Kama tutaufanyia kazi mpango, mpango utatufanyia kazi.

- Kushika mstari kunaingiza kwenye akili zetu. Kuutafakari mstari kunauingiza mioyoni mwetu, na mara unapokuwa mioyoni mwetu, tunaweza kuutumia katika maisha yetu.

***Hadithi**:* Huko nyuma, nilishangaa kwa nini niliweza kushika mstari na kisha nisiukumbuke wiki inayofuata. Niliona kwamba ufunguo utakaonisaidia ni kifungu cha 2 (f) kwenye ukurasa 236, ambacho kilinihamasisha kuhakiki au kutathmini mstari huu mara moja baada ya kuwa nimeushika kwanza kwa kunukuu rejea, mstari, rejea, mara 30. Jambo lingine ambalo lilinisaidia ni kunukuu mstari mara kwa mara pale ninapowashirikisha wengine. Tukiwa na mistari, tunaweza kuitumia au kuipoteza.

*Kushika andiko kunatusaidia kulijua Neno la Mungu, na kutafakari kunatusaidia kumjua Mungu.*

11. **Marudio ya Mlolongo wa Mistari Iliyoshikwa** (Ukurasa 238).

***Marudio:***

- Waambie wanafunzi kwamba tunaandika tarehe tuliyoshika kwenye safu ya “Tarehe uliposhika” tunapokuwa tumeuchunguza au kuuhakiki mstari mara moja baada ya kuwa tumeushika kwanza kwa kunukuu rejea, mstari, rejea mara 30.
- Inachukua kama dakika tano mpaka nane tu kunukuu rejea, mstari, rejea mara 30 mstari unapokuwa umeushika.
    - Ni busara kuwekeza muda wako ili uweze kushika mistari hii ili kwamba, wakati wowote, Mungu aweze, kuileta katika akili yako kukunufaisha wewe au watu wengine.
    - Moja ya mistari hii inapaswa kuwa jambo ambalo wewe au rafiki yako anahitaji kukuona wewe ukiitumia unapopita katika nyakati ngumu.

12. Watake wanafunzi kuweka mistari ifuatayo kwenye kadi za maandiko (Ukurasa 235):

- **1 Wakorintho 10:13**
- **2 Wakorintho 12:9**

***Marudio:***

- Fungua mfuko wa ndani ulio nyuma ya kijitabu kidogo na chukua kadi iliyo wazi kwa ajili ya kila mstari utakaoshika juma hili.
- Andika rejea *1Wakorintho 10:13* katikati ya moja ya kadi hizo.
    - Rejea ni kama anwani.
- Unapaswa kuwa na rejea za maandiko upande mmoja na mstari uliochapwa au ulioandikwa upande mwingine ili kwamba uweze kuuangalia mstari na kuona kama unaweza kunukuu rejea – au kuangalia katika rejea na kuona kama unaweza kuunukuu mstari.
- Rudia hatua na kadi nyingine, tumia 2Wakorintho 12:9
- Mara unapokuwa umeushika mstari na kunukuu rejea, mstari, rejea mara 30, weka tarehe uliyoshika upande huo huo wa kadi kama rejea ya andiko.

***Muhimu:***

- Toa muda ili kuandika mistari hii kwenye kadi darasani ili kwamba wanafunzi waweze kuzibeba kwa juma zima na kuikariri wakati wanamsubiri mtu fulani, au wamekwama kwenye foleni, au wanapopumzika, n.k. kama hutafanya hilo darasani, Shetani ataweka vikwazo kwa wanafunzi na kufanya hilo kuwa gumu kwa wao kupata mistari ya kukariri kabla ya kukutana tena.

- Kumbuka kwamba kushika mstari kunaufanya kuingia katika akili zetu. Kutafakari kunauhamisha kwenda kwenye mioyo yetu. Kwa hiyo, tunashika mistari mapema kadri iwezekanavyo katika juma ili tuwe na mistari mingi ambayo tutaitafakari kabla ya kukutana tena. Kwa nini tuitafakari? Tunataka Mungu kuitumia katika maisha yetu kutubadilisha katika mfano Wake.

*Kushika na kutafakari andiko kunatusaidia kumjua Mungu**.***

13. Wahamasishe wanafunzi kuonyesha upendo wao kwa Mungu mara tatu kila saa wanayokuwa macho juma hili *"Ninakupenda, Ee Bwana, uliye nguvu zangu"* (Zaburi 18:1 NIV).

***Maelezo:***

- Tunaposema, "Bwana, Nakupenda," tunaomba maombi ya kumwabudu Mungu

- Tunataka kuendeleza hali ya kuonyesha upendo wetu kwa Mungu siku nzima kila siku. Mazoea haya ni sehemu muhimu ya kanuni za kibiblia katika mabadiliko ya maisha ambayo tutajifunza ndani ya majuma mawili.

***Kumbusho****:* Wanafunzi wanaweza kuhitaji kitu fulani ili kuwakumbusha kusema, "Bwana, Ninakupenda" siku nzima.

- Kama inawezekana, mpe kila mwanafunzi kinukta kidogo au kitu fulani atakachokiweka kwenye saa yake, kioo cha kuangalia nyuma cha gari, kompyuta, n.k. kitu chochote kinachoweza kuwa kichocheo cha kumkumbusha mwanafunzi kumwambia Bwana "ninakupenda" siku nzima.

14. Wahamasishe wanafunzi kutafuta fursa za kushirikisha kile Mungu anachowafundisha.

    ***Maelezo****:* Tunataka kuwasaidia wanafunzi kuwa na utulivu katika kuzungumza habari za Yesu katika maeneo yote ya maisha yao.

15. Tafuta umakini wa wanafunzi kwa **kazi** zao za **Ziada** (Kurasa 255-256).

    ***Soma darasani****:* Toa muda ili kusoma ukurasa 255 kwa sauti darasani, na hakikisha kwamba kila mmoja anaielewa kazi ya ziada.

    - ***Wahamasishe wanafunzi kuwa waaminifu kwa Mungu na kukutana Naye kila siku kwa ajili ya muda wao wa utulivu.***

16. Funga kwa maombi.

    ***Mfano:*** Waalike wanafunzi kuungana nawe kupiga magoti mnapoomba pamoja na kumshukuru Mungu kwa ajili ya kukutana nanyi na kipekee kuzungumza na kila mmoja wenu.

## Mwongozo wa Kiongozi na Ujumbe wa Mwandishi........................Kipindi cha 9

1. Anza kwa maombi.

   *Mfano:* Waalike wanafunzi kupiga magoti pamoja nawe mnapoomba pamoja na kuukabidhi muda kwa Mungu.

2. Mtake kila mmoja kufungua katika karatasi ya **Ufuatiliaji** ambayo inahitajika siku hiyo. Kisha unaweza **kuzikagua na kuzisaini** (Ukurasa 280).

   ***Uwajibikaji:*** Ukaguzi na uwekaji sahihi karatasi zao za Ufuatiliaji kila juma huwafundisha wanafunzi katika kanuni ya uwajibikaji iliyofundishwa katika Warumi 14:12.

3. Soma **"Kwa kuwa Kusudi langu la dhati ni kwamba Nimjue Yeye"** (Ukurasa 9). Mtake mtu mmoja kushirikisha Kuvuta taswira kwake sehemu moja ya mstari huu na kusikiliza pale anaporudisha Maombi yake kwa Mungu kama ombi lake binafsi. **Wakumbushe wanafunzi kuweka mwelekeo wao kwa Yesu** (Waebrania 12:2).

   ***Kumbusho:*** Moja ya sababu kuu zinazotufanya tutathmini Wafilipi 3:10 (AMP) kila juma ni:

   > **Ili kuyaelekeza macho yetu kwa Yesu** na Yesu pekee yake na ili kutukumbusha kwamba **Kusudi letu la dhati ni kumjua Yeye**.

4. Mwombe mtu mmoja kushirikisha kisha **K**ufikiria kwa kina, **K**uvuta taswira, na **K**uombea tena kwa Mungu **Mahubiri au Ujumbe wa somo lake** (Kurasa 21-24).

5. Jadili **Maswali ya Marudio ya Kazi za Ziada** (Ukurasa 256).

   ***Maelezo:***

   - Tumia swali la 5 kwenye ukurasa 256 ili kuwahamasisha wanafunzi kuzungumza kwa wengine habari za Yesu na mambo ambayo amewafundisha.
   - Ruhusu mtu mmoja katika kundi kusimulia uzoefu unaotokana na somo la juma lililopita wakati alipozung-

umza na mtu yeyote juu ya Yesu au kushirikisha jambo lolote ambalo Mungu anamfundisha.

6. Soma/jadili kwa kina mafunzo ya **Jinsi gani naweza Kuyajaza maisha yangu kwa Moambi?** (Kurasa 135-146). Unaposoma na kujadili, mara kwa mara tulia na kuwapa wanafunzi fursa ya **K**ufikiria, **K**uvuta taswira na **K**uomba kwa unyenyekevu**.**

   ***Kurasa 136-140:*** Katika sehemu hii, "Jinsi gani naweza kuyajaza maisha yangu kwa Maombi?" Kuna sifa sita zilizofichika kwa ajili ya maombi.

   - Ni kweli kwamba Mungu anaweza kufanya lolote analotaka kufanya, kwa hiyo, anaweza kujibu ombi lolote kwa wakati wowote hata kama hatujatimiza masharti yake. Anaweza kufanya hivyo tu kwa sababu Yeye ni Mungu.
   - Je kuna jambo lolote tunaloweza kufanya ili kwamba Mungu asike na kujibu maombi yetu sawa sawa na vile tunavyotaka yajibiwe?
     - Katika maandiko, tunaona hapa chini kuna sifa sita kwa ajili ya maombi yaliyojibiwa:
       1. Marko 11:25 (NIV) kwenye ukurasa 138—***<u>MSAMAHA</u>:***
          - Kama tunataka kusamehewa, ni lazima tuwasamehe wengine. Kusamehe maana yake, "kuacha, kuondoka, na kuachilia." Kama tunaweka vinyongo, hatutakuwa na uhakika kwamba Mungu atasikia na kujibu maombi yetu.
       2. 1 Yohana 1:9 kwenye ukurasa 138—***<u>kwenye ukurasa </u>:***
          - Mungu ni mwaminifu hata atusamehe na kututakasa sisi pale tunapoungama dhambi zetu. Mstari uliotangulia, Isaya 59:2, unaelezea kwamba tunahitaji msamaha kwa sababu dhambi huharibu ushirika wetu na Mungu, inatutenga sisi katika kuupata ushirika na Mungu ambao tuliumbwa ili kuufurahi.

***Marudio***: Hapa ni mahali pazuri kuelezea tofauti kati ya uhusiano na Mungu na ushirika na Mungu.

- Mara tunapoweka imani yetu kwa Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi wetu binafsi, Mungu anaweka ulinzi na hakuna awezaye kutuondoa mikononi mwake (Yohana 10:28). Milele tunakuwa na **uhusiano na Mungu** (Yohana 1:12). Hakuna nguvu katika ulimwengu iliyo na uwezo wa kuweza kutuondoa sisi mikononi mwake kwa sababu Mungu ndiye mwenye nguvu kubwa mbinguni na duniani (Mathayo 28:18). Kwa hiyo katika uhusiano, Mungu ndiye anayetushikilia sisi wakati wote wa wokovu wetu (Yohana 5:24).

  **Katika ushirika, tunajishikilia kwa Mungu**. Pale tunapotenda dhambi, tunajitenga wenyewe mbali na Mungu na ushirika wetu na Mungu unavunjika (Isaya 59:2). Kumbuka kwamba Mungu ndiye *"aliyekuita (tuita sisi) katika ushirika na Mwanaye Yesu Kristo Bwana wetu*"…. (1Wakorintho 1:9 NIV). Yeye hataki ushirika kuvunjika, kwa hiyo, pale tunapotenda dhambi, ni lazima **tuitubie mara moja dhambi hiyo** (1Yohana 1:9) na kuachilia udhibiti wa maisha yetu tena kwa Mungu (Warumi 6:13).

  ***Kielelezo***: Vuta taswira Mungu akiwa na mikono iliyonyooshwa. Mkono wa Mungu wa kulia unawakilisha uhusiano wetu na Mungu na mkono wa Mungu wa kushoto unawakilisha ushirika wetu na Mungu. **Katika mkono wake wa kulia** tunajiona wenyewe

tukipumzika kwa amani na usalama kwa sababu tunajua kwamba hakuna kitakachotuondoa mikokoni Mwake. **Uhusiano wetu uko salama kwa sababu anatushikilia sisi**. Katika ushirika unauona mkono wake wa kushoto umenyooshwa, na sisi tunajiona kama mtoto akishikilia kidole cha Mungu. Pale tunapotenda dhambi, tunaruhusu ushirika wetu kuvunjika. **Ushirika wetu na Mungu hauko salama ukilinganishwa na uhusiano wetu na Mungu kwa sababu tunawajibika kwa ajili ya ushirika wetu, na wakati mwingine tunatenda dhambi**.

***Mifano:***

- Tunao watoto wawili wa kiume. Wangeweza kuamua kwamba hawataki mimi niwe baba yao na kwenda mahakamani kutaka majina yao yabadilishwe. Au wangeweza kusema kwamba mimi siyo baba yao. Lakini mimi ni baba yao, na hakuna kinachoweza kuubadili ukweli huo. Hata mwana mpotevu bado alikuwa ni mtoto kwa baba yake (Luka 15:11-32). Kwa namna hiyo hiyo, **mara tunapofanyika wana wa Mungu, tunabakia kuwa hivyo kuwa watoto wake siku zote (Yohana 5:24). Huu ni mfano wa uhusiano**.

- Uhusiano kati ya mimi na watoto wangu wawili hauwezi kuvunjika, lakini wanapoasi, ushirika wetu unavunjika. Hata hivyo, siku zote, msamaha unakuja baada ya kuungama kwao (1 Yohana 1:9). Kwangu

mimi, baba yao, japokuwa dhambi zao zingewezakuwa nyekundu kama bendera, pale wanapoziungama na kusamehewa, wanakuwa weupe kama theluji (Isaya 1:18). Uhusiano wetu unarejeshwa. **Huu ni mfano wa ushirika**.

3. Yohana 14:13 (NKJV) ukurasa 139—***OMBA KWA JINA LA YESU***:

***Marudio***—Kuomba kwa jina la Yesu hakumaanishi kumalizia tu maombi yetu kwa kutumia maneno "kwa jina la Yesu" – japokuwa hakuna ubaya wowote katika kusema maneno hayo ikiwa yanatoka moyoni. Ninaamini tunaomba kwa jina la Yesu pale tunapotambua kwamba hatustahili kuwa na mwingiliano wa moja kwa moja na Baba, lakini tumepewa upendeleo maalumu kwa sababu Yesu alikufa juu ya msalaba kwa ajili ya dhambi zetu. Kwa hiyo, hatuwezi kumwendea kwa majina yetu wenyewe lakini kwa jina la Mwanaye, tukikumbuka kile alichokifanya Yesu kwa ajili yetu juu ya msalaba.

***Kielelezo:*** Kati ya mifano hii miwili ni upi unaonyesha hali ambayo ungependa kuhusika nayo katika kusaidia?

***Mfano #1***—Ukiwa mtaani, mtu fulani anakuja kwako na kukuomba kiwango kikubwa cha pesa.

***Mfano #2***—Mtu mwingine anakuja kwako na kusema, "Mimi ni rafiki wa mwanao. Nina tatizo kubwa, na nimemwambia mtoto wako juu ya hili. Ameniambia kwamba kama nikija kwako na kukushirikisha tatizo langu, utanisaidia."

Ni yupi kati ya watu hawa wawili unafikiri utavutiwa naye zaidi katika kumsaidia? Ni yule aliyekuja kwako kwa jina la mwanao.

4. Yakobo 1:6-7 kwenye ukurasa 139—
***<u>OMBA KWA IMANI, AMINI KUWA UTA-POKEA</u>:***

- Mtu anayeona shaka kwamba atapokea jibu kutoka kwa Mungu kwa hakika hatapokea. Kabla Yesu hajamponya mtoto aliyepagawa na mapepo, Yesu alisema kwa baba wa kijana, “Yote yawezekana kwake yeye aaminiye.” Mara moja baba akasema, *“Naamini, nisaidie niweze kushinda kuto amini kwangu”* (Marko 9:23-24 NIV). “Kama ukiamini, utapokea chochote unachoomba katika sala” (Mathayo 21:22 NIV). *“Hata sasa hamjaomba neno lolote kwa jina langu. Ombeni nanyi mtapata, na furaha yenu itatimia”* (Yohana 16:24 NIV).

  ***Nukuu:*** “Kuamini kwamba Bwana atasikia maombi yangu kunaheshimu Ukweli wake, nguvu zake, upendo wake, ukarimu wake, na hekima yake.”

  —Charles Haddon Spurgeon

5. Mathayo 26:39 (NKJV) kwenye kurasa 139-140—
***<u>OMBA KWAMBA MAPENZI YA MUNGU YAFANYIKE</u>:***

- Hili ndilo jambo la muhimu zaidi ambalo tunaweza kulifanya ikiwa tunataka kuwa na uhakika Mungu atasikia na kujibu maombi yetu. Hakuna kinachoonyesha imani yetu zaidi kuliko sisi kuwa na ujasiri zaidi katika Mungu kwamba tunataka mapenzi yake zaidi kuliko hata mapenzi yetu wenyewe. Ni kukubali kwamba tunatambua kwamba tupo hapa katika ulimwengu huu ili kuliishi kusudi ambalo ametuitia.

  ***Marudio:***

  ***Mapenzi yetu***—Pale tunapofika mahali ambapo tunakuwa na ujasiri mkubwa katika Mungu kiasi kwamba tunataka mapenzi yake zaidi kuliko tunavyotaka mapenzi yetu wenyewe,

basi tunayachukua mapenzi yake kama yetu wenyewe.

- Katika Mathayo 26:39 (NKJV), tunayo picha nzuri sana ya Yesu katika maombi. Tunamwona akimwomba Baba. *"... Ikiwezekana, kikombe hiki kiniepuke; lakini si kama nitakavyo mimi, bali kama utakavyo wewe."*
    - Inawezekana huu ndio ulikuwa uamuzi mgumu ambao Yesu alizimika kuukabili kwa sababu "Kikombe hiki" kinawakilisha dhambi zetu, na hii inamaanishat:
        - Alipaswa kuzichukua dhambi zetu zote juu yake Mwenyewe ili kuomba kwa ajili ya dhambi zetu. Fikria juu ya hilo. Kamwe hakuwahi kutenda dhambi au kuwa na hatia au aibu iliyotokana na dhambi.
        - Kwa sababu Yesu alikuwa radhi kuwa mtii na kuchukua dhambi zetu juu yake mwenyewe, dhambi zetu zingepaswa kumtenga Yeye na Baba. Fikiria juu ya hilo. Yesu kamwe hakuwahi kutengwa na Baba.
    - Pale Yesu aliposema, *"... wala-kini si kama nitakavyo mimi, bali kama utakavyo wewe."* Alionyesha mfano kwamba siku zote tunapaswa kutaka mapenzi ya Mungu yawe juu ya mapenzi yetu, bila kujali gharama.

6. 1 Yohana 3:22 (AMP) kwenye kurasa za 140—***<u>JIZOEZE KUWA NA MSIMAMO WA UTII</u>:***

- Utii huleta baraka, na mazoea ya utii yanampendeza Mungu kipekee. Mazoea ya utii huja pale tunapojizoeza msimamo wa utii. **MSIMAMO WA UTII ni mtazamo ambao unasema, "Bwana, nitakutii; Wewe sema tu."** Uamuzi wa kutii ulikwisha fanywa kabla hatujajua nini Mungu anatutaka kufanya.

    - ***Mfano:*** Petro anatupatia mfano mkubwa wa **MSIMAMO** huu **WA UTII** pale anaposema, *"Bwana tumefanya kazi ya kuchosha usiku kucha, na hatujapata kitu: lakini* ***kwa neno lako nitazishusha nyavu****"* (Luka 5:5). Tunao uthibitisho kwamba alikuwa tayari ameamua kutii chochote Yesu atakachomwambia kufanya. Alikuwa amejizoeza kuwa na MSIMAMO WA UTII.

**Katika muhtasari, hapa chini kuna sifa sita kwa ajili ya maombi yanayojibiwa tulizoziona katika maandiko:**

1. **Wasamehe wengine.**
2. **Ungama dhambi zako.**
3. **Omba katika Jina la Yesu.**
4. **Omba kwa imani; Amini kuwa utapokea.**
5. **Omba kwamba mapenzi ya Mungu yafanyike.**
6. **Jizoeze kuwa na Msimamo wa Utii.**

***Ukurasa 143, sehemu B****:* Kuendeleza ushirika binafsi wa karibu na Mungu katika maombi ni mradi wa kudumu (maisha yote).

***Kurasa 144-145, sehemu C:*** TMaisha yasiyo na nidhamu ni maisha yaliyopotea na yasiyo na utii. Nidhamu ni sehemu kubwa ya utii, na utii ni ufunguo katika ukuaji na ukomavu wa kiroho. Usitegemee kuona ukuaji wa kiroho ulio makini bila kuwa na nidhamu.

***Kurasa 145-146, sehemu D:*** Weka umakini katika siku moja tu kwa wakati.

*Marudio:*

- Hii ni moja ya kanuni muhimu zilizofundishwa katika Neno la Mungu—**Ishi siku moja kwa wakati**. Zungumza na Mungu leo katika maombi.

- Mbinu ya Shetani ni kutenda kwa siri. Yeye ni mjanja sana hata kutuambia kwamba kuomba leo ni upuuzi. Anajua tunaweza kushtukia mtindo huo. Anachofanya, ni kunong'oneza kwenye masikio yetu, "Kuomba leo ni wazo zuri, lakini una mambo mengi sana leo, na tayari umeshachelewa. Kwa nini usisubiri mpaka kesho? Fikiri juu ya hilo!

- Wakati wo wote tunaposhindwa kuzungumza na Mungu juu ya mambo yanayotuhusu, Shetani anapata ushindi.

*Kutafakari katika kweli tunazojifunza katika Usomaji wa Biblia hutusaidia kumjua Mungu.*

7. Jadili **Notsi za kila siku katika Kusoma Biblia (NK-SKB)** (Kurasa 65-72) walizotengeneza wanafunzi juma lililopita. Waombe watu wawili au watatu :

   a. **K**ushiririka moja ya notsi zao.

   b. **K**ufikiria kwa kina juu ya notsi hizo.

   c. **K**uvuta taswira ya notsi hizo.

   d. **K**uombea notsi hizo kwa Mungu kama moambi binafsi ya **K-K-K-K**. Baada ya kuwa wamemaliza, uwe mhamasishaji au mtia moyo kwao.

   *Kuombea notsi hizo kwa Mungu kama moambi binafsi ya K-K-K-K. Baada ya kuwa wamemaliza, uwe mhamasishaji au mtia moyo kwao.*

8. Muombe kila mtu kunukuu, kisha mtake mmoja wao afanye **KKK**

   - 1 Wakorintho 10:13.

9. Muombe kila mtu kunukuu, kisha mtake mmoja wao afanye **KKK**

    - 2 Wakorintho 12:9.

10. Soma/Jadili na kutafakari juu ya (**KKK**) kweli zilizo katika **“Tahadhari….Tahadhari….Tahadhari”** (Kurasa 25-27).

    ***Ukurasa 25:***

    - Moja ya mambo tunayotaka kujifunza kutoka kwenye “Tahadhari…Tahadhari….Tahadhari” ni umihimu wa kuyatazama maisha kutokana na mtazamo wa Mungu, kwa msimamo sahihi wa moyo.

        ***Kielelezo****:* Kuteleza kwa ubao juu ya mapovu ya mawimbi ya maji ni tatizo kwa mwogeleaji—bali ni furaha kwa mtelezaji. Inategemea na mtazamo wako.

    - Andika mstari huu katika kitabu chako kidogo cha mwanafunzi, chenye kichwa “Tahadhari…Tahadhari….. Tahadhari” *“Wapenzi, msione kuwa ni ajabu ule msiba ulio kati yenu, unaowapata kama moto ili kuwajaribu, kana kwamba ni kitu kigeni kiwapatacho”* (1 Petro 4:12 NIV).

        ***Mfano****:* Ikiwa hatuyaangalii maisha kutokana na mtazamo wa Mungu, kwa moyo wenye msimamo sahihi, tunaweza kukamatwa nje ya eneo salama pale tunapoteseka na kupitia masumbufu yenye maumivu na kujikuta tukijiuliza wenyewe swali kama aliloji-uliza Gideoni kwenye Waamuzi 6:13 (NKJV): *“Ee Bwana wangu, ikiwa Bwana yu pamoja nasi, mbona mambo haya yote yametupata? Yako wapi matendo yake ya ajabu...”*

    - Tazama mfuatano (mfululizo) ulioko kwenye Warumi 5:3-4 (LIV):

        - Matatizo na masumbufu.
        - Jifunze saburi.
        - Uthabiti wa tabia.
        - Mtegemee Mungu.

- Tumaini na imani imara na thabiti, inayokomaa (pevuka)

***Ukurasa 26:***

- Tazama mfuatano (mfululizo) ulio katika Yakobo 1:2-4 (NLT):
    - Tatizo linatokea.
    - Imani inajaribiwa.
    - Saburi inakua.
    - Imara katika tabia (Tabia inaimarika).
    - Tayari kwa lolote, ukomavu/kupevuka

***Kurasa 26-27:***

- Tazama katika Yakobo 1:13-14 (NLT) kwamba Mungu kamwe hamjaribu mtu.

***Muhtasari wa "Tahadhari….Tahadhari….Tahadhari" (Kurasa 25-27):***

**Mateso yanapaswa kutarajiwa katika maisha ya Mkristo**. Ni kawaida (1 Petro 4:12 NIV).

**Kutokana vifungu hivi** tunaona jinsi Mungu anavyoyatazama masumbufu, magumu, matatizo na nyakati za taabu katika maisha yetu. Anayaoona kama fursa kwa ajili ya ukuaji na ukomavu wa kiroho. Kama tuanataka kuwa na mafanikio katika maisha ya Kikrsito, ni lazima tuendeleze msimamo sahihi na kuyatazama mambo haya kulingana na mtazamo wa Mungu na siyo mtazamo wetu wenyewe.

***Kielelezo:*** Nilikuwa naendesha gari kuelekea juu mlimani nyuma ya lori, na linakwenda kwa takribani mwendo wa maili tano kwa saa, kwa hiyo niliamua kulipita. Nilipokuwa nalipita, nilifika juu ya kilele cha mlima nikagongana uso kwa uso na lori lingine lililokuwa linatokea upande mwingine. Tatizo langu lilikuwa wapi? Jibu ni kwamba nilikosa uvumilivu na mtazamo. Katika mtazamo wangu ilionekana salama kupita, katika mtazamo wa Mungu angeweza kuona kwamba haikuwa salama. Kama ningekuwa

nimemuuliza Yeye nini cha kufanya na kusubiri kutoka kwake kuniambia, ningeweza kuwa salama. Siku zote jaribu kuangalia mambo katika nyakati za tabu, masumbufu, na majaribu mazito katika mtazamo wa Mungu. Katika mtazamo wake, Mungu anasema kwamba hayo ni mazuri kwetu. Kwa hiyo kubali kwa imani kile Mungu anachosema kwa sababu Mungu hawezi kusema uongo.

***Kibainishi:*** Geuza kitabu chini juu juu ya meza au kishike mkononi ili kwamba kisimame wima na kuonekana kama pembetatu au mlima. Sasa vuta taswira ya kitabu kama mlima na fikiria kwamba ulikuwa unaendesha gari upande mmoja wa mlima, pasipo kuwa na uwezo wa kuona nini kilicho upande mwingine. Vuta taswira Mungu akiwa juu ya mlima akiangalia chini na anaona pande zote mbili za mlima. Ni yupi aliye na mtazamo mzuri—sisi au Mungu?

- Jambo moja nzuri ambalo linatokea kutokana na baadhi ya uzoefu unaochanganya katika maisha yetu ni kwamba uzoefu ule umetupeleka karibu zaidi mikononi mwa Yesu, Bwana na Mwokozi wetu anayetupenda.

- Kifungu hiki tulichokisoma hivi punde katika sehemu hii kinatuonyesha kwamba kuna mfuatano (mfululizo) unaohusika katika kufikia ukomavu wetu kiroho. **Hakuna tumaini la kufikia lengo la ukomavu wa kiroho bila kupitia masumbufu, shida, nyakati za taabu na majaribu mazito—na kujifunza jinsi ya kuitikia vizuri (kwa usahihi)**.

- Ni lazima tujifunze *"kustahimili magumu ..... kama askari wazuri wa Kristo Yesu"* (2 Timotheo 2:3 NIV).

- Ikiwa tutaweka lengo letu kwa Yesu na kumwamini, udhaifu wetu unaweza kuwa nguvu zetu—*"Neema yangu yakutosha; maana uweza wangu hutimilika katika udhaifu."* (2 Wakorintho 12:9 NKJV). Mara nyingi katika maisha ya Kikristo, pale mtu anapokuwa ametembea na Mungu kwa miaka mingi, tunaona nguvu ndani ya maisha ya mtu huyo. Hata hivyo, kadri anavyoachilia udhibiti wa maisha yake kwa Mungu kila siku na kuishi

chini ya udhibiti wa Mungu, Mungu anabadilisha nguvu zake kwa udhaifu wake.

- Wakati mwingine tunaweza kushangaa kwa nini uvumilivu unaonekana kuwa jambo kubwa kiasi hicho kwa Mungu. Je, inawezekana kwamba ni wa muhimu kwa sababu kadri tunavyomsubiri Mungu kwa saburi, Yeye na wengine wanauona ujasiri wetu katika Yeye na imani yetu katika utendaji?

- Ni vigumu kwetu sisi kuelewa jinsi gani Yesu alivyojifunza kitu chochote kwa sababu kama Mungu alijua kila kitu, lakini kama mwanadamu, *"Alijifunza kutii kutokana na mateso aliyoyapata"* (Waebrania 5:8 NIV). Kwa hiyo, tunajua kwamba mateso yanaweza kutusaidia kujifunza kuwa na utii kwa Mungu.

- Kamwe Mungu hamjaribu mtu yeyote.

- Majaribu siyo dhambi, lakini kujiachilia katika jaribu ni dhambi.

***Ni lazima tujifunze kuona mambo kama Mungu anavyoyaona (kuyatazama maisha katika mtazamo wa Mungu), tunapaswa kuelewa kwamba Mungu anajua kila kitu. Katika mtazamo wa Mungu tunaona kwamba:***

**Shetani ANATUJARIBU sisi ili kutuharibu**. Hii ni njia ya Shetani ya kurudi tena kwa Mungu. Si kwamba anakuja kutuumiza, anakuja kutuharibu/kutuangamiza.

**Mungu anaruhusu MAJARIBU katika maisha yetu kutufanya tuwe na nguvu**. Mungu anataka kutujengea tabia ya kiungu ndani yetu ili kwamba tuwe wakomavu kiroho, wenye nguvu na imara katika tumaini na imani.

**Mungu anaruhusu TUJARIBIWE ili kutuonyesha jinsi gani tunapimwa katika viwango vyake**. Je ni kiwango gani ambacho Wakristo wanapima maendeleo yao katika kukomaa kiroho? Neno la Mungu katika maandishi ni Biblia, na katika mwili ni Yesu. Vyote ni Neno la Mungu na ndicho kiwango pekee ambacho tunayapima maisha yetu. Kwa hiyo, pale ninapojaribiwa, ninaweza kuona jinsi ninavyoendelea kwa kuona ama mawazo yangu, msimamo, na matendo yangu yako katika utii katika kanuni zilizofundishwa katika Neno la

Mungu, Biblia, au kama ninafuata mfano wa Yesu aliotupatia pale alipoishi hapa duniani, akituachia sisi kielelezo kwa ajili ya kuishi maisha ya Kikristo.

***Vielelezo vitatu kutuonyesha jinsi gani Mungu anatumia nyakati za taabu, masumbufu na majaribu mazito katika maisha yetu kwa faida yetu:***

1. ***Uzoefu Unaoshindana***—marashi fulani yametengenezwa kwa kusaga petali za waridi. Petali zinaposagwa, harufu nzuri inatokea.

    ***Utekelezaji***—Pale Mkristo anapopitia uzoefu unaoshindana lakini anakaza macho yake kwa Yesu na kuendelea kumwamini Mungu, harufu nzuri inazalishwa ambayo hupanda juu ili kumbariki Mungu na kutoka nje kumbariki mwanadamu (2 Wakorintho 2:14-16).

    - Mara nyingi tunafikiri kwamba hatutaweza kusimama wakati mwingine wa uzoefu huu wa ushindani, lakini kumbuka: *"Mateso ya mwenye haki ni mengi, lakini Bwana humponya [sisi] nayo yote"* (Zaburi 4:19 NKJV).

    - Katika mtazamo wa Mungu, anaona uzoefu huu wenye ushindani kama fursa kwa ajili yetu ili kukua kiroho na kuleta utukufu Kwake.

    - Kumbuka kwamba kupitia uzoefu wenye ushindani:

        - Kusudi la Shetani ni kutuharibu sisi.

        - Kusudi la Mungu katika kuyaruhusu ni kutuleta katika ukomavu ili kwamba tuweze kuleta utukufu Kwake.

2. ***Uzoefu unaotokana na Mikandamizo***—Almasi inaanza kama kipande cha mkaa, lakini baada ya kuwekwa kwenye mkandamizo mkubwa kwa miaka, inageuka kuwa almasi nzuri.

    ***Utekelezaji***—Mara nyingi mgandamizo katika maisha yetu ni mkubwa kiasi kwamba tunashangaa kama tutaweza kusimama tena, lakini kum-

buka: *"Katika mambo yote Mungu hutenda kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema, yaani, wale walioitwa kwa kusudi lake"* (Warumi 8:28 NIV). Kwa hiyo, hakuna kinachoweza kugusa maisha yetu isipokuwa Mungu amekiruhusu, na pale anaporuhusu sisi kuwa katika mgandamizo, anatazama kutlingana na mtazamo Wake kama njia kwa ajili ya hilo kufanya kazi kwa faida yetu na utukufu Wake.

    - Tunajua kwamba Yesu ni *"... nuru ya ulimwengu"* (Yohana 9:5) na kwamba almasi inaakisi mwanga katika pande zote. Kwa hiyo, kwa kuruhusu hali ya migandamizo, Mungu anatupatia fursa ya kubadilishwa katika mfano wake. Kisha, kama ilivyo almasi, tunaweza kumuakisi Yeye kwa kila mtu ambaye tunamkaribia.

- Kumbuka kwamba kupitia uzoefu wenye migandamizo:

    - Kusudi la Shetani ni kutuharibu/kutuangamiza sisi.

    - Kusudi la Mungu katika kuruhusu migandamizo ni kutuleta kwenye ukomavu ili kwamba tuweze kumletea utukufu Yeye.

3. ***"Uzoefu wa Kupita kwenye Moto"***—Fedha halisi ni matokeo ya fedha iliyopitishwa kwenye moto mkali na kuyeyushwa, na kisha taka za juu ya chuma, uchafu, vinaondolewa.

    ***Utekelezaji***—Dhambi katika maisha yetu ni kama takataka zilizo ndani ya fedha. Kwa hiyo, Mungu anaruhusu sisi kupitia uzoefu tunaoweza kuuelezea kama "Kupita kwenye moto" ili kutufanya tuzione dhambi zetu, takataka, ambazo ni dhambi tunazopaswa kuzitubia na kuziacha.

    ***Moto Unaosafisha***
    —Mwandishi Hafahamiki

    Hapo zamani kidogo, wanawake kadhaa walikutana kwenye jiji fulani ili kusoma maandiko na kuwafanya wawe gumzo la

maongezi. Walipokuwa wakisoma sura ya tatu ya Malaki, walikutana na maelezo yenye mguso kwenye mstari wa tatu: *"Naye ataketi kama mtu asafishaye na atakasaye fedha."*

Maoni ya mwanamke mmoja yalikuwa kwamba yalikusudiwa kuwasilisha maoni ya ushawishi wa utakaso wa neema ya Kristo. Kisha alipendekeza kumtembelea mfua fehda na kutoa taarifa kwenye kikundi kile alichokisema juu ya somo hili. Alikwenda kama alivyoahidi, na bila kumwambia malengo ya ujio wake, alimuomba kujua mchakato wa kusafisha fedha, ambapo alimwelezea kwa ufasaha.

"Lakini Ndugu," alisema, "unakaa tu wakati kazi ya kusafisha inaendelea?"

"Aa ndiyo, mama," alijibu mfua fedha. Ni lazima nikae macho yangu yakiwa yameelekezwa makini kwenye tanuru, kwani ikiwa muda unaotakiwa kwa ajili ya usafishaji ukizidi hata kwa kiwango kidogo, fedha itaharibika**."**

Mwanamke yule mara moja aliona uzuri, na faraja pia, ya maelezo haya, "*Naye ataketi kama mtu asafishaye na atakasaye fedha."* Kristo analiona hilo ni hitaji kuwaweka watoto wake kwenye tanuru, macho yake akiyaelekeza kwenye kazi ya usafishaji/ utakasaji, na hekima na upendo wake, vyote vinahusika katika kiwango kilicho bora kwa ajili yake. Majaribu yao hayaji bila mpangilio, kwa maana, *"hata nywele za vichwa vyenu zimehesabiwa"* (Mathayo 10:30).

Wakati yule mwanamke anaondoka dukani, mfua fedha alimwita arudi na kusema bado ana mengi ya kumwambia. **Yeye alijua tu pale mchakato wa kusafisha unapokamilika kwa kuona taswira yake mwenyewe ikiakisiwa kwenye fedha**. Ni mfano mzuri kiasi gani! Wakati Kristo atakapoiona tas-

wira Yake ndani ya watu Wake, kazi Yake ya kutakasa itakuwa imekamilika.

- Tuna *"... jaribiwa.... Katika tanuru ya mateso"* kwa ajili yake (Isaya 48:10-11 NIV). Kama "*Tutayaelekeza macho yetu kwa Yesu"* (Waebrania 12:2 NIV) wakati tunapopita kwenye moto, tutakua, *"tukiendelea kubadilishwa (katika roho) katika mfano wake..."* (Wafilipi 3:10 AMP).

- Kumbuka kwamba pale tunapopitia uzoefu wa "kupita kwenye moto:

  - Kusudi la Shetani ni kutuharibu sisi.
  - Kusudi la Mungu katika kuyaruhusu ni kutuleta katika ukomavu ili kwamba tuweze kumletea utukufu Yeye.

***Kumbuka***—Mungu siyo tu anataka kutupa fursa ili kukomaa kupitia masumbufu na nyakati za kujaribiwa kwetu, lakini anatupenda na anataka kuuonyesha upendo wake kwetu. Pale **akili** yetu **inapofikia mwisho** na kulia kwake kwa imani, atakutana nasi pale **akili yetu inapoishia**, atatuliza dhoruba, na kutuongoza.

> *Wapanda mbinguni, watelemka vilindini, Nafsi yao yayeyuka kwa hali mbaya. Wayumba yumba, wapepesuka kama mlevi na* ***akili zao zote*** *zawapotea. Wakamlilia Bwana katika dhiki zao, akawaponya na shida zao. Huituliza dhoruba,ikawa shwari, mawimbi yake yakanyamaza. Ndipo walipofurahi kwa kuwa yametulia naye huwaleta mpaka bandari waliyoitamani. Na wamshukuru Bwana kwa fadhili zake, na maajabu yake kwa wanadamu"* (Zaburi 107:26-31 NKJV)

***Matokeo waliyoyatamani***—Hebu turuhusu majaribu, masumbufu, na vipindi vya kujaribiwa na yote mengine magumu ya maisha ambayo *hukupeleka wewe kwenye kina mikononi mwa Mungu*. Anakupenda, na ni mwaminifu.

11. Kuchunguza **Mpango wa Kushika Maandiko** (Ukurasa 236).

    ***Marudio:*** Kama tunaufanyia kazi mpango, mpango utafanya kazi.

    - Kushika mstari kunauingiza kwenye akili zetu. Kutafakari juu ya mstari kunauingiza kwenye mioyo yetu, na mara unapokuwa mioyoni mwetu, tunaweza kulitekeleza hilo katika maisha yetu.

12. Marudio ya **Mlolongo wa ya Mistari Iliyoshikwa** (Ukurasa 238).

    - Baada ya wanafunzi kuwa wameshika mstari na kuunukuu rejea, mstari, rejea mara 30, watake kuandika tarehe kwenye ukurasa 238, katika safu ya "Tarehe Uliposhikwa.

13. Watake wanafunzi kuweka mistari ifuatayo kwenye kadi (Ukurasa 235):

    - **1 Petro 5:7**
    - **Wafilipi 4:19**

    ***Marudio:***

    - Fungua kwenye mfuko wa ndani nyuma ya kijitabu kidogo cha mwanafunzi, na chukua kadi moja iliyo wazi ya mstari kwa ajili ya kila mstari utakaoushika juma hili.
    - Mara unapokuwa umeushika mstari, na kunukuu rejea, mstari, rejea mara 30, weka tarehe uliyoushika upande huo huo wa kadi kama andiko la rejea.

    *Kushika na kutafakari katika maandiko kunatusaidia kumjua Mungu.*

14. 1Jadili **Changamoto za Kusoma Biblia Kila Siku mwezi wa tatu** (Ukurasa 50). Wahamasishe wanafunzi kuanza changamoto hizi kesho asubuhi.

    ***Maelezo:***

    - Hii ni nyenzo tunayowahamasisha wanafunzi kuitumia ili kusoma Biblia yote mara moja kwa mwaka kwa kipindi chote cha maisha yao yote kilichobakia.

*Kujiwekea nadhiri wenyewe ya kusoma Neno la Mungu lote mara moja kwa mwaka na kutafakari kile tunachosoma hutusaidia sisi kumjua Mungu.*

15. Wahamasishe wanafunzi kuonyesha upendo wao kwa Mungu mara tatu kila saa wanapokuwa macho kila juma: *"Nakupenda, Ee Bwana, nguvu zangu"* (Zaburi 18:1 NIV).

    ***Maelezo:***

    - Pale tunaposema, "Bwana, nakupenda" tunaomba maombi ya kumwabudu Mungu.
    - Tunataka kuchochea jinsi tunavyoonyesha upendo wetu kwa Mungu wakati wote wa siku kila siku. Mazoea haya ni ya muhimu kwa ajili ya kanuni za kibiblia zinazobadilisha maisha tutakayojifunza katika vipindi vya juma linalofuata.

16. Wahamasishe wanafunzi kutafuta fursa za kushirikisha kile Mungu anachowafundisha.

    ***Maelezo:*** Tunataka kuwasaidia wanafunzi kuwa na utulivu katika kuongea juu ya Yesu katika maeneo yote ya maisha yao.

17. Tafuta umakini wa wanafunzi kwa ajili ya **Kazi** zao **za Ziada** (Kurasa 257-258).

    ***Soma darasani:*** Toa muda wa kusoma ukurasa 257 kwa sauti darasani na kuhakikisha kwamba kila mmoja anaielewa kazi ya ziada.

    - ***Wahamasishe kuwa waaminifu kwa Mungu na kukutana Naye kila siku katika wakati wao wa utulivu.***

18. Funga kwa Maombi.

    ***Mfano:*** Waalike wanafunzi kuungana nawe kupiga magoti mnapoomba pamoja na kumshukuru Mungu kwa kukutana na wewe na kipekee kwa kuzungumza na kila mmoja wenu.

## Mwongozo wa Kiongozi na Ujumbe wa Mwandishi......................Kipindi cha 10

1. Anza kwa maombi.

   ***Mfano:*** Waalike wanafunzi kupiga magoti pamoja nawe mnapoomba pamoja na kuukabidhi muda kwa Mungu.

2. Mtake kila mmoja kufungua katika karatasi ya **Ufuatiliaji** ambayo inahitajika siku hiyo. Kisha unaweza **kuzikagua na kuzisaini** (Ukurasa 281).

   ***Uwajibikaji:*** Ukaguzi na uwekaji sahihi karatasi zao za Ufuatiliaji kila juma huwafundisha wanafunzi katika kanuni ya uwajibikaji iliyofundishwa katika Warumi 14:12.

3. Soma **"Kwa kuwa Kusudi langu la dhati ni kwamba Nimjue Yeye"** (Ukurasa 9). Mtake mtu mmoja kushirikisha **K**uvuta taswira kwake sehemu moja ya mstari huu na kumsikiliza pale anaporudisha Maombi yake kwa Mungu kama ombi lake binafsi. **Wakumbushe wanafunzi kuweka mwelekeo wao kwa Yesu** (Waebrania 12:2).

   ***Kumbusho:*** Tunahakiki Wafilipi 3:10 (AMP) kila juma kwa sababu kuu tatu:

   1. **Ili kuyafanya macho yetu yamwelekee Yesu** na Yesu pekee yake na kutukumbusha kwamba **kusudi letu la dhati ni kumjua Yeye.**
   2. Ili kutukumbusha kwamba **kanuni kama zilivyo siyo mwisho wa mambo. Hizo ni njia tu ambazo Mungu ametupatia ili kumjua Yesu** kwa kina, kwa undani, na kibinafsi.
   3. **Ili kutafakari juu ya kweli zenye nguvu** katika mstari huu ili kwamba ziweze kuhama kutoka kwenye ukurasa kwenda kichwani na kisha kwenda mioyoni mwetu **ili kwamba tuweze kubadilishwa katika mfano wa Yesu**.

4. Mwombe mtu mmoja kushirikisha, kisha **K**ufikiria kwa kina, **K**uvuta taswira na **K**uombea tena kwa Mungu **Notsi za Mahubiri au Somo lake** (Kurasa 21-24).

***Marudio:***

- Tunapaswa kuhudhuria ibada za kuabudu tukitarajia Mungu kuzungumza nasi. Pale anapozungumza nasi, tunapaswa kuwa tayari kuandika kile anachosema. Mara tunapokiandika, basi tunaweza kuzitunza notsi mpaka tunapopata fursa ya kutafakari kweli hizo. Pale tunapotafakari (**K**ufikiria kwa kina, **K**uvuta taswira, na **K**uziombea kweli hizo tena kwa Mungu kama maombi), tunaihamisha kweli kutoka vichwani mwetu kwenda mioyoni mwetu ambako inaweza kufanya kazi kwa namna yake katika utekelezaji.

*Pale tunapotulia ili kutafakari juu ya ujumbe tulioutengeneza wakati tunamsikiliza Mungu anaposema nasi katika mahubiri, inatusaidia kumjua Yeye.*

5. Jadili **Maswali ya Marudio ya Kazi za Ziada** (Ukurasa 258).

***Maelezo:***

- Tumia swali la 5 katika ukurasa 258 kuwahamasisha wanafunzi kuzungumza kwa wengine habari za Yesu na mambo ambayo Anawafundisha .

    - Mruhusu mmoja wao katika kundi kusimulia kuhusu uzoefu unaotokana na juma lililopita wakati alipozungumza na mtu fulani kuhusu Yesu au kushirikisha kitu chochote ambacho Mungu amemfundisha.

6. Uliza kama kurasa za **Tahadhari….Tahadhari…. Tahadhari** (Kurasa 25-27) ziliwasaidia. Kwa nini?

***Muhtasari wa Tahadhari….Tahadhari….Tahadhari:***

- Mateso yanapaswa kutarajiwa katika maisha ya Ukristo. Ni ya kawaida (1 Petro 4:12 NIV).

    - ***Nukuu***—Wakati akiwa kwenye miaka 70 hivi, Rev. Don J. Milam aliulizwa, "Ikiwa ungepata fursa ya kuishi tena, ungemwomba Mungu akupe nini?" Alijibu,

        > Ningemwomba Mungu ***anizidishie matatizo mara mbili zaidi*** kwa sababu ilikuwa ni kupitia uzoefu wa maisha ya mambo magumu *ndipo nilisukumwa kwenye kina mikononi mwa Mun-*

*gu*. Ilikuwa ni katika nyakati hizo ndipo nilipogundua kwamba

- Mungu pekee yake ndiye anatosha kwa ajili ya mahitaji yangu yote.
- Hakuna kinachoweza kunitenga na upendo wa Mungu.
- Hakuna kinachoweza kuniondoa mikononi Mwake.
- Msalaba unakuja kwanza na kisha taji.
- Inatangulia kwanza bustani na kisha utukufu wa Pentekoste.
- Kunatangulia kwanza kuugua na vilio na kisha furaha kuu.

Wakati wengine wanaishi kwa mifumo ya milango mitano ya fahamu—nini wanaona, kugusa, kusikia, kuonja na kunusa—sisi tunaishi kwa imani. Na jaribu la imani ni la thamani zaidi kuliko dhahabu iliyojaribiwa motoni kwa sababu ya jinsi Mungu anavyojifunua Mwenyewe kwetu kupitia uzoefu huo.

Ni kwa imani, iliyojaribiwa kwa moto, ndipo tunakuwa na ujasiri kiasi hicho katika Mungu kwamba wakati anaongea nasi kupitia Biblia, tunaamini na kuifanyia kazi.

- Kutokana na vifungu hivi tunaona jinsi Mungu anavyoyaangalia masumbufu, magumu, matatizo, na nyakati za taabu katika maisha yetu. Anayaona kama fursa kwa ajili ya ukuaji wa kiroho na kwa ajili ya ukomavu wetu. Na kama tunataka kufanikiwa katika maisha ya Kikristo, tunapaswa kuendeleza msimamo mzuri na kuyatazama mambo haya katika mtazamo wa Mungu na siyo mtazamo wetu wenyewe.
- Vifungu ambavyo tumevisoma hivi punde katika sehemu hii vinatuonyesha kwamba kuna mfuatano (mfululizo) unaohusika katika kuufikia ukomavu wa kiroho. Hakuna tumaini la kufikia lengo la ukomavu wa kiroho nje ya kupitia masumbufum magumu, nyakati za taabu na nyakati za kujaribiwa na kujifunza jinsi ya kuitikia kwa usahihi.

- Ni lazima tujifunze *"kustamili taabu..... kama askari mzuri wa Kristo Yesu"* (2 Timotheo 2:3 NIV).
- Ikiwa tunaelekeza lengo au mwelekeo wetu kwa Yesu na kumwamini Yeye, udhaifu wetu unaweza kuwa nguvu zetu—*"Neema yangu ya kutosha: maana nguvu zangu zinakamilishwa katika udhaifu....."* (2 Wakorintho 12:9 NKJV). Mara nyingi maisha ya Mkristo, pale anapotembea na Mungu kwa miaka mingi, tunaona nguvu na hatutambui kwamba huko nyuma nguvu hizi zingeweza kuwa udhaifu. Hata hivyo, kadri anavyoachia udhibiti wa maisha yake kwa Mungu kila siku na kuishi chini ya udhibiti wa Mungu hubadili nguvu Zake kwa udhaifu huo.
- Wakati mwingine tunaweza kushangaa kwa nini uvumilivu unaonekana kuwa kama jambo kubwa kwa Mungu. Inawezekana kwamba ni wa muhimu kwa sababu kadri tunavyomsubiri Mungu kwa saburi, Yeye na wengine huona ujasiri wetu Kwake na imani yetu katika matendo?
- Ni vigumu kwetu kuelewa jinsi Yesu alivyojifunza kila kitu kwa sabu kama Mungu alijua kila kitu, lakini kama mwanadamu, *"Alijifunza utii kutokana na kuteseka kwake"* (Waebrania 5:8 NIV). Kwa hiyo, tunajua kwamba mateso yanaweza kutusaidia kujifunza kuwa na utii kwa Mungu.
- Kamwe Mungu hamjaribu mtu.
- Majaribu siyo dhambi, bali kujiachilia katika majaribu ni dhambi.

7. Soma/jadili kwa kina mafunzo ya **Kuyajaza Maisha Yangu kwa Upendo** (Kurasa 148-154). Unaposoma na kujadili, mara kwa mara, tulia ili kutoa fursa kwa wanafunzi **K**ufikiria kwa kina, **K**uvuta taswira, na **K**uomba**.**

***Ukurasa 148:***

- Tambua kwamba **Yesu Kristo ni kitovu** cha gurudumu hili, ambalo linawalikisha maisha yetu binafsi. Yesu anatakiwa kuwa kitovu cha maisha yetu ambaye katika yeye kila kitu katika maisha yetu kinahusika. Pale hili linapokuwa dhahiri maishani mwetu, upendo wetu kwa Mungu unaongezeka katika maombi, nje kwa waamini wenzetu katika ushirika, na nje kwa waliopotea kupitia ushuhudiaji.

***Ukurasa 149:***

- Tambua sentensi ya kwanza ya para ya kwanza katika ukurasa huu: "Kwa uchaguzi wangu wa hiyari namruhusu Roho Mtakatifu kuzalisha ndani yangu kitu fulani ambacho hakiwezi kuzalishwa katika namna yake ya kawaida isipokuwa kwa Roho Mtakatifu, na hilo ni upendo."

    - **"Kwa uchaguzi wangu wa hiyari" katika para hii inamaanisha kwamba kwa tendo la hiyari yako, ni lazima uchague ama kumruhusu au kutomruhusu Roho Mtakatifu kuzalisha upendo wa kweli ndani yako**. Hili linaweza kutokea pale unapoishi chini ya udhibiti wa Mungu. Kwa hiyo, kwa tendo la hiyari yako ni lazima uchague kila siku kuachilia udhibiti wa maisha yako kwa Mungu na kumruhusu kuwa msimamizi wa maisha yako kwa siku hiyo. Kisha upendo wake wa kweli unaweza kuzalishwa na kuakisiwa kupitia wewe.

## **Kwa nini ninapaswa kuyajaza maisha yangu katika upendo kwa Mungu?** (Ukurasa 149, Sehemu II. A-Ukurasa 154)

***Ukurasa 152:*** Yesu akasema, akawambia, "*Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote na kwa akili zako zote"* (Mathayo 22:37 NKJV).

- Jinsi gani utaonyesha kumpenda Mungu kwa moyo wako wote? Kuna njia nyingi za kuonyesha upendo huu wa dhati kwa Mungu, na mara nyingi inakuwa dhahiri katika utoaji wa kujidhabihu.

    ***Hadithi #1:*** Sisi wenyewe tumeshuhudia utoaji wa kujidhabihu katika kanisa letu. Wakati tulipopoteza karibu kila kitu cha jengo la kanisa letu kwa moto, Mungu alifanya katika mioyo ya watu wakajitoa kwa kujidhabihu ili kulijenga upya.

    ***Hadithi #2:*** Huko Romania, tuliona moja ya mifano yenye kugusa ya kumpenda Mungu kwa moyo wote. Jumapili moja asubuhi yenye mvua, mchungaji na karibu watu sitini walikusanyika ili kuabudu na kutoa matoleo waliyokuwa wakiyaombea kwa takribani majuma kadhaa. Walikuwa wakijaribu kujenga jengo la kanisa katika eneo na ulikuwa ni wakati kwa wazazi kununua

kalamu na madaftari kwa ajili ya watoto wao kuanza shule. Katika kusanyiko ambalo hakuna watu matajiri, walitoa takribani $3,000 taslimu, pete nne za harusi, jozi moja ya darubini ya kuona mbali na gari moja. Gari hilo la miaka miwili lilitolewa na mchungaji na mke wake. Tulishuhudia watu wakitoa kupita uwezo wao ambao wangeweza kufikia katika muda wa majaribu makubwa na umaskini wa kupita kawaida.

8. Ruhusu kundi kujigawa katika jozi (wavulana kwa wavulana na wasichana kwa wasichana). Mtake kila mmoja kushirikisha kisha **KKK yafuatayo wakati mshirika wake akimsikiliza**:

   a. **Mistari ya kushika** juma hili.
      - 1 Petro 5:7
      - Wafilipi 4:19

   b. **Notsi za kila siku katika Kusoma Biblia (NK-SKB)** (Kurasa 65-72) zilizotengenezwa juma hili lililopita.

   - Tunaligawa kundi katika jozi ili kwamba kila mmoja aweze kuwa na nafasi ya kushirikisha notsi moja au mbili za UBKS na mistari iliyokaririwa katika juma lililopita na kisha **K**ufikiria kwa kina, **K**uvuta taswira, na **K**uombea mistari na notsi za UBKS tena kwa Mungu kama maombi binafsi.
   - Hamasisha wanafunzi kuwa mawakili wema wa hili na siyo kuzungumza juu ya kitu kingine chochote. Huu ni wakati wa kufanyia mazoezi na kukua katika nidhamu au kanuni ya kutafakari

.

9. Warudishe wanafunzi kwenye kundi kubwa na watake waweke mistari ifuatayo kwenye kadi za maandiko (Ukurasa 235):

   - **Mithali 3:5-6**
   - **1 Yohana 1:9**

   ***Marudio:***

   - Geuza mfuko kwa ndani nyuma ya kijitabu kidogo, na chukua kadi moja ya mistari iliyo wazi kwa kila mstari ambao utakuwa unaushika juma hili.

***Muhimu:***

- Ni muhimu sana kuandika mistari hii kwenye kadi darasani. Wanafunzia wanaweza kuzichukua juma nzima na kuzitumia wakati wanasubiri, wanapokuwa kwenye mapumziko, n.k. ili kuishika mistari. Kama hawafanyi hilo darasani, Shetani ataweka vikwazo vingi mbele ya wanafunzi na kulifanya hilo kupata mstari wa kukariri kuwa gumu kabla hamjakutana nao tena.
- Kumbuka kwamba kushika mstari huuingiza kwenye akili zetu. Kutafakari huuhamisha kwenda mioyoni mwetu. Kwa hiyo, tunaishika mistari hii mwanzoni mwa juma, mapema kadri iwezekanavyo ili kwamba tuweze kuwa na kitu zaidi cha kutafakari kwa juma kabla hatujakuana tena. Kwa nini kutafakari maandiko? Tunataka Mungu kuitumia mistari katika maisha yetu kutubadilisha katika mfano Wake.

*Kushika na kutafakari maandiko kunatusaida kumjua Mungu.*

10. Soma/jadili na kutafakari (**KKK**) juu ya kweli katika **Kanuni ya Kutumbukiza na Kuondoa** (Kurasa 28-29). Wahamasishe wanafunzi kufanyia mazoezi kanuni hii kwa kuonyesha upendo wao kwa Mungu mara tatu kila saa wanayokuwa macho katika juma hili kwa kusema tu, “Bwana, kwa kweli ninakupenda” (Zaburi 18:1 NIV).

    ***Maelezo:*** Kwa watu wengi Kanuni ya Kutumbukiza na Kuondoa imekuwa ni elimumwendo (yenye nguvu), kanuni inayobadisha maisha ambayo imewasaidia kupata ushindi dhidi ya Shetanai katika vita dhiti ya mawazo, misimamo au mitazamo na matendo.

    - Sisitiza **tafsiri ya kanuni** iliyo juu kwenye ukurasa wa 28—**Kanuni ni kweli iliyotolewa na Mungu ambayo inakuwa msingi au sababu inayoinua msimamo wa imani na matendo**.
        - **Hii ni ya muhimu kwa sababu njia zinabadilika mara kwa mara, lakini kanuni kamwe haibadilika. Kanuni hizi, pale tunapozipata katika Neno la Mungu, zinapoasiliwa (kuchukuliwa) na kutumiwa katika maisha yetu zinatumika kwa Roho Mtakatifu kufanya upya mawazo, misimamo, na matendo yetu.**

- Moja ya faida ya maisha yetu kujengwa kwenye msingi wa kanuni za kibiblia ni kwamba kanuni hiyo hiyo inaweza kutumika katika mazingira mengi tofauti.

- Tunahitaji kuelewa kwamba kanuni hii ni ya kushambulia na siyo kujihami. Katika mchezo wowote, mtu binafsi, au timu mara chache inaweza kupata ushindi ikiwa mchezaji au wachezaji wakati wote wanacheza kwa kujihami.

  - **Mara nyingi sisi kama Wakristo tumeshindwa kwa sababu siku zote tunacheza kwa kujihami na mara chache au kamwe hatuchezi kwa kushambulia.**

    ***Mifano***: Mara nyingi tunasubiri mpaka Shetani ametushambulia ili kujaribu kuona jinsi gani tutaitikia. Shetani yupo kwenye kushambulia, na sisi moja kwa moja tunakuwa kwenye kujihami.

- ***Kanuni hii ya Kutumbukiza na Kuondoa*** inaweza kubadilisha ghafla jinsi tunavyoishi maisha yetu. Itatuonyes jinsi ya kuyaishi maisha yetu katika kushambulia na siyo kujihami.

  ***Hadithi***: Kwa miaka mingi, nilikuwa nikishindwa pale nilipokabiliwa na jaribu kwa sababu nilielekeza lengo au mwelekeo kwenye jaribu na nilimuomba Mungu kunisaidia nisijiachilie. Mwaka mmoja nilipokuwa nikisoma Biblia, Mungu alizungumza nami kupitia Wafilipi 4:8 na alinionyesha nilikuwa naangukia kwenye mtego wa Shetani. Nilikuwa nacheza kwa kujihami na kuitikia katika njia isiyo sahihi. Shetani asingeweza kufurahia zaidi.

  - Kabla jaribu hata halijaja, ninapaswa kuwa mtii kwa Bwana pale aliposema *"Fikiri juu ya mambo haya."*
    - Ni mambo gani ningepaswa kuwa nay-afikiria?
      - *"Mambo yoyote yaliyo ya **kweli**,"*
      - *"Mambo yoyote yaliyo ya **staha**,"*
      - *"Mambo yoyote yaliyo ya **haki**,"*

- *"Mambo yoyote yaliyo* ***safi,"***
- *"Mambo yoyote yaliyo ya* ***kupendeza,"***
- *"Mambo yoyote yaliyo na* ***sifa njema,"***
- *Mambo yenye* **wema au uadilifu***, na*
- ***Sifa***.

- Kwa nini ninapaswa kujizoeza katika kanuni hii *"kuyafikiri mambo hayo"*?

  - Kanuni hii, kama zilivyo kanuni zote "kutokana na Neno la Mungu, ni ya binafsi kutoka kwa Mungu kuja kwetu."

  - *"Maana kama mtu afikirivyo ndani ya moyo wake ndivyo alivyo…" (*Mithali 23:7 NKJV). Mstari huu unatufundisha kwamba **sisi ni matokeo ya kufikiri kwetu wenyewe**. Kwa hiyo, tunahitaji kufikiri juu ya vile tunavyotaka kuwa.

- Pale ninapotafakari mstari huu, ninatambua kwamba haya ni maelezo sahihi ya Yesu. Kuna watu na mambo yanayostahili sifa kwa sababu wakati mwingine yanaakisi baadhi ya sifa hizi, lakini hakuna sifa inayostahili kama Yesu, Neno lililo hai (Yohana 1:1). Yesu ndiye mfano halisi wa kweli na uaminifu. Yeye ndiye mfano wa kile kilicho haki, kile ambacho ni safi, kile ambacho kinapendeza, na kile ambacho ni taarifa nzuri. Yeye ndiye anayeuelezea wema au uaminifu na hakika anastahili sifa zetu na hakuna mwingine.

- Katika utendaji, jinsi gani kweli hii—"*fikiria au tafakari juu ya mambo haya"* kutoka Wafilipi 4:8 inafanya kitu cha tofauti katika maisha yetu?

  - Nilianza kuzijaza siku zangu kwa kuonyesha upendo kwa Mungu. Haya ni maombi ya kuabudu.

    - Kwa siku nzima, nilianza kuonyesha upendo wangu kwa Mungu kwa kusema tu, "Bwana, nakupenda kweli kweli" au Bwana, ninakupenda kwa sababu Wewe ni *mtakatifu* (au *mwenye haki,* au w*ewe ni kweli, upendo*, au *mwaminifu*)."

- Nilianza kuijaza siku yangu kwa kumshukuru Mungu kwa yote aliyonifanyia na anaendelea kufanya kwa ajili yangu na wengine.
- Nilianza kuijaza siku yangu kwa kumsifu Mungu kwa ajili ya rehema na neema Yake.
    - Mara nilipoanza kufanyia kazi mambo hayo katika maisha yangu, nilianza kuona kwamba:
        - Nilipata ufahamu zaidi juu ya upendo wangu kwa Mungu.
        - Nilikuwa na ufahamu zaidi wa uwepo wa Mungu.
        - Nilikuwa na ufahamu zaidi ya wema wa Mungu, rehema na neema katika maisha yangu.

***Maelezo:*** Wakati Mungu alipokuwa akisema nami kupitia Wafilipi 4:8, tulikuwa tukifanya kazi ya mkataba, kwa vigezo vya serikali, tukibadilisha bamba la saruji (zege) kwenye kiwanja chao cha ndege. Tulikuwa tukitumia kipande kikubwa cha kifaa ambacho kilifanya kazi kwa kanuni ya kupenyeza na kuhamisha. Ncha ya kipande cha kifaa hicho iliingia unene wa lile bamba la saruji na, kwa sababu hakukuwa na nafasi kwa ajili ya ncha na bamba kwa wakati mmoja, bamba liliondolewa pale ncha ilipopenya kwenye lile bamba (zege).

***Utekelezaji:*** Kwa kutumia kipande kidogo cha kifaa kulinipa muonekano wa taswira ya Mungu anavyotaka sisi tutumie kanuni kutoka Wafilipi 4:8 katika maisha yetu. **Ni lazima tudhibiti kile tunachokifikiria kwa kupenyeza na kujaza akili zetu kwa Neno la Mungu na kuonyesha upendo, shukrani, na sifa kwa Mungu, na kitu kingine chochote kitaondoka**.

***Kanuni ya Kutumbukiza na Kuondoa*** ni kanuni ya muhimu sana katika Neno la Mungu ambayo nitajaribu kuilezea kwa namna nyingine.

- Fikiria kwamba ninayo glasi iliyojaa maji machafu na ninapenyeza hiyo glasi iliyojaa maji

machafu kwa kuijaza vipande vya thamani vya almasi. Nimefanya nini? Nimeondoa maji machafu ndani ya glasi kwa kuweka kitu kingine cha thamani zaidi. Kwa namna hiyo hiyo, ninaondoa mawazo yasiyo ya kimungu yaliwekwa akilini mwangu na Shetani pale ninapokuwa mtii kwa Mungu na kuijaza akili yangu kwa kitu kingine cha thamani zaidi kama vile vitu alivyoniamuru mimi kuvifikiria katika Wafilipi 4:8.

- Wakati tunapofahamu kwamba tunajaribiwa, mara moja, tunapaswa kugeuka na kumwangalia Yesu (Waebrania 12:2). Cheza kama mshambuliaji. Tupenyeze na kujaza akili zetu kwa mawazo ya upendo, shukrani, na sifa kwa Mungu.

    - Ni kweli hatusubiri mpaka tumejaribiwa kuifanyia kazi kanuni hii. Tunaifanyia kazi kanuni hii wakati wote kila siku, na kisha pale jaribu linapokuja, tunakuwa washindi kwa sababu tunafuata mwitikio wa Mungu uliopangwa.

        - Pale tunapoifanyia kazi kanuni hii, tutaona kwamba mara baada ya kuwa tumejaribiwa, tunakuwa tumemwelekea Yesu na tunajihusisha kabisa katika kuonyesha upendo wetu, shukrani, na sifa Kwake hata tunalisahau jaribu.

- Shetani hawezi kuweka baadhi mawazo au msimamo mbaya ndani ya akili zetu kama akili zetu tayari zimejaa Neno la Mungu, upendo, shukrani na sifa kwa Mungu.

- Je kuna eneo ambalo mara kwa mara unajihisi kushindwa? Tumia kanuni hii na upate ushindi.

***Ahadi:*** Kanuni hii inakuja na ahadi kwa wale ambao wanaitumia, na ahadi ni kwamba *“Na Mungu wa amani atakuwa pamoja nanyi”* (Wafilipi 4:9).

- *“Utamlinda Yeye katika amani kamilifu, Yeye ambaye mawazo yake yametulia Kwako, Kwa sababu anakutumaini Wewe”* (Isaya 26:3 NKJV).

- Namna tunavyoziweka akili zetu kuwa au kukaa (kujifunza na kumshikilia) kwa Mungu ni *"kufikiri juu ya hayo."*

- Kama tunataka ushindi dhidi ya Shetani katika vita vya mawazo, misimamo au mitazamo, na matendo, ni lazima tuifanyie kazi kanuni hii.
- **Mtu yule anayeifanyia kazi kanuni hii anapokea vyote, USHINDI na AMANI**.

11. Wahamasishe wanafunzi kutafuta fursa ili kushirikisha kile ambacho Mungu anawafundisha.

    ***Maelezo:*** Tunataka kuwasaidia wanafunzi kuwa na utulivu pale wanapozungumza habari za Yesu katika kila eneo la maisha yao.

12. Tafuta umakini wa wanafunzi katika **Kazi** zao **za Ziada** (Kurasa 259-260).

    ***Soma darasani:*** Toa muda wa kusoma Ukurasa 259 kwa sauti darasani, na hakikisha kwamba kila mmoja anaielewa kazi ya ziada.

    ***Wahamasishe wanafunzi wako*** kukutana na Mungu alfajiri na mapema kwa ajili ya muda wao wa utulivu.

    > ***...Ee Mungu, Mungu wangu; Nitakutafuta kwa bidii asubuhi na mapema...*** (Zaburi 63:1). (*Strong's Exhaustive Concordance of the Bible*, "Hebrew and Chaldee Dictionary," Ukurasa 114, namba 7836)

13. Funga kwa maombi.

    ***Mfano:*** Waalike wanafunzi kuungana nawe kupiga magoti mnapoomba pamoja na kumshukuru Mungu kwa ajili ya kukutana nanyi na kipekee kuzungumza na kila mmoja wenu.

## Mwongozo wa Kiongozi na Ujumbe wa Mwandishi...................... Kipindi cha 11

1. Anza kwa maombi.

    ***Mfano:*** Waalike wanafunzi kupiga magoti pamoja nawe mnapoomba pamoja na kuukabidhi muda kwa Mungu.

2. Mtake kila mmoja kufungua katika karatasi ya **Ufuatiliaji** ambayo inahitajika siku hiyo. Kisha unaweza **kuzikagua na kuzisaini** (Ukurasa 282).

    ***Uwajibikaji:*** Ukaguzi na uwekaji sahihi karatasi zao za Ufuatiliaji kila juma huwafundisha wanafunzi katika kanuni ya uwajibikaji iliyofundishwa katika Warumi 14:12. Pia inakusaidia wewe kama kiongozi kuona kama wanafunzi wako:

    - Wanafanya kazi za ziada na kujijengea mtindo wa maisha au
    - Wanahitaji kuhamasishwa au kutiwa moyo na wewe.

3. Soma **"Kwa kuwa Kusudi langu la dhati ni kwamba Nimjue Yeye"** (Ukurasa 9). Mtake mtu mmoja kushirikisha Kuvuta taswira kwake sehemu moja ya mstari huu na kusikiliza pale anaporudisha Maombi yake kwa Mungu kama ombi lake binafsi. **Wakumbushe wanafunzi kuweka mwelekeo wao kwa Yesu** (Waebrania 12:2).

    ***Kumbusho:*** Tunahakiki Wafilipi 3:10 (AMP) kila juma kwa sababu kuu tatu:

    1. **Ili kuyafanya macho yetu yamwelekee Yesu** na Yesu pekee yake na kutukumbusha kwamba **kusudi letu la dhati ni kumjua Yeye.**
    2. Ili kutukumbusha kwamba **kanuni kama zilivyo siyo mwisho wa mambo. Hizo ni njia tu ambazo Mungu ametupatia ili kumjua Yesu** kwa kina, kwa undani, na kibinafsi.
    3. **Ili kutafakari juu ya kweli zenye nguvu** katika mstari huu ili kwamba ziweze kuhama kutoka kwenye ukurasa kwenda kichwani na kisha kwenda mioyoni mwetu **ili kwamba tuweze kubadilishwa katika mfano wa Yesu**.

4. Mwombe mtu mmoja kushirikisha kisha **K**ufikiria kwa kina, **K**uvuta taswira kwake na **K**uombea tena kwa Mungu **Notsi za Mahubiri au Somo lake** (Kurasa 21-24).

    *Tunaposimama ili kutafakari notsi tulizoziandika wakati tunamsikiliza Mungu anapozungumza nasi katika mahubiri, inatusaidia kumjua Mungu.*

5. Jadili **Maswali ya Marudio ya Kazi za Ziada** (Ukurasa 260).

    ***Maelezo:***

    - Tumia swali la 6 katika ukurasa 260 kuwahamasisha wanafunzi kuzungumza kwa wengine habari za Yesu na mambo ambayo Anawafundisha.
        - Mruhusu mmoja wao katika kundi kusimulia juu ya uzoefu unaotokana na somo la juma lililopita wakati alipozungumza na mtu yeyote habari za Yesu au kushirikisha kitu chochote ambacho Mungu amemfundisha.

6. Soma/Jadili kwa kina mafunzo ya **Kuyajaza Maisha Yangu katika Upendo** (Kurasa 155-164). Unaposoma na kujadili, mara kwa mara tulia kidogo na kuwapa wanafunzi fursa ya **K**ufikiria kwa kina, **K**uvuta taswira na **K**uomba.

    **Kwa nini niyajaze maisha yangu kwa upendo kwa ajili ya Wakristo wenzangu?** (Kurasa 155-159)

    ***Ukurasa 155:***

    - Mungu ametupa sisi maelekezo: *"Upendano kwa ajili ya ndugu udumu na uwe zoezi la kudumu—kamwe usiruhusu ushindwe"* (Waebrania 13:1 AMP).

        ***Hadithi:*** Upendo kwa ajili ya ndugu ni jambo tulililoliona huko Romania kwa miaka mingi, lakini hadithi moja iliyotupa changamoto ni hadithi ya mhandisi kijana ambaye alipoteza kazi kwa ajili ya kukutwa na Biblia kwenye dawati lake. Kimsingi katika kipindi hiki kila mtu alifanyia kazi serikalini, kwa hiyo ikiwa ulipoteza kazi, usingeweza kupata kazi nyingine. Kisha serikali ilikufanyia upekuzi, na kama hukuwa na kazi, uliwekwa gerezani. Kwa

namna hiyo, ilikwepa lawama za utesaji wa kidini: Waliichukua kazi kutoka kwa Mkristo, walimweka gerezani kwa kutokuwa na kazi, na walisema kwamba alikuwa gerezani kwa sababu hakuwa anafanya kazi. Mhandisi huyu kijana alikuwa na familia na alikuwa mshirika hai katika kanisa huko Bucharest. Kila siku kwa miaka tisa, waamini wenzake katika kanisa lake walimpelekea chakula ili kumsaidia yeye na familia yake. Kamwe hakikuwa kingi kwa sababu kilikuwa ni kidogo sana kuweza kumtosha kila mtu. Kila siku alitunza kidogo tu kwa ajili ya familia yake na aligawa kilichobaki kwa wengine wenye mahitaji. Mhandisi akawa mchungaji wa kusanyiko hili na leo ni mmoja wa wachungaji wanaoheshimiwa sana huko Romania. **Upendo wa ndugu hawa uliendelea siku baada ya siku. Yalikuwa ni mazoea ya kudumu na kamwe hayakushindwa.**

## **Kwa nini niyajaze maisha yangu kwa ajili ya waliopotea?** (Kurasa 160-164)

***Ukurasa 160:***

- Mungu ametuambia, *"Yeyote asiyependa hamjui Mungu, kwa sababu Mungu ni upendo"* (1 Yohana 4:8 NIV).
  - Kama hatuwapendi waliopotea hata tukashindwa kuwashirikisha habari njema, Mungu, anasema hatumjui Yeye.

    ***Hadithi:*** Tunao marafiki wamishenari huko Ulaya Mashariki. Moja ya majukumu yao ni kutafuta upenyo kwenye shule zote za Ulaya Magharibi na kugawa kitabu kilichojaa maandiko kwa kila mtoto. Kitabu kinaelezea juu ya maisha ya Kristo na kumwalika msomaji kumpokea Kristo katika maisha yake kama Bwana na Mwokozi. Katika shule moja marafiki zetu walitoa kitabu kwa mvulana, na matokeo ya kusoma kwake kitabu hicho, alikuwa Mkristo. Alikichukua kitabu kwa rafiki yake nyumbani lakini hakumwona rafiki yake kwa sababu alikuwa mgonjwa. Alikiacha kitabu kwa wazazi wa mvulana na kuwaomba wamsomee rafiki yake. Wazazi na mvulana mgonjwa hawakuwa waamini, lakini wazazi walipokuwa wamkisomea kitabu kwa sauti yule kijana, wote waliokolewa. Katika siku

chache kijana alifariki na alizikwa na kitabu mkononi mwake. Wazazi walianza kushirikisha habari njema za Yesu kwa marafiki zao na majirani, na kwa miezi michache waliwaleta takribani marafiki na majirani mia moja katika imani iliyo ndani ya Kristo.

- Njia kuu ya kuonyesha upendo kwa waliopotea ni kuwaambia habari za Yesu.

7. Ruhusu kundi ligawanyike katika jozi (wavulana kwa wavulana na wasichana kwa wasichana). Mtake kila mtu kushirikisha kisha **KKK** yafuatayo wakati mshirika mwenza wake akimsikiliza:

    a. **Mistari iliyokaririwa** kwa juma hili lililopita:

    - Mithali 3:5-6
    - 1 Yohana 1:9

    b. **Notsi za kila siku katika Kusoma Biblia (NKSKB)** (Kurasa 65-72) zilizoandikwa juma hili lililopita.

    - Tunaligawa kundi katika jozi ili kwamba kila mmoja aweze kupata nafasi kushirikisha kwa kuongea mistari aliyoishika juma hili na ujumbe mmoja au mbili za UBKS na kisha **K**ufikira kwa kina, **K**uvuta taswira na **K**uombea mistari na notsi za UBKS tena kwa Mungu kama maombi binafsi.
    - Wahamasishe wanafunzi kuwa mawakili wema wa muda huu na siyo kuzungumza juu ya jambo lingine lolote. Huu ni wakati wa kufanyia mazoezi na kukua katika kanuni au nidhamu ya kutafakari.

8. Warudishe wanafunzi tena kwenye kundi kubwa na watake kuweka mistari ifuatayo kwenye kadi za mistari (Ukurasa 235):

- **Warumi 3:23**
- **Warumi 6:23**
- **Yohana 3:16**

*Marudio:*

- Geuza mfuko kwa ndani nyuma ya jalada la kijitabu kidogo na toa kadi moja iliyo wazi kwa kila mstari utakaoukariri juma hili.
- Mara unapokuwa umeushika mstari na kunukuu rejea, mstari rejea mara 30, weka tarehe uliokariri upande huo huo wa kadi kama andiko rejea.

***Muhimu:***

- Ni muhimu sana kuiandika mistari hii kwenye kadi darasani. Wanafunzi wanaweza kuzichukua kwa juma zima na kutumia wakati wanapokuwa wanasubiri, wanapumzika, n.k. ili kushika mistari. Ikiwa hutafanya hivyo darasani, Shetani ataweka vikwazo vingi mbele ya wanafunzi na kufanya hilo kuwa gumu kwa wao kushika mistari kabla hamjakutana tena.

- Kumbuka kwamba kushika mstari kunauingiza kwenye akili zetu. Kutafakari kunauhamisha kwenda mioyoni mwetu. Kwa hiyo, tunashika mistari mapema kadri iwezekanavyo mwanzoni mwa juma ili kwamba tuwe na muda zaidi katika juma kuitafakari kabla hatujakutana tena. Kwa nini kutafakari maandiko? Tunataka Mungu kuitumia mistari katika maisha yetu kutubadilisha katika mfano Wake.

*Kushika na Kutafakari maandiko kunatusaidia kumjua Mungu.*

9. Soma/jadili na kutafakari kweli za (**KKK**) katika… **Damu Mikononi Mwetu?** (Kurasa 37-43) Wakumbushe wanafunzi kuhakiki na **KKK** kweli hizi mara kwa mara.

***Maelezo:***

- "…Damu Mikononi mwetu"
    - Inatuhamasisha katika maeneo ya:
        - Kuzungumza kwa uwazi habari za Yesu katika mazungumzo yetu ya kila siku.
        - Kuwaalika wengine kumpokea Yesu kama Bwana na Mwokozi wao binafsi.
- Bila shaka litakuwa kumbusho la mara kwa mara kwetu la umuhimu na uharaka wa kushuhuhudia.
- Linatoa baadhi ya majibu kwa maswali muhimu kama vile:
    - Kwa nini ni haraka sana kushirikisha ujumbe Wake?
    - Ujumbe Wake ni nini?

    - Ni akina nani wajumbe wake?
    - Nini mbinu yake?
    - Nini wajibu wetu, na nini wajibu wa Roho Mtakatifu?
    - Motisha yetu ni nini?
    - Jinsi gani tunaweza kuwa na ufanisi katika kushirikisha ujumbe wake?
- Inamalizia kwa changamoto za uinjilisti za kila siku.
- ***Hadithi:*** Nilikuwa Afrika na baba mkwe wangu kwa siku thelathani kwa safari ya kimisheni. Tulipata uzoefu mwingi, mmoja ambalo kamwe sitausahau ni hadithi ya binti tuliyekutana naye ambaye alikuwa akipata nafuu hospitalini maeneo ya huko porini. Kabla ya ujio wetu, alijifungasha kwenda mtoni ili kupata maji ya kunywa ndipo mamba alipomng'ata mguuni mwake na kuanza kumvutia kwenye kina kirefu cha maji. Hili halikuwa jambo geni kwa sababu watu wengi walikuwa wamepoteza maisha kutokana na kuchukuliwa na mamba, lakini hadithi hii ilikuwa na mwisho usio wa kawaida. Shangazi wa msichana alisikia kilio chake na aliona kile kilichokuwa kinatokea. Ghafla alikimbilia mtoni na kumvuta msichana kutoka mdomoni mwa mamba na kumleta ukingoni akiwa salama. Watu katika kijiji chake hawakujua nini cha kufanya. Walijaribu kusaidia kwa kuweka dawa ya kuua wadudu kwenye kidonda cha binti huyu, lakini hali ilizidi kuwa mbaya. Mtu mmoja kutoka kijijini alimbeba kwa baiskeli msichana kwenda hospitali, ambapo iliwachukua masaa kadhaa. Daktari aliweza kuuokoa mguu, na wakati msichana huyu mdogo alipokuwa hospitali, mmishenari alimuongoza binti huyu kuwa Mkristo na alimfundisha kushona wakati alipokuwa akiendelea kupata nafuu. Sijui sehemu ya hadithi iliyobakia, lakini ninachojua ni kwamba alikuwa anarudi tena kijijini ambako angekuwa ndiye Mkristo pekee yake akiwa na ujuzi ambao atawafundisha wengine wakati akiwafundisha habari kuhusu Yesu.

    - Ingeweza kuwa rahisi kwa shangazi kusimama ukingoni na wengine na kuangalia tu rafiki au ndugu mwingine akipotelea kwenye mdomo wa mamba, lakini aliamua kutoruhusu hilo kutokea. Alipaswa

kuishinda hofu, lakini upendo wake, huruma na kujali kwake kwa ajili ya binti huyu ulikuwa ni zaidi ya hofu yake. Fikra zangu ni kwamba leo katika kijiji mahali fulani huko Zimbabwe, kuna watu wengi wanaomjua Yesu na kujua jinsi ya kushona – yote haya kwa sababu ya shangazi aliyelijali kiasi cha kufanya jambo fulani wakati wengine wasingeweza.

***Ukurasa 38, sehemu ya III:***

- Mdo 1:8 (NKJV) katika kifungu cha pili inasema, *"... Nanyi mtakuwa mashahidi Wangu..."*
    - Katika sheria za Marekani neno *mta* linamaanisha pasipo hiyari.

***Ukurasa 39:***

- Marejeo ya "wajibu wetu" katika ukurasa 39, sehemu ya V. B inahusika kwa kila Mkristo.
- Kujali kunakuwa moja ya hamasa yetu za msingi (angalia sehemu VI.B). Yesu anasema katika Yohana 10:10, "Mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele" [katika kipimo kamili].*"*

    ***Hadithi:*** INilikuwa kwenye miaka ishirini wakati mama mmoja mzuri, akiwa kwenye miaka sabini aliponijia nikiwa kanisani na kuniuliza ikiwa nitaweza kwenda kumtembelea mwanamme mmoja kwa niaba yake. Alinionya kwamba alikuwa anatokea katika mji aliokulia na kwamba alikuwa mtu katili, mtu mhuni asiyeamini aliyewahi kumjua. Sasa alikuwa katika hali mbaya kiafya na Mungu alimpa kujali kwa hali ya juu sana juu ya kiroho chake. Alikuwa na hofu kwamba angeweza kufa bila Kristo na kuishi milele yote akiwa ametengwa na Mungu. Nilimwambia nitakwenda kuzungumza naye.

    Muda mfupi baada ya hilo, nilikwenda kumtembelea katika nyumba iliyochakaa ambayo ilikuwa imegeuzwa kuwa mahali pa kutunzia wazee. Katika siku hizo nyumba za kutunzia wazee hazikuwa safi, na harufu ilikuwa ya kutisha. Niliingia kwenye ile nyumba na kuuliza mahali ambapo ningeweza kumpata mtu yule. Wafanyakazi walinichukua

nyuma ya nyumba, kwenye ukumbi ambao ulikuwa umezungushiwa ili kutengeneza chumba kingine.

Watu waliokuwa wakimhudumia mtu yule hawakupenda kuwa karibu naye kwa sababu bado alikuwa katili na mhuni, lakini niliketi na kuanza kuzungumza naye. Mara mazungumzo yetu yalihamia kwa Yesu. Baada ya kuzungumza kwa muda, nilimshirikisha Yohana 10:10 na kumwambia kwamba Yesu alikuja kufa msalabani kwa ajili ya dhambi zetu ili kwamba tuwe na uzima. Kisha nilisema, "Kwa hiyo, mpaka mtu anapoweka tumaini lake kwa Yesu, hata kuishi anakuwa haishi, anatembea tu akiwa mfu."

Mtu yule aliangalia chini, machozi yakimtiririka mashavuni mwake. Kisha aliniangalia machoni na kusema, "Na mimi hata kutembea sitembei." Pale ndipo nilipogundua kwamba mtu yule hata kutembea alikuwa hatembei. Nilimwambia jinsi anavyoweza kupokea msamaha wa Mungu, kuokolewa na kumpata Yesu kama Bwana na Mwokozi wake binafsi. Aliitikia kwa kumwomba Mungu msamaha na kumwalika Yesu aingie moyoni mwake.

Nilirudi kumtembelea mara kadhaa na kumkuta mtu mpya. Mungu aliweza kumpatia utu mpya, na wahudumu wake waliniambia kuhusu mabadiliko ndani yake.

- Kila mmoja anastahili fursa ili kumjua Yesu—hata watu katili na wahuni kabisa tunaowajua. Ikiwa hilo ni kweli, inakuwaje kuhusu marafiki, ndugu na majirani zetu?

***Ukurasa 43:***

- Kabla ya kushirikisha "Changamoto za Uinjilisti za Kila Siku," unaweza kutaka kusimulia yafuatayo:

***Hadithi:*** Miaka kadha a iliyopita tulimsikia mwinjilisti akishirikisha kitu fulani alichokipitia wakati akihudhuria seminari ya New Orleans. Alikuwa akiendesha mwendo wa masafa marefu kurudi nyumbani baada ya kuhubiri katika huduma ya uamsho. Ilikuwa ni katikati ya usiku, na alikuwa amechoka sana. Alipokuwa akikatisha daraja la

Pontchartrain karibu na New Orleans, ghafla alimwona mtu kwa mbali, akiwa amesimama katikati ya barabara yake, akipiga kelele na kupunga mikono yote miwili. Mwanafunzi yule alikuwa amechoka na akafikiria angeweza tu kuhamia barabara nyingine na kumpita yule mtu. Lakini kila wakati alipobadilisha barabara, mtu yule alihamia kwenye barabara ile, akipiga kelele na akipunga mikono yote. Hatimaye, mwanafunzi yule alikuja karibu kuona kwamba mtu aliyekuwa akipunga shati lake hewani alijaribu kumsimamisha. Kwa hiyo alisimama, akatoka nje ya gari lake na kwenda mpaka alipokuwa yule mtu ili kuona kuna tatizo gani. Mtu yule alikuwa amechanganyikiwa (pagawa). Alipoweza kusema, mtu yule alisema, sehemu ya daraja imevunjwa na meli kubwa, na basi alilokuwamo limetumbukia chini ya maji. Wengi ndani ya basi walikuwa wamekufa, lakini yeye aliweza kutoka nje ya basi kwa kupanda kwenda barabara kuu ili kuwasimamisha watu wasitumbukie darajani  na kufa. Mwinjilisti yule alituambia, "Nilimkumbatia na kumshukuru—na nikamshukuru tena." Kwa muda wote wa usiku uliosalia alisimama na mtu yule katikati ya barabara kuu, wakipigi kelele "SIMAMA, SIMAMA, SIMAMA au unaangamia."

- Kama tungekuwa katika nafasi ya mtu yule aliyetoka kwenye basi, tungeweza kufanya kitu gani?
- Je linaonekana jambo geni kwamba wakati mwingine tunaweza kujali sana kwa ajili ya maisha ya watu kimwili na kujali kidogo sana kwa ajili ya nafsi zao?
- "Mungu, tupatie huruma kwa ajili nafsi/roho za watu."

10. Wahamasishe wanafunzi kuonyesha upendo wao kwa Mungu mara tatu kila saa wanayokuwa macho kwa juma hili, *"Ninakupenda, Ee Bwana nguvu zangu"* (Zaburi 18:1 NIV).

***Maelezo:***

- Tunaposema, "Bwana, ninakupenda," tunaomba maombi ya kumwabudu Mungu.

- Tunataka kuendeleza kuonyesha upendo wetu kwa Mungu wakati wote wa siku kila siku. Hii ni njia moja ya kufanyia mazoezi Kanuni ya **Kutumbukiza na Kuondoa**.

- Tunataka kuendelea kufanyia mazoezi kanuni hii mpaka inapokuwa hali ya kawaida, kwa asili inakuwa sehemu yetu.

11. Wahamasishe wanafunzi kutafuta fursa za kushirikisha kile ambacho Mungu amewafundisha.

    ***Maelezo:*** Tunataka kuwasaidia wanafunzi kuwa na utulivu wanapozungumza habari za Yesu katika kila eneo la maisha yao.

12. Tafuta usikivu wa wanafunzi katika **kazi** zao **za ziada** (Kurasa 261-262).

    ***Soma darasani:*** Ruhusu muda wa kusoma ukurasa 261 kwa sauti darasani na hakikisha kwamba kila mmoja anaielewa kazi ya ziada.

    - ***Watie moyo wanafunzi wawe waaminifu kwa Mungu katika kukutana Naye kila siku kwa ajili ya wakati wao wa utulivu).***

13. Funga kwa Maombi.

    ***Mfano:*** Waalike wanafunzi kuungana nawe kupiga magoti mnapoomba pamoja na kumshukuruMungu na wewe na kipekee kuzungumza na kila mmoja wenu.

## Mwongozo wa Kiongozi na Ujumbe wa Mwandishi......................Kipindi cha 12

1. Anza kwa maombi.

   ***Mfano:*** Waalike wanafunzi kupiga magoti pamoja nawe mnapoomba pamoja na kuukabidhi muda kwa Mungu.

2. Mtake kila mmoja kufungua katika karatasi ya **Ufuatiliaji** ambayo inahitajika siku hiyo. Kisha unaweza **kuzikagua na kuzisaini** (Ukurasa 283).

   ***Uwajibikaji:*** Ukaguzi na uwekaji sahihi karatasi zao za Ufuatiliaji kila juma huwafundisha wanafunzi katika kanuni ya uwajibikaji iliyofundishwa katika Warumi 14:12.

3. Soma **"Kwa kuwa Kusudi langu la dhati ni kwamba Nimjue Yeye"** (Ukurasa 9-10). Mtake mtu mmoja kushirikisha Kuvuta taswira kwake sehemu moja ya mstari huu na kusikiliza pale anaporudisha Maombi yake kwa Mungu kama ombi lake binafsi. **Wakumbushe wanafunzi kuweka mwelekeo wao kwa Yesu** (Waebrania 12:2).

   ***Kumbusho:*** Tunahakiki Wafilipi 3:10 (AMP) kila juma kwa sababu kuu tatu:

   1. **Ili kuyafanya macho yetu yamwelekee Yesu** na Yesu pekee yake na kutukumbusha kwamba **kusudi letu la dhati ni kumjua Yeye**.
   2. Ili kutukumbusha kwamba **kanuni kama zilivyo siyo mwisho wa mambo. Hizo ni njia tu ambazo Mungu ametupatia ili kumjua Yesu** kwa kina, kwa undani, na kibinafsi.
   3. **Ili kutafakari juu ya kweli zenye nguvu** katika mstari huu ili kwamba ziweze kuhama kutoka kwenye ukurasa kwenda kichwani na kisha kwenda mioyoni mwetu **ili kwamba tuweze kubadilishwa katika mfano wa Yesu**.

4. Mwombe mtu mmoja kushirikisha, kisha **K**ufikiria kwa kina, **K**uvuta taswira, na **K**uombea tena kwa Mungu **Notsi za Mahubiri Somo lake** (Kurasa 21-24).

   *Tunapotulia kidogo ili kutafakari notsi tulizoziandika wakati tunapomsikiliza Mungu anapozungumza nasi katika mahubiri, inatusaidia kumjua Mungu.*

5. Jadili **Maswali ya Marudio ya Kazi za Ziada** (Ukurasa 262).

   ***Maelezo:***

   - Tumia swali la 4, 5 na 6 katika ukurasa 262 kuwahamasisha wanafunzi kuzungumza kwa wengine habari za Yesu na mambo ambayo Anawafundisha.
     - Mruhusu mmoja wao katika kundi kusimulia juu ya uzoefu unaotokana somo la juma lililopita wakati alipozungumza na mtu fulani kuhusu Yesu au kushirikisha kitu chochote ambacho Mungu amemfundisha.

6. Soma/Jadili kwa kina mafunzo ya **Kuyajaza Maisha Yangu katika Upendo (**Kurasa 165-170) Unaposoma na kujadili, mara kwa mara tulia kidogo na kuwapa wanafunzi fursa ya **K**ufikiria kwa kina, **K**uvuta taswira na **K**uomba.

   **Jinsi gani naweza kuyajaza maisha yangu kwa upendo wa Mungu?** (Kurasa 165-170)

   ***Kurasa 166-167, sehemu c:*** Hizi zinaweza kuwa kurasa za muhimu zaidi katika kijitabu kidogo cha mwanafunzi. Mawazo au dhana ni za muhimu sana kiasi kwamba zinaweza kuonekana tena kwenye mafunzo ya juma linalofuata katika kurasa za 172-173, sehemu c. Kwa nini kurasa hizi za muhimu sana?

   - **Ni za muhimu kwa sababu hapa mistari inatufundisha umuhimu wa kujiachilia katika udhibiti wa Roho Mtakatifu na kumwalika Yeye kuwa msimamizi katika maisha yetu kila siku—ni ufunguo katika kuishi maisha ya ushindi ya Kikristo.** Alipoishi hapa duniani:
     - Yesu hakufanya dhambi, na Anapokuwa katika udhibiti wa maisha yetu, sisi pia tutaweza.
     - Yesu alifanya uamuzi sahihi kila wakati, na pale Anapokuwa katika udhibiti wa maisha yetu, sisi pia tutaweza.
     - Yesu alimaliza kazi na kulitimiza kusudi lile ambalo Baba alimtuma. Pale anapokuwa mdhibiti wa maisha yetu, sisi pia tutalitimiza.

- Yesu aliitikia katika kila tatizo na hali au mazingira katika maisha yake kama vile tu Baba alivyomtaka iwe. Pale anapokuwa mdhibiti wa maisha yetu, kwa hiyo sisi pia tutaweza.

- Yesu aliakisi tunda la Roho Mtakatifu—upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole na kiasi. Pale anapokuwa katika udhibiti wa maisha yetu, sisi pia tutaweza.

- **Kama tunajifunza kanuni au nidhamu zote za kiroho na kushindwa kujifunza kuishi chini ya udhibiti wa Mungu, tutakuwa si chochote zaidi ya kuwa washikilia sheria.**
- Hebu tuangalie kwa karibu kurasa 166-167, sehemu c:

  - Neno kujiacchilia  katika kifungu cha kwanza kwenye mstari wa 2 ukurasa 171, sehemu C (katikati ya ukurasa), ni kutoka Warumi 6:13, ambayo linasema, *"... Jitoeni wenyewe kwa Mungu..."* Tafsiri nyingine inasema, *"....Jiachilieni wenyewe katika mikono ya Mungu..."* Ni dhahiri Mungu anasema nasi kwamba tunapaswa kumwacha Yeye awe msimamizi wa maisha yetu kwa kuachilia udhibiti wa maisha yetu Kwake.

  - Yohana 15:4 (NKJV) inasisitiza mambo kadhaa kwetu:

    - Maneno haya, *"kaeni ndani Yangu Nami ndani yenu"* ni kweli inayozungumzia juu ya kuyafanya makao yetu katika Yesu kama tu Yeye alivyofanya makao Yake ndani yetu. Hulibeba wazo la kushirikisha maisha na kuwa katika pumziko na ushirika tulivu na Yesu.

    - Sehemu ya mstari inayobaki, *"kama vile tawi lisivyoweza kuzaa pekee yake, isipokuwa limekaa ndani ya mzabibu, vivyo nanyi hamwezi msipokaa ndani Yangu..."* ni onyo kwetu kwamba tunahitaji kukaa katika ushirika na Yeye. Ni lazima tuwe na bidii katika kuungama dhambi mara moja na kuachilia udhibiti wa maisha yetu tena kwa Yesu kama tunataka kuzaa matunda kwa ajili ya Mungu.

        - Uthibitisho kwamba **tunakaa ndani ya Yesu** ni utii wetu Kwake na Roho Wake aliyetupatia.


            ***Wale wanaotii*** *amri Zake wanaishi ndani Yake, na Yeye ndani yao. Na hivi ndivyo tunavyojua kwamba anakaa ndani yetu. Tunajua hilo kwa* ***Roho wake aliyetupa*** (1 Yohana 3:24 NIV).

- Wafilipi 2:13 (AMP) inasisitiza kwamba:
    - Hatujaribu kufanya kazi ya Mungu katika nguvu zetu wenyewe. Ikiwa tutafanya hivyo, tutashindwa.
    - Pale tunapoishi chini ya udhibiti wa Neno la Mungu:
        - Mungu anakuwa kazini ndani yetu:
            - Yeye anatutia nguvu.
            - Hutuumbia ndani yetu nguvu na shauku ya:
                - Kutaka kufanya kazi kwa ajili Yake.
                - Kufanya kazi kwa ajili ya furaha njema, utoshelevu na kupendezwa kwake.
            - Kama hatuna shauku ya kufanya kazi kwa ajili ya Mungu au kumletea furaha, utoshelevu na kumpendeza Yeye, tunadhirihisha kwamba hatuishi chini ya udhibiti wake.

- Wagalatia 5:22-25 (LIV) inasisitiza:
    - Mistari 22-23—Hakuna ubishi kwamba *"... Pale Roho Mtakatifu* ***anapodhibiti*** *maisha yetu* ***atazalisha aina hii ya tunda ndani yetu****":*
        - Upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole na kiasi.
            - Hili ni tunda la Roho Mtakatifu, na ni **Roho Mtakatiuf anayeweza kulizalisha katika hali yake halisi**.

- Tumehakikishiwa kwamba ikiwa Roho Mtakatifu yupo katika udhibiti, Atazalisha tunda hili ndani yetu.
    - Pale wengine wanapoliona tunda hili ndani yetu, kwa hakika Roho Mtakatifu ni mdhibiti, na tunamruhusu Yeye kuwa msimamizi.
    - Pale anapokuwa siyo mdhibiti wa maisha yetu, hakutakuwa na tunda halisi la Roho Mtakatifu.
- Mstari wa 24—*"Wale walio wa Kristo wameusulubisha utu wao wa asili wenye tamaa mbaya juu ya msalaba Wake na alizigongomelea dhambi zao pale."*
  - Jinsi gani tunausulubisha utu wetu wa asili wenye tamaa msalabani Kwake na kuzigongomelea dhambi pale?
    - Pale tunapoachilia udhibiti na kiti cha enzi ndani ya mioyo yetu kwa Mungu, hapo ndipo tunausulubilia utu wetu wa dhambi wa asili kwa sababu ndani ya mioyo yetu kuna nafasi mbili tu – kiti cha enzi na msalaba. Pale utu wetu wa kale wenye asili ya dhambi unapokuwa haupo kwenye kiti cha enzi, ni lazima uwe juu ya msalaba.

***Kielelezo:***




**RM = Roho Mtakatifu**
**UWKWD = Utu Wetu wa Kale wa Dhambi**

- Mstari wa 25—"Kama tunaishi sasa kwa nguvu za Roho Mtakatifu, hebu tuufuate uongozi wa Roho Mtakatifu katika kila eneo la maisha yetu."
    - Ni wajibu wetu:
        - Kujiachilia katika udhibiti wa Roho Mtakatifu.
        - Kukaa chini ya udhibiti wa Roho Mtakatifu.
        - Kuhakikisha kwamba tunaachilia kila eneo la maisha yetu kwa Roho Mtakatifu na kwamba hakuna kilichozuiliwa katika udhibiti Wake:
            - Hakuna chumba cha siri au faragha katika mioyo yetu kilichoandikwa "Mambo Binafsi" au "Usiingie"
    - Kutupa sisi fursa ya kuishi chini ya udhibitii wa Roho Mtakatifu ni kielelezo kikubwa cha upendo wa Mungu, rehema na neema Yake kwetu.
    - **Maombi yetu yanapaswa kuwa**: "Bwana, nitakwenda popote Unaponitaka kwenda na kufanya chochote unachonitaka kukifanya; ninachokitaka ni kutembea katika kitovu cha mapenzi Yako na kuleta furaha, heshima na utukufu Kwako na udhibiti Wako."
- Jambo moja ambalo linathibitisha kwamba tunampenda Mungu ni kwamba *"...Amri zake siyo nzito"* (1 Yohana 5:3 NKJV).

7. Ruhusu kundi kugawanyika katika jozi (wavulana kwa wavulana na wasichana kwa wasichana). Mtake kila mmoja kushirikisha kisha **KKK** yafuatayo wakati mshiriki wake mwenza akimsikiliza:
    a. **Mistari Iliyokaririwa** juma hili lililopita:
        - Warumi 3:23
        - Warumi 6:23
        - Yohana 3:16

    b. **Notsi za UBKS** zilizoandaliwa juma hili lililopita.

- Wahamasishe wanafunzi kuwa mawikili wema wa muda huu na si kuzungumza juu ya kitu kingine chochote. Huu ni wakati wa kutenda na kukua katika nidhamu ya kutafakari.

8. Warudishe wanafunzi tena katika kundi kubwa na watake kuweka mistari ifuatayo kwenye kadi za mistari (Ukurasa 235):

**• Yohana 1:12 • Efeso 2:8-9**

***Marudio:***

- Geuza kwenye mfuko ulio ndani nyuma ya jarida la kijitabu kidogo na kuchukua kadi ya mstari iliyo wazi kwa ajili ya kila mstari utakaokuwa unaushika juma hili.

***Muhimu:***

- Ni muhimu sana kuandika mistari hii kwenye kadi darasani. Wanafunzi wanaweza kutembea nayo kwa juma zima ili kuitumia muda kuikariri katika juma hili wanapokuwa wanasubiri, wanapumzika, n.k. Kama hutafanya hivi darasani, Shetani anaweza kuweka vikwazo mbele ya wanafunzi na kufanya hili kuwa gumu kwa ajili yao kupata mistari ya kukariri kabla ya kukutana nao tena.
- Kumbuka kwamba kushika mistari kunaiingiza katika akili zetu. Kutafakari kunaihamisa kwenda mioyoni mwetu, kwa hiyo, tunaishika mistari mapema katika juma kadri iwezekanavyo ili kutupa muda zaidi tuweze kuitafakari kabla ya kukutana tena. Kwa nini kutafakari maandiko? Tunataka Mungu kuitumia mistari katika maisha yetu ili kutubadilisha kuwa katika mfano Wake.

*Kushika na kutafakari maandiko kunatusaidia kumjua Mungu.*

9. Wahamasishe wanafunzi kuonyesha upendo wao kwa Mungu mara tatu kila saa wanayokuwa macho kwa juma hili, *"Ninakupenda, Ee Bwana nguvu zangu"* (Zaburi 18:1 NIV).

***Maelezo:***

- Tunaposema, "Bwana, ninakupenda," tunaomba maombi ya kumwabudu Mungu.

- Tunataka kuchochea kuonyesha upendo wetu kwa Mungu wakati wote wa siku kila siku. Hii ni njia moja ya kuzifanyia kazi **Kanuni ya Kuweka Kitu Mbadala**.
- Tunataka kuendelea kufanyia mazoezi hili mpaka linapokuwa la kawaida, la asili kwa upande wetu.

10. Wahamasishe wanafunzi kutafuta fursa za kushirikisha kile ambacho Mungu amewafundisha.

    ***Maelezo:*** Tunataka kuwasaidia wanafunzi kuwa na utulivu wanapozungumza habari za Yesu katika kila eneo la maisha yao.

11. Tafuta umakini au usikivu wa wanafunzi katika **kazi** zao **za ziada** (Kurasa 263-264).

    ***Soma darasani:*** Ruhusu muda wa kusoma ukurasa 263 kwa sauti darasani na hakikisha kwamba kila mmoja anaielewa kazi ya ziada.

    ***Wahamasishe wanafunzi kukutana na Mungu mapema kila asubuhi katika muda wao wa utulivu***.

    > ***...Ee Mungu, Mungu wangu, Nitakutafuta kwa bidii asubuhi mapema...*** (Zaburi 63:1). (*Strong's Exhaustive Concordance of the Bible*, "Hebrew and Chaldee Dictionary," Ukurasa 114, namba 7836)

12. Funga kwa Maombi.

    ***Mfano:*** Waalike wanafunzi kuungana nawe kupiga magoti mnapoomba pamoja na kumshukuru Mungu kwa kukutana nanyi na kipekee kuzungumza na kila mmoja wenu.

## Mwongozo wa Kiongozi na Ujumbe wa Mwandishi......................Kipindi cha 13

1. Anza kwa maombi.

   ***Mfano:*** Waalike wanafunzi kupiga magoti pamoja nawe mnapoomba pamoja na kuukabidhi muda kwa Mungu.

2. Mtake kila mmoja kufungua katika karatasi ya **Ufuatiliaji** ambayo inahitajika siku hiyo. Kisha unaweza **kuzikagua na kuzisaini** (Ukurasa 284).

   ***Uwajibikaji:*** Ukaguzi na uwekaji sahihi karatasi zao za Ufuatiliaji kila juma huwafundisha wanafunzi katika kanuni ya uwajibikaji iliyofundishwa katika Warumi 14:12.

3. Soma **"Kwa kuwa Kusudi langu la dhati ni kwamba Nimjue Yeye"** (Ukurasa 9). Mtake mtu mmoja kushirikisha Kuvuta taswira kwake sehemu moja ya mstari huu na kumsikiliza pale anaporudisha Maombi yake kwa Mungu kama ombi lake binafsi. **Wakumbushe wanafunzi kuweka mwelekeo wao kwa Yesu** (Waebrania 12:2).

   ***Kumbusho:*** Tunahakiki Wafilipi 3:10 (AMP) kila juma kwa sababu kuu tatu:

   1. **Ili kuyafanya macho yetu yamwelekee Yesu** na Yesu pekee yake na kutukumbusha kwamba **kusudi letu la dhati ni kumjua Yeye**.
   2. Ili kutukumbusha kwamba **kanuni kama zilivyo siyo mwisho wa mambo. Hizo ni njia tu ambazo Mungu ametupatia ili kumjua Yesu** kwa kina, kwa undani, na kibinafsi.
   3. **Ili kutafakari juu ya kweli zenye nguvu** katika mstari huu ili kwamba ziweze kuhama kutoka kwenye ukurasa kwenda kichwani na kisha kwenda mioyoni mwetu **ili kwamba tuweze kubadilishwa katika mfano wa Yesu**.

4. Mwombe mtu mmoja kushirikisha kisha **K**ufikiria kwa kina, **K**uvuta taswira, na **K**uombea tena kwa Mungu **Notsi za Mahubiri au Somo lake** (Kurasa 21-24).

***Marudio:***

- Tunahudhuria ibada ya kuabudu tukitarajia Mungu kuzungumza nasi. Pale Anapozungumza, tunapaswa kujiandaa kuandika kile Anachokisema. Mara tunapokiandika, tunaweza kuzitunza notsi mpaka tunapokuwa na muda wa kuzitafakari kweli zilizomo ndani yake. Pale tunapotafakari (**K**ufikiria kwa kina, **K**uvuta taswira na **K**uombea kweli hizo tena kama maombi binafsi), tunazihamisha kweli kutoka vichwani mwetu kwenda mioyoni mwetu ambako zinaweza kufanya kazi yake katika utekelezaji.

*Tunapotulia kidogo ili kutafakari notsi tulizoziandika pale tunapomsikiliza Mungu anapozungumza nasi katika mahubiri, inatusaidia kumjua Mungu.*

5. Jadili **Maswali ya Marudio ya Kazi za Ziada** (Ukurasa 264).

***Maelezo:***

- Tumia swali la 4, 5  na 6 katika ukurasa 264 kuwahamasisha wanafunzi kuzungumza kwa wengine habari za Yesu na mambo ambayo Anawafundisha.

  - Mruhusu mmoja wao katika kundi kusimulia juu ya uzoefu unaotokana na somo la juma lililopita wakati alipozungumza na mtu yeyote kuhusu Yesu au kushirikisha kitu chochote ambacho Mungu amemfundisha.

6. Soma/Jadili kwa kina somo la **Jinsi gani naweza kuyajaza maisha yangu na upendo kwa ajili ya wengine (Wakristo wenzangu na waliopotea)?** (Kurasa 171-178)  Unaposoma na kujadili, mara kwa mara tulia kidogo ili kuwapa wanafunzi fursa ya **K**ufikiria kwa kina, **K**uvuta taswira na **K**uomba.

***Ukurasa 171, sehemu B. 1. a:*** Tunaweza kuendeleza upendo kwa ajili ya waliopotea kwa kuwaona kama Mungu anavyowaangalia katika hali yao ya kupotea.

- Jinsi gani Mungu anamwangalia mtu aliyepotea?

- *"...mliishi mbali na Kristo…. Mmefarakana na watu wa Mungu…. Pasipo Mungu na pasipo tumaini"* (Efeso 2:12 NLT).

    - Je tunawezaje kuizuia mioyo yetu na upendo wetu kwa mtu mwenye hali hiyo?

***Kurasa 172-173, sehemu c, 1-4:*** Angalia notsi zetu zote kuanzia mafunzo ya juma lililopita katika kurasa 166-167, sehemu c.

- Weka msisitizo au mkazo tena kwa baadhi ya vipengele muhimu kutoka kwenye mafunzo ya juma lililopita.
    - Kwa nini? Kweli zilizojadiwa hapo ni za muhimu katika kuishi maisha ya Kikristo ya ushindi.

***Ukurasa 178:***

***Andika*** katika ukurasa huu mambo haya mawili kuhusu upendo wa kweli:

1. Ni kitu kinachoakisi (toa picha halisi) zaidi kuliko vile kinavyotendwa.
2. Ni uchaguzi. Ni lazima nichague kujiachilia kwenye udhibiti wa Roho Mtakatifu na kumruhusu kuzalisha upendo kupitia mimi.

7. Ruhusu kundi kugawanyika katika jozi (wavulana kwa wavulana na wasichana kwa wasichana). Watake kila mtu kushirikisha kisha **KKK** yafuatayo wakati mshirika wake mwenzi anamsikiliza:

    a. Mistari iliyokaririwa juma lililopita:

    - Yohana 1:12 • Efeso 2:8-9

    b. **Notsi za kila siku katika Kusoma Biblia (NK-SKB)** (Kurasa 65-72) zilizotengenezwa juma lililopita.

    - Wahamasishe wanafunzi kuwa mawakili wema wa muda huu na wasizungumzie kuhusu kitu kingine chochote. Huu ni muda wa kufanyia mazoezi na kukua katika nidhamu ya kutafakari.

8. Warudishe wanafunzi tena kwenye kundi kubwa na watake kuweka mistari ifuatayo kwenye kadi za mistari (Ukurasa 235):

- **Luka 9:23** • **Warumi 6:13** • **Yohana 15:4**

***Marudio:***

- Geuza kwenye mfuko upande wa ndani nyuma ya jaridi la kijitabu kidogo na chukua kadi ya mstari iliyo wazi kwa kila mstari utakaoukariri juma hili.

***Muhimu:***

- Ni muhimu sana kuandika mistari hii kwenye kadi darasani. Wanafunzi wanaweza kutembea nazo juma lote na kuzitumia katika juma hili kukariri mistari wakati wanapokuwa wanasubiri, wanapokuwa kwenye mapumziko, n.k.
- Kumbuka kwamba kushika mistari kunaingiza akilini mwetu. Kutafakari kunaihamishia kwenda kwenye mioyo yetu.

*Kushika na kutafakari maandiko kunatusaidia kumjua Mungu.*

9. Wape wanafunzi jaribio juu ya **Jinsi ya Kutambua Kiwango cha Upendo Wangu** (Ukurasa 30). Watake kujumlisha pointi zao na kugawanya namba hiyo kwa 1.40 kupata asilimia ya pointi za jumla zinazoweza kupatikana. Watake kutafakari (**KKK**) jinsi ya kuboresha maeneo yao yenye udhaifu kwa kuyaachilia katika udhibiti wa Roho Mtakatifu kila siku.

***Maelezo:*** Hili ni jaribio ambalo litakupa changamoto na kukufunulia kiwango cha ubora wa upendo wako.

- Natumaini kuwa jaribio hili:
    - Linatufanya sisi kutambua maeneo ambayo tunapungukiwa katika kuakisi upendo wa Mungu.

- Linatukumbusha kwamba kiwango pekee ambacho tunapaswa kuupimia upendo wetu ni Neno la Mungu – Yesu, Neno linaloishi (lililo hai), na Biblia, Neno lililoandikwa.

- Linatusaidia kuelewa jinsi gani tulivyo na upungufu katika nguvu zetu wenyewe za kupenda kama Mungu anavyopenda, huku tukijifunza jinsi mapenzi ya Mungu yanavyoakisi upendo Wake kupitia sisi pale tunapojiachilia katika udhibiti Wake na kumuruhusu kuwa msimamizi wa maisha yetu.

- Mtake kila mmoja wa wanafunzi kuchukua kipande cha karatasi na kuiweka kama hivi:

A | B

1.
2.
3.
4-12 {
13.
14.

Total ____ ____

÷ ÷

1.40 1.40

= =

____ % ____ %

- Msiandike majina juu ya karatasi zenu, lakini fanya A iwakilishe mtu fulani ambaye kwa kweli unafikiri unampenda na ifanye B iwakilishe mtu fulani ambaye kwa kweli siyo rahisi kwa wewe kumpenda.

- Chini upande wa kushoto wa ukurasa, weka namba 1 hadi 14.

- Ukiwa na watu wako A na B akilini, pitia jaribio kwenye ukurasa 30, na jitathmini mwenyewe kwa kutumia kipimo cha 1 hadi 10, 10 ikiwa alama ya juu ya ubora wa upendo kwa safu zote mbili A na B.
- Jumlisha kila safu na gawanya jumla ya kila safu kwa 1.40 ili kupata asilimia ya pointi zote zinazowezekana.
    - Unaweza kutaka kuchukua au kuleta mashine ya hesabu darasani ili kuitumia darasani.
- Sasa liweke kundi katika mjadala. Unaweza kuwauliza wanafunzi baadhi ya maswali kama haya yafuatayo:
    - Nini kilikushangaza zaidi juu ya matokeo ya jaribio lako? Elezea.
    - Je Mungu alikuonyesha baadhi ya maeneo yenye udhaifu ambayo unahitaji kuboresha? Tuambie kuhusu maeneo hayo.
    - Kwa kuwa kanuni ya Kiblia ni Kweli zilitolewa na Mungu ambazo zinakuwa msingi au sababu ya kuamsha mitazamo ya imani na matendo, jinsi gani tunaweza kwa maneno yetu kuonyesha swali la kwanza kama kanuni (1 Wakorintho13:4 LIV)?
        - Jibu: Upendo ni kuvumilia.
            - Sasa, Jinsi gani tunaweza, kwa imani kuruhusu kweli hiyo iliyotolewa na Mungu kubadilisha mitazamo na matendo yetu mabaya?
                1. **Kubali wajibu (kuwajibika)** kwa ajili ya mitazamo na matendo yetu mabaya, na kumtii Mungu.
                2. **Tambua** kwamba *"(siyo kwa nguvu zako mwenyewe) kwa kuwa ni Mungu anayeleta matokeo*

*yanayotakiwa katika utendaji ndani yako—akitutia nguvu na kuzalisha uwezo na shauku.-yote katika mapenzi na kutenda kwa ajili ya furaha na utoshelevu na kupendezwa kwako."* (Wafilipi 2:13 AMP).

- Kama ni kuzaa tunda la Roho Mtakatifu au kufanya kazi ya huduma, **hatuwezi** kufanya pasipo Mungu.
    - **Mungu hataweza kuzalisha tunda la Roho Mtakatifu ndani yetu isipokuwa amefanyika kuwa mdhibiti wa maisha yetu** (Wagalatia 5:22 LIV).
    - Pia ni kweli kwamba mara nyingi **Mungu hataweza** kutenda kazi ya huduma pasipo sisi kwa sababu Amechagua kututumia sisi.
    - Tuliumbwa katika Kristo Yesu kufanya kazi njema (Efeso 2:10 NIV), na tumekirimiwa vipawa *"kwa ajili ya kuwakamilisha* [kuwaandaa] *watakatifu* [watu wa Mungu], *kwa kazi ya huduma* [kazi za kuhudumia], *ili kuujenga* [kujenga] *mwili wa Kristo"* (Efeso 4:12).
        - Kwa hiyo, **Kimsingi Mungu amechagua kufanya kazi ya huduma kupitia sisi**.

- Isaya anasema, *"Nami nikasikia sauti yake Bwana akasema, tumtume nani, na ni nani atakwenda kwa ajili yetu? Ndipo niliposema, Mimi hapa, nitume mimi. Naye akaniambia, Nenda…"* (Isaya 6:8-9).
    - Inafurahisha na kuhamsisha pia kwamba **kile Mungu alichotaka kufanya na Isaya ilikuwa kutaja hitaji, na Isaya alijitolea kumruhusu Mungu kulitimiza kusudi hilo kupitia yeye**.

3. **Mtumaini au mwamini Mungu kukamilisha kazi yake ndani yetu ya kutufinyanga na kutuumba katika mfano wake**.
4. **Shirikiana na Mungu** kupitia utii kwa kufanyia kazi kanuni za kiroho ambazo zinatuwezesha kuyajaza maisha yetu kwa Neno la Mungu na maombi. Tunapofanya hili, atatuandaa na kututumia kuleta utukufu Kwake.
    - Kazi yetu ni *"Msiwe wasikiaji wa neno tu, hali mkijidanganya nafsi zetu*

*namna hiyo. Fanyeni kile linachosema"* (Yakobo 1:22 NIV).

5. **Tafakari (K**ufikiria kwa kina, **K**uvuta taswira na **K**uombea) kweli hizi ndani ya mioyo yetu kwa sababu kutafakari juu ya kweli hutuongoza kuzitekeleza kweli hizo.
6. **Kuachilia** udhibiti wa maisha yetu kwa Yesu kwa sababu pale anapokuwa katika udhibiti, Atajiakisi mweyewe kupitia sisi, na Yeye ni kweli na upendo pia.
   - Kama Yesu angekuwa kwenye udhibiti wakati wote wa maisha yetu, kiwango chetu cha ufaulu siku zote kingekuwa 100%..

- Je, ni jinsi gani kutafakari kanuni kumi na nne zilizodokezwa au kuelezwa katika jaribio hili zinaweza kutusaidia sisi? Elezea.
- Jinsi gani unafikiri kuishi chini ya udhibiti wa Mungu kunaweza kutusaidia kumpenda Mungu zaidi katika uhusiano wetu? Elezea.

- **Wahamasishe wanafunzi kujitoa katika jaribio hili mara kwa mara ili kuangalia ubora wa upendo wao katika mahusiano yao**.

10. Jadili **Changamoto za Kusoma Biblia Kila Siku kwa Mwezi wa Nne na Baadaye** (Ukurasa 50). Wahamasishe wanafunzi kuanza katika changamoto hii kesho asubuhi.

    ***Maelezo:*** Hii huongeza sehemu ya mwisho ya Kalenda ya Usomaji wa Biblia Kila Siku, ambayo hutoa mpango kwa ajili ya usomaji wote mara moja kwa mwaka kwa kipindi chote cha maisha yetu.

    - Hii huongeza sehemu ya mwisho ya Kalenda ya Usomaji wa Biblia Kila Siku, ambayo hutoa mpango kwa ajili ya

usomaji wote mara moja kwa mwaka kwa kipindi chote cha maisha yetu?

- **Njia ya kupata uelewa wa picha nzima, kweli ambazo Mungu anataka kuuwasilisha kwetu katika Biblia ni kuisoma yote katika ujumla wake, kwa kila mtu mzima**. Njia nyingine ya kuliingiza Neno la Mungu katika akili zetu, kama vile kusikia Neno linalohubiriwa, kujifunza Neno na kulishika Neno hilo, kwa ujumla huzingatia katika vipengele vidogovidogo au sehemu ya maandiko katika muda wowote. Kwa upande mwingine, kusoma Biblia yote mara moja kwa mwaka kunatupatia picha nzima tunayoihitaji. Njia zote nne za kuliingiza Neno la Mungu kwenye akili zetu ni za muhimu kwa sababu tunahitaji kujifunza ili kuhakikia au kutathmini Neno la Mungu kupitia njia zote mbili, yaani hadubini inayopima kwa karibu na darubini inayoona mbali.

- **Kwa kadri tunavyosoma zaidi Biblia yote, ndivyo tunavyozidi kuwa na msingi katika kweli hizi.**

- Mara kwa mara Mungu anatushirikisha kweli moja kutoka kwenye Neno lake na kisha analileta katika mizani (ulinganifu) kwa kutuonyesha kweli nyingine katika Neno lake. **Kusoma Biblia yote mara moja kwa mwaka kunatufanya tuwepo katika shauri lote la Mungu ili kwamba aweze kuzionyesha kweli zenye ulinganifu tunazozihitaji katika maisha yetu.** Hii inaweza kutusaidia katika kuzuia kupoteza muda katika sehemu ndogo au kuyakita maisha yetu katika kweli zisizo na uwiano.

- Tunahitaji kuhakikisha kwamba tunaisoma Biblia yote mara moja kwa mwaka kwa kipindi chote cha maisha yetu. Mara kwa mara sikiliza Neno la Mungu linalohubiriwa. Kwa uthabiti tunajifunza na kushika Neno la Mungu kwa sababu hivi ndivyo tunavyoiingiza kweli kwenye vichwa vyetu. Kisha tunatafakari katika kila moja ya kweli hizi

ili kuzihamishia kutoka kwenye vichwa vyetu kwenda mioyoni mwetu ambako Mungu anazitumia kutubadilisha katika mfano wake.

11. Wahamasishe wanafunzi kuonyesha upendo wao kwa Mungu mara tatu kila saa wanayokuwa macho juma hili *"Ninakupenda, Ee Bwana, nguvu zangu"* (Zaburi 18:1 NIV).

12. Wahamasishe wanafunzi kutafuta fursa kwa ajili ya kushirikisha kile ambacho Mungu anawafundisha.

    ***Maelezo:*** Tunataka kuwasaidia wanafunzi kuwa watulivu katika kuzungumza habari za Yesu katika maeneo yote ya maisha yao.

13. Tafuta kupata umakini wa wanafunzi kwa **Kazi** zao **za Ziada** (Kurasa 265-266).

    ***Soma darasani:*** Ruhusu muda wa kusoma ukurasa 262 kwa sauti darasani na hakikisha kwamba kila mmoja anaielewa kazi ya ziada.

    - ***Wahamasishe kuwa waaminifu kwa Mungu na kukutana Naye kila siku katika wakati wao wa utulivu.***

14. Funga kwa Maombi.

    ***Mfano:*** Waalike wanafunzi kuungana nawe kupiga magoti mnapoomba pamoja na kumshukuru Mungu kwa kukutana nanyi na kipekee kuzungumza na kila mmoja wenu.

## Mwongozo wa Kiongozi na Ujumbe wa Mwandishi......................Kipindi cha 14

1. Anza kwa maombi.

    ***Mfano:*** Waalike wanafunzi kupiga magoti pamoja nawe mnapoomba pamoja na kuukabidhi muda kwa Mungu.

2. Mtake kila mmoja kufungua katika karatasi ya **Ufuatiliaji** ambayo inahitajika siku hiyo. Kisha unaweza **kuzikagua na kuzisaini** (Ukurasa 285).

    ***Uwajibikaji:*** Ukaguzi na uwekaji sahihi karatasi zao za Ufuatiliaji kila juma huwafundisha wanafunzi katika kanuni ya uwajibikaji iliyofundishwa katika Warumi 14:12. Pia inakusaidia wewe kama kiongozi kuona kama wanafunzi wako:

    - Wanafanya kazi za ziada na kujijengea mtindo wa maisha au
    - Wanahitaji kuhamasishwa au kutiwa moyo na wewe.

3. Soma **"Kwa kuwa Kusudi langu la dhati ni kwamba Nimjue Yeye"** (Ukurasa 9). Mtake mtu mmoja kushirikisha Kuvuta taswira kwake sehemu moja ya mstari huu na kumsikiliza pale anaporudisha Maombi yake kwa Mungu kama ombi lake binafsi. **Wakumbushe wanafunzi kuweka mwelekeo wao kwa Yesu** (Waebrania 12:2).

    ***Kumbusho:*** Tunahakiki Wafilipi 3:10 (AMP) kila juma kwa sababu kuu tatu:

    1. **Ili kuyafanya macho yetu yamwelekee Yesu** na Yesu pekee yake na kutukumbusha kwamba **kusudi letu la dhati ni kumjua Yeye**.
    2. Ili kutukumbusha kwamba **kanuni kama zilivyo siyo mwisho wa mambo. Hizo ni njia tu ambazo Mungu ametupatia ili kumjua Yesu** kwa kina, kwa undani, na kibinafsi.
    3. **Ili kutafakari juu ya kweli zenye nguvu** katika mstari huu ili kwamba ziweze kuhama kutoka kwenye ukurasa kwenda kichwani na kisha kwenda mioyoni mwetu **ili kwamba tuweze kubadilishwa katika mfano wa Yesu**.

4. Mwombe mtu mmoja kushirikisha kisha **K**ufikiria kwa kina, **K**uvuta taswira na **K**uombea tena kwa Mungu **Notsi za Mahubiri au Somo lake** (Kurasa 21-24).

    *Tunapotulia ili kuzitafakari notsi tulizoziandika wakati tunapomsikiliza Mungu anapozungumza nasi katika mahubiri, inatusaidia kumjua Mungu.*

5. Jadili **Maswali ya Marudio kwa Kazi za Ziada** (Ukurasa 266).

    ***Maelezo:***

    - Tumia swali la 6, 7 na 8 katika ukurasa 266 kuwahamasisha wanafunzi kuzungumza kwa wengine kuhusu Yesu na mambo ambayo Anawafundisha.

        - Mruhusu mmoja wao katika kundi kusimulia juu ya uzoefu unaotokana na somo la juma lililopita wakati alipozungumza na mtu yeyote kuhusu Yesu au kushirikisha kitu chochote ambacho Mungu Anamfundisha.

6. Soma/Jadili kwa kina somo la **Jinsi gani naweza kuyajaza maisha yangu na upendo kwa ajili ya wengine (Wakristo wenzangu na waliopotea)**? (Kurasa 179-186)  Unaposoma na kujadili, mara kwa mara tulia kidogo ili kuwapa wanafunzi fursa ya **K**utafakari, **K**usawiri/kufafanua na **K**uomba.

    ***Kurasa 179-180:***

    - Katika kurasa hizi kuna kanuni kumi na nne zilizoorodheshwa ambazo zinatoka kwenye 1Wakorinto 13 na zinatuonyesha jinsi ya kuuonyesha upendo wetu kwa wengine (Wakristo wenzetu na waliopotea).

        - Jinsi gani tunaweza kuziondoa kanuni hizi kwenye ukurasa na kuziweka mioyoni mwetu? Angalia notsi za mwandishi katika mafunzo ya juma lililopita.

    ***Kurasa 180-182:***

    - Kila mmoja wetu anawajibika kwa ajili ya ushirika wetu na Wakristo wengine na Wakristo ndani ya kanisa letu.

**Hapa kuna mambo manne ambayo ni lazima tuyafanyie kazi ili kudumisha ushirika wenye upendo**:

1. **Umoja (Maelewano).**
2. **Ubia (Uwenzi).**
3. **Kushirikiana au Kushirikishana.**
4. **Kuwa pamoja au Umoja**

***Ukurasa 183, sehemu c) (1):***

- *"Kwa hiyo mahali popote tunapokwenda tunazungumzia habari za Kristo kwa wote ambao watatusikiliza....."* (Wakolosai 1:28 LIV). Hii ni moja ya changamoto kubwa kwa waamini wakweli katika Neno la Mungu lote.

    - Mstari huu unatufundisha kwamba tunapaswa kujiandaa kuzungumza habari za Kristo kwa wote ambao watakao tusikiliza.

      ***Hadithi #1:*** Hii ni hadithi juu ya mkasa wa kuwa shahidi asiyejiandaa au asiyetaka. Wakati Vita ya Pili ya Dunia ilipoanza, Newman alikuwa mwanafunzi chuoni. Miaka mingi baadaye alikuwa mchungaji wetu. Wakati alipokuwa chuoni, alikuwa na rafiki wa karibu sana. Walifanya kila kitu pamoja. Walitembea kwenda darasani pamoja, walitumia muda wao wa ziada pamoja, walikuwa ni marafiki wazuri sana. Wakati vita ilipoanza, vijana wote katika darasa lake walikwenda kwenye ofisi ya kujiandikisha siku iliyofuata na walijiunga na jeshi. Newman na rafiki yake mpenzi walikwenda pamoja, lakini walitenganishwa na wakapalekwa makambi tofauti ya mafunzo; kwa hiyo, Newman hakumuona rafiki yake tena kwa muda mrefu.

      Newman alipigana Ulaya chini ya Jenerali Patton. Kila mara alionekana kuwa katika sehemu ya mapigano makali huko vitani. Alipandishwa cheo kufikia ngazi ya kapteni kama kamanda wa mstari wa mbele. Katika kombania yake ya wanaume 100, kila mwanamme isipokuwa Newman na wanaume wengine watatu waliuawa na kubadilishwa mara tano zaidi, ikimaanisha kwamba karibu wanaume 500 walikuwa wameuawa chini ya uongozi wake.

Siku moja kombania ya Newman na kombania zingine kutoka Marekani zilihusika katika kuutwaa mji. Newman alikuwa amesimama kwenye kona ya jengo wakati askari wa Kimarekani alikimbia kukatiza eneo la wazi na alipigwa mara kadha kwa bunduki ya rashasha (machine gun) ya adui. Newman aliona nini kilikuwa kimetokea na akamkimbilia yule mtu kuona kama angeweza kumsaidia. Mtu yule alikuwa amelala uso wake ukielekea chini, kwa hiyo Newman akamgeuza. Kwa mshangao, alikuwa ni rafiki yake mpenzi wa chuoni.

Wakati alipokuwa amemshikilia rafiki yake mikononi mwake, rafiki alisema, "Nisaidie! Nisaidie!"

Newman alimjibu, "Subiri! Madaktari wako njiani! Msaada unakuja!"

"Hapana" alisema rafiki wa Newman. "Niambie habari za Yesu"

Baadaye Newman alisema, "Nilikuwa Mkristo wa kawaida tu, kiasi kwamba kamwe sikuwahi kuzungumza naye habari za Yesu, na sikujua nini cha kusema." Kwa masikitiko makubwa, ndani ya muda mfupi rafiki yake mpenzi alifariki mikononi mwake na alikwenda kwenye umilele pasipo Kristo, kwa sababu tu Newman hakuwa amejiandaa kushirikisha Habari Njema za Yesu.

***Hadithi #2:*** Katika kulinganisha, hapa kuna hadithi yenye changamoto kuhusu shahidi aliyejiandaa na aliyekuwa na utayari aliyetumika katika kombania ya Newman. Sajenti Beck alizungumza juu ya Yesu kwa kila mtu ambaye angeweza kusikiliza na alikuwa shahidi mwaminifu kwa ajili ya Kristo. Siku moja amri ilitolewa kutoka makao makuu kwa ajili ya Newman kupeleka kikosi kwenye doria nyuma ya kambi ya maadui, kwa hiyo alikwenda kwenye kombania na kupitia orodha ya watu walio kwenye kombania na kuwaita majina ya wanaume waliotakiwa kwenda kwenye doria.

Baada ya majina kuitishwa, Sgt. Beck alimwendea Newman na kusema, "Afande, ninaweza kuongea na wewe kama Mkristo na Mkristo mwenzie, siyo kama sajenti kwa kapteni?"

"Ndiyo," Newman alijibu.

Sgt. Beck alisema, "Afande, umeita majina ya watu ambao sio Wakristo kuongoza doria hii, na unajua kwamba watu hawa watauawa na hawatarudi tena kutoka kwenye doria hii. Kwa hiyo, mtu huyu ataishi milele yote jehanamu. Nimekuwa nikimshuhudia mtu huyu, na yuko karibu kabisa kumpokea Kristo kama Bwana na Mwokozi wake binafsi. Tafadhali usimpeleke mtu huyu kwenye doria hii."

New man alisema, "Samahani, siwezi kutuma mtoto wa mama mwingine badala yake. Sajenti, unajua kwamba tunatumia mfumo wa mzunguko katika kuwatuma watu kwenye doria na wakati jina lako linapofikia, ni lazima uende."

Sgt. Beck akasema, "Lakini afande, mtu huyu ataishi milele jehanamu."

"Samahani, lakini sina uchaguzi," Newman alisema kwa msisitizo.

"Ndiyo, unao," Sgt. Beck alijibu. "Afande, ninajitolea kuchukua nafasi yake kuongoza doria."

Newman alimwambia Sgt. Beck kwamba atapaswa kufikiria juu ya pendekezo lake. Kamwe hakuwahi kukabiliana na Mkristo kama Sgt. Beck, kwa hiyo alikwenda nje nyuma ya hema lake, akapiga magoti, na kumwomba Mungu nini cha kufanya. Kisha Newman akarudi na kumwambia Sgt. Beck kwamba atamruhusu kuchukua nafasi ya yule mtu mwingine.

Usiku ule doria iliondoka. Miale ya adui iliangaza angani wakati watu wale walipofika katikati ya mto. Maji yalikuwa yamefikia vifuani wakati bunduki za rashasha zilipoanza kufyatuliwa.

Muda mfupi baada ya hapo, amri ilikuja kutoka makao makuu kwamba Newman alitakiwa kuongoza kombania yake kuwashambulia maadui. Newman alipiga simu makao makuu na kusema kwamba hawezi kushambulia kwa sababu baadhi ya watu wake walikuwa kwenye doria kati ya kombania yake na maadui. Makao makuu walimjibu tu, "Siyo uamuzi wako. Shambulia mara moja"

Newman alitii amri, na watu wake walipigana kwa siku tatu, usiku na mchana. Mara baada ya mapigano kusimama, Newman aliita majina. Alipoita jina la Sgt Beck hakukuwa na jibu. Aliita jina lake mara kadhaa, lakini maneno yake yalikutana na ukimya tu.

Hatimaye, askari mmoja wa Kimarekani akiwa na miguu iliyoganda kwa baridi, alisimama na kusema, "Afande, Sgt. Beck aliuawa na askari wa maadui chini ya mlima wa 317."

Baada ya kumaliza kuita majina, Newman alitoka na kuutafuta mwili wa Sgt Beck. Alichukua bunduki yake aina ya rifle, alichomeka singe yake ardhini, na kuweka kofia yake juu yake ili kwamba mwili wa Sgt Beck uweze kupatikana na kupata maziko ya heshima.

Newman baadaye alisema, "Sgt. Beck alikuwa mtu wangu wa kwanza kukutana naye Mkristo aliyejitoa kwa dhati, mtu ambaye hakuwa tu shahidi aliyejianda na kuwa tayari, bali mtu ambaye alikuwa tayari kutoa maisha yake ili kwamba mtu aliye dhambini aweze kupata nafasi nyingine ya kumpokewa Kristo kama Bwana na Mwokozi wake binafsi."

- Pia katika ukurasa 183, sehemu C.2, tunaona Mathayo 28:19 (NIV) ambako tumeelekezwa *"... kwenda na kuwafanya wanafunzi..."* **Kuwafanya wanafunzi kuna sehemu tano:**

  1. **Nenda au Kwenda**—Hatutakiwi kukaa na kimyakimya tukisubiri watu kutujia sisi. Tutakiwa kuwaendea, na tunatakiwa kwenda tukiwa na kusudi.

  2. **Kufanya Uinjilisti—Kuwaambia waliopotea habari njema kwamba** *"...Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu kama yanenavyo Maandiko na kwamba alizikwa, na kwamba alifufuliwa siku ya tatu kama yanenavyo maandiko"* (1 Wakorintho 15:3-4 NIV).

     - Na kisha eleza jinsi wanavyoweza kupata msamaha wa Mungu, uzima wa milele, mbinguni na Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi wao binafsi.

- Kuna mipango na programu nyingi zinazopatikana ili kuwasaidia watu kuwa na ufanisi zaidi katika kushuhudia habari za Kristo, na tunamhasisha kila mtu kupata mafunzo yoyote anayoweza kupata kuhusu ushuhudiaji, lakini ushuhudiaji siyo mgumu hivyo. Ni rahisi tu kumwambia mtu fulani kile unachokijua kuhusu Yule unayemjua, Yesu. Tathmini au hakiki "Jinsi gani tunaweza kuwa na ufanisi zaidi katika kushirikisha ujumbe Wake?" (Kurasa 41-42, sehemu VII)

    - Kushuhudia kunachukua ufahamu mpya wa umuhimu na uharaka pale tunapotambua kwamba wale wasio na Kristo hawana tumaini. *"... Wakiishi mbali na Kristo…Wamefarakana na Watu wa Mungu… pasipo Mungu na pasipo tumaini"* (Efeso 2:12 NLT).

- Mafunzo ya *Ushirika wa Mtu na Mungu* yametayarishwa kuwahamasisha na kuwatia moyo wanafunzi kujihusisha katika kuwa mashahidi walio hai kwa ajili ya Kristo.

3. **Kubatiza**—Ni wajibu wetu kuwasisitiza waamini hawa wapya umuhimu wa kubatizwa, mapema kadiri iwezekanavyo, kama tendo la utii kwa Bwana wetu. Kuzamisha ndani ya maji ni picha ya kufa, kuzikwa na kufufuka kwa Yesu. Ubatizo ni ushuhuda katika ukweli kwamba mtu huyu ameokolewa na anakuwa mfuasi mtiifu kwa Yesu.

4. **Fundisha**—Wafundishe na kuwaelekeza waamini jinsi ya kumjua Mungu, jinsi ya kuwa na uhusiano na ushirika wa kina na undani na Yeye, na jinsi ya kuupata uzima tele Yesu aliousema katika Yohana 10:10.

5. **Ongezeka/zidisha**—Kiroho zalisha wanafunzi ambao watafanya wanafunzi.

- Mafunzi ya *Ushirika wa mtu na Mungu* yametayarishwa kuwa nyenzo yenye “uwezo wa kupokezana” ambayo ni rahisi sana kuitumia na bado imejaa ukweli wenye kina kiasi kwamba mwamini wa kweli anaweza kuitumia kufanya wanafunzi. Ina ufanisi unaolingana katika kumfundisha Mkristo mpya kama ilivyo kwa watu ambao wamekuwa Wakristo kwa muda mrefu.

***Ukurasa 184, sehemu 5:***

- *“...muwe tayari siku zote kumjibu kila mtu awaulizaye habari za tumaini lilioo ndani yenu...”* 1 Petro 3:15 (NEB).
    - Tunapoelewa kwamba Biblia ni itifaki bora inayojitosheleza, tunajua kwamba mstari huu hausisistizi kwamba tunapaswa kukaa kimya katika nyumba zetu na kusubiri watu kuja kwetu ili kwamba tuweze kuwaambia habari za Yesu. Hii inaweza kutokea mara kwa mara, lakini maelekezo tuliyo nayo kutoka kwa Mungu ni **NENDA UKAWAAMBIE** (Mathayo 22:9, na 28:19; Marko 5:19; Luka 15:4-7; Yohana 15:16 na mingine mingi).
    - Kile tunachofundishwa katika 1Petro 3:15 ni kwamba tunapaswa siku zote kujiandaa kushirikisha kwa nini tunalo tumaini. Tunajiweka katika hali ya kupatikana kwa kwenda kwa wengine, na tunajaribu kutengeneza mazingira ambayo kupitia maswali yetu ambayo yatawahamasisha wasikilizaji wetu kuuliza habari za tumaini letu-au, angalau, kufunguka katika kushirikisha kwetu.

      ***Hadithi:*** Miaka kadhaa iliyopita tulikuwa na mkutano wa uamsho kanisani kwetu kwa juma moja. Nilikuwa nikitembelea baadhi ya nyumba katika eneo letu na kuwaalika watu katika huduma yetu. Niligonga kwenye mlango mmoja na japokuwa kioo kilikuwa kimefungwa, hakuna mtu aliyekuja mlangoni, kwa hiyo nikagonga tena. Nilisikia kama ghasia ndani na kisha nikasikia mtu akisema kwa sauti nzito ya kukwaruza, “Nini unataka?” Nilijitambulisha na kumwambia jina la kanisa langu na kwamba nimekuja tu kuwatembelea.

Alipofungua mlango, ilikuwa ni dhahiri kwamba alikuwa anakunywa. Nilizungumza naye kwa muda mfupi na kisha nikamwomba kama atapenda kwenda kwenye mkutano wa uamsho pamoja nami jioni inayofuata. Alitulia kwa muda kisha akasema, “Siwezi kwenda, nguo zangu ni chafu.”

“Nenda ukazilete”, nilisema, “nami nitazipeleka kwa dobi na kuzileta tena kwako kwa wakati ili uweze kwenda nami kesho usiku.”

Hili lilimshanga mtu huyu, na alionekana kuwa bado mtulivu zaidi. Alisema, “Utafanya hivyo?”

“Ndiyo,” Nilimwambia.

Kwa hiyo alifungua mlango na kunikaribisha niingie. Yeye na mimi tulirudi chumbani ambako alivuta sanduku la mbao lililochakaa, na akaanza kuangalia nguo zake. Hatimaye, alizipata na nilizichukua.

Jioni ile baada ya kufika nyumbani kutoka kwenye huduma ya uamsho, Mhudumu wetu wa Elimu alinipigia kuniuliza kama nilimjua mtu mmoja aliyeitwa “John”. Alikuwa ni mtu yule yule niliyemtembelea mapema jioni ile. Aliendelea kuniambia jinsi John alivyoingia kanisani kwetu baada ya ibada na kusema, “Ninataka kuokoka.” Mwinjilisti, Eddie Martini, alimchukua John kwenda katika chumba cha mchungaji cha kusomea na alimwelezea jinsi ya kuwa Mkristo. John aliomba kumpokea Kristo. Nilifurahi sana.

Nikiwa na nguo safi za John mkononi, nilikwenda kumchukua kwa ajili ya huduma ya jioni inayofuata. Kulikuwa na ujumbe kwenye kioo cha mlango uliosema kwamba, “Acha nguo zangu. Siwezi kwenda.” Kioo cha mbele kilikuwa kimefungwa, kwa hiyo niliendelea kugonga mpaka hatimaye John alikuja mlangoni. Alijisikia aibu sana. Mmoja wa marafiki zake alimtembelea mchana na kumpa kinywaji, na John alikunywa.

Nilimchukua kwenda naye kupata kahawa kidogo, na ama usiku ule au usiku uliofuata John alikwenda nami kwenye huduma ya uamsho kwa kusudi la kufanya uamuzi wake hadharani. Mara mwaliko ulipoanza, niliomba, “Bwana, sijui kama uamuzi wa

John ni kweli au la, kwa hiyo kama ulikuwa ni wa kweli na unamtaka kwenda mbele wakati wa mwaliko, mfanye aniombe wakati wa kwenda mbele.

Nikiwa hata sijamaliza kuomba John alikuwa amesimama pembeni yangu na kusema, "Je. Tunakwenda sasa?"

"John," Nilisema. "unataka kila mtu ndani ya kanisa hili kujua kwamba umemwamini Kristo kama Bwana na Mwokozi wako Binafsi?

John alinitazama kuanzia chini hadi juu na akasema, "Hii ndiyo sababu nilikuja, ama siyo?

"Ndiyo John," Nilimwambia. "Hii ndiyo sababu ulikuja."

Tukauitikia mwaliko ili kwamba John aweze kufanya uamuzi wake hadharani. John alibatizwa kuonyesha kwamba alikuwa mfuasi wa Yesu, na muda mfupi baadaye akawa mtunzaji wa kanisa letu. Hizo ndizo zilikuwa siku za furaha zaidi katika maisha ya John. Alifariki miaka michache baada ya kuokoka, inawezekana kutokana na unywaji wa miaka mingi, japokuwa alikuwa kwenye umri wa miaka arobaini hivi. Inafurahisha kwangu kujua kwamba siku moja nitamwona John mbinguni.

- **Kwa nini ninawasimulia hadithi hii ndefu?**
    - **Kuna watu wengi kama John ambao hawatakuja mpaka tunapokwenda kuwaalika.**
    - **Wakati mwingine tunaweza kuchukua nguo chafu na zilizochakaa kuzifua kuonyesha kwamba tunajali.**
    - **Kama hatuonyeshi upendo wetu kwa John na wengine kama yeye kupitia ushuhudiaji, nani atafanya?**
    - **Je, si kila mtu anastahili fursa ya kumjua Yesu kama Bwana na Mwokozi wake binafsi?**

***Hadithi:*** Siku moja nilipokuwa nawatembelea watu waliopotea ambao hawakuwa wakijihu-

sisha na kanisa katika eneo letu, mwanamme mmoja aliniambia, baada ya kuwa ameomba kumpokea Yesu, “Nashukuru sana! Nilikuwa nikitarajia kwamba siku moja mtu fulani atakuja kuniambia zaidi juu ya Yesu.”

***Ukurasa 185:***

- Je, wakati gani tunayajaza maisha yetu na upendo kwa ajili ya Wakristo wenzetu na waliopotea na kisha kuuonyesha upendo huo kwa ajili yao?
    - Jibu = LEO!
- Jinsi gani tunaweza kuyajaza maisha yetu na upendo kwa ajili ya Wakristo wenzetu na waliopotea na kisha kwa uaminifu kuuonyesha upendo huo kwao?
    - Jibu = KUJIACHILIA KATIKA UDHIBITI WA ROHO MTAKATIFU! Pale anapokuwa katika udhibiti, anaweza kuakisi upendo Wake kupitia sisi.

7. Ligawe kundi katika jozi (wavulana kwa wavulana na wasichana kwa wasichana). Mtake kila mmoja kushirikisha kisha **KKK** yafuatayo wakati mshirika wake mwenza anamsikiliza:

    a. **Mistari iliyokaririwa** juma hili lililopita:

    - Luka 9:23 • Warumi 6:13 • Yohana 15:4

    b. **Jumbe za JKSKB** (Kurasa 65-72) zilizotengenezwa juma hili lililopita.

    - Wahamasishe wanafunzi kuwa mawakili wema wa muda na si kuzungumza habari za kitu kingine chochote. Huu ni muda wa kufanyia mazoezi na kukua katika nidhamu ya kutafakari.

8. Warudishe wanafunzi tena kwenye kundi kubwa na watake kuweka mistari ifuatayo kwenye kadi za mistari (ukurasa 235):

- **2 Timotheo 3:16-17** • **Waebrania 4:12**

***Muhimu:***

- Kumbuka kwamba kushika mistari hiyo kunaiingiza katika akili zetu. Kutafakari kunaihamisha kwenda kwenye mioyo yetu. Kwa hiyo, tunashika mistari mapema iwezekanavyo katika juma ili kutupa muda zaidi wa kuitafakari kabla hatujakutana tena. Kwa nini tutafakari maandiko? Tunataka Mungu kuitumia mistari katika maisha yetu kutubadilisha katika mfano wake.

  *Kushika na kutafakari maandiko kunatusaidia kumjua Mungu.*

9. Wahamasishe wanafunzi kuonyesha upendo wao kwa Mungu mara tatu kila saa wanayokuwa macho juma hili *"Ninakupenda, Ee Bwana, Nguvu zangu"* (Zaburi 18:1 NIV).

   - Tunataka kuendelea kufanyia mazoezi mpaka inapokuwa kawaida, sehemu ya maisha yetu kwa asili.

10. Wahamasishe wanafunzi kutafuta fursa za kushirikisha kile ambacho Mungu anawafundisha.

    ***Maelezo:*** Tunataka kuwasaidia wanafunzi kuwa na utulivu wanapongea juu ya Yesu katika kila eneo la maisha yao.

11. Tafuta kupata usikivu wa wanafunzi katika **Kazi** zao **za Ziada** (Kurasa 267-268).

    ***Soma darasani:*** Ruhusu muda wa kusoma ukurasa 267 kwa sauti darasani na hakikisha kwamba kila mmoja anaielewa kazi ya ziada.

    ***Wahamasishe wanafunzi*** kukutana na Mungu mapema kila asubuhi katika muda wao wa utulivu.

    > ***...Ee Mungu, Mungu wangu, Nitakutafuta kwa bidii asubuhi mapema...*** (Zaburi 63:1). (*Strong's Exhaustive Concordance of the Bible*, "Hebrew and Chaldee Dictionary," Ukurasa 114, namba 7836)

12. Funga kwa Maombi.

    ***Mfano:*** Waalike wanafunzi kuungana nawe kupiga magoti mnapoomba pamoja na kumshukuru Mungu kwa kukutana nanyi na kipekee kuzungumza na kila mmoja wenu.

## Mwongozo wa Kiongozi na Ujumbe wa Mwandishi......................Kipindi cha 15

1. Anza kwa maombi.

    ***Mfano:*** Waalike wanafunzi kupiga magoti pamoja nawe mnapoomba pamoja na kuukabidhi muda kwa Mungu.

2. Chukua karatasi ya **Ufuatiliaji** ya leo (Ukurasa 286).

3. Jadili swali lifuatalo: **Kwa nini tunapaswa kuwekeza maisha yetu katika mafunzo ya uanafunzi?**

    ***Wahamasishe au watie Moyo:*** Wasaidie wanafunzi kuona thamani ya kuwekeza maisha yao katika kumruhusu Mungu kuzalisha walimu wa wanafunzi kupitia wao kwa sababu:

    1. **Ni amri ya Yesu** kwamba *"Tuende kuwafanya wanafunzi"* **(**Mathayo 28:19 NIV).

    2. **Ndicho Yesu alichotuachia kuwa kielezo kwetu**, na tunatakiwa kuwa kama Yeye.

    3. **Tunaona hili likidhihirishwa katika maisha ya Paulo** kama alivyoufuata mfano wa Yesu katika kuwafanya wanafunzi. Paulo alimfundisha Timotheo, kisha akamhamasisha Timotheo kufanya hivyo hivyo katika maisha ya wengine, ambao nao wangefanya hivyo katika maisha ya wengine, n.k. **"***Na mambo yale uliyoyasikia kwangu kati ya mashahidi wengi, uwakabidhi watu waaminifu watakaowafundisha na wengine pia"* (2 Timotheo 2:2 NKJV).

    4. **Kufanya wanafunzi ndio njia itakayowezesha kuzidisha huduma zetu** kwa sababu inalipa gawio kwa ajili ya umilele. Pale tunapofanya wanafunzi, tunakuwa watii na kulitimiza kusudi ambalo Mungu ametupatia uhai. Huduma hii aliyotupatia sisi itaendelea kuishi katika maisha ya wale watu waaminifu ambao tumewafundisha kadri wanavyoendelea kufanya wanafunzi. Ongezeko la kiroho linaendelea kupitia vizazi vingi hata baada ya kuwa tumesahauliwa. **Kama tutakuwa waaminifu kufanya**

**wanafunzi na Yesu akachelewesha ujio wake, kila mmoja wetu atawajibika, kupitia kanuni ya ongezeko la kiroho, kwa zaidi ya watu milioni moja kuokolewa na kufundishwa kabla ya kurudi kwake**.

***Maelezo:*** Kielelezo kifuatacho kinaonyesha nini kingetokea kama tungewekeza maisha yetu katika kufanya wanafunzi kama Yesu alivyotufundisha. Ni mpango wa Mungu na njia ya haraka ya kuufikia ulimwengu kwa ajili ya Kristo.

***Dhana:***

1. Mpango kwa ajili ya kufanya wanafunzi ambao Yesu aliutambulisha kwetu una dhana kwamba mwamini wa kweli, mwanafunzi, atakuwa mtii kwa Yesu na kufanya wanafunzi.

2. Kwa kielelezo hiki tutadhania kwamba kila mtu aliyefundishwa anaendelea kuwafundisha wanfaunzi wawili kwa mwaka mpaka kila mmoja katika ulimwengu amefundishwa (amekuwa mwanafunzi).

***Swali:*** **Ni wa jinsi gani ni kwa muhimu kumtii Yesu?**

Ikiwa tutaanza na Mkristo mmoja tu leo, itachukua muda gani kwa kila mtu ulimwenguni—makadirio ya watu bilioni 7.28 kufikia mwaka 2014—kupata fursa ya kumpokea Yesu kama Bwana na Mwokozi na kisha kufundishwa, kuandaliwa kuishi katika maisha ya ushindi kama Wakristo, na kufundishwa kufanya wanafunzi wanaofanya wanafunzi?

***Jibu:*** Itachukua chini ya miaka 16.5. Lakini kwa sababu kutokutii amri ya Yesu ya kwenda na kufanya wanafunzi, Zaidi ya theluthi mbili ya watu ulimwenguni wanabakia bila kuokolewa, na mamilioni hawajawahi kusikia habari za Yesu.

*Mwonekano :*

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Sasa** | 1 | **(Wewe)** | |
| Mwaka | .5 | Wanafunzi | 2 |
| Mwaka | 1 | Wanafunzi | 4 |
| Mwaka | 1.5 | Wanafunzi | 8 |
| Mwaka | 2 | Wanafunzi | 16 |
| Mwaka | 2.5 | Wanafunzi | 32 |
| Mwaka | 3 | Wanafunzi | 64 |
| Mwaka | 3.5 | Wanafunzi | 128 |
| Mwaka | 4 | Wanafunzi | 256 |
| Mwaka | 4.5 | Wanafunzi | 512 |
| Mwaka | 5 | Wanafunzi | 1,024 |
| Mwaka | 5.5 | Wanafunzi | 2,048 |
| Mwaka | 6 | Wanafunzi | 4,096 |
| Mwaka | 6.5 | Wanafunzi | 8,192 |
| Mwaka | 7 | Wanafunzi | 16,384 |
| Mwaka | 7.5 | Wanafunzi | 32,768 |
| Mwaka | 8 | Wanafunzi | 65,536 |
| Mwaka | 8.5 | Wanafunzi | 131,072 |
| Mwaka | 9 | Wanafunzi | 262,144 |
| Mwaka | 9.5 | Wanafunzi | 524,288 |
| Mwaka | 10 | Wanafunzi | 1,048,576 |
| Mwaka | 10.5 | Wanafunzi | 2,097,152 |
| Mwaka | 11 | Wanafunzi | 4,194,304 |
| Mwaka | 11.5 | Wanafunzi | 8,388,608 |
| Mwaka | 12 | Wanafunzi | 16,777,216 |
| Mwaka | 12.5 | Wanafunzi | 33,554,432 |
| Mwaka | 13 | Wanafunzi | 67,108,864 |
| Mwaka | 13.5 | Wanafunzi | 134,217,728 |
| Mwaka | 14 | Wanafunzi | 268,435,456 |
| Mwaka | 14.5 | Wanafunzi | 536,870,912 |
| Mwaka | 15 | Wanafunzi | 1,073,741,824 |
| Mwaka | 15.5 | Wanafunzi | 2,147,483,648 |
| Mwaka | 16 | Wanafunzi | 4,294,967,296 |
| Mwaka | 16.5 | Wanafunzi | 8,589,934,592 |
| Mwaka | 17 | Wanafunzi | 17,179,869,184 |

**Miitikio inayoweza kutolewa** katika maagizo ya Yesu kwetu ya kwenda kuwafanya wanafunzi:

1. Kila mtu haifanyi kazi yake, kwa hiyo kwa nini mimi nifanye?

2. Sina muda; hebu mtu mwingine aifanye.
3. Kuna gharama kubwa sana.
4. Tukiufafanua au kuuchambua mwitikio wa Isaya kwa Bwana, "Niko hapa Bwana. Nitume mimi, nitumie mimi, nirurusu tu nijihusishe katika jambo lolote ambalo ni kubwa kuliko mimi mwenyewe. Bwana, ninataka maisha yangu yawe na thamani kwa ajili yako" (Isaya 6:8).

4. Mwombe mtu mmoja kushirikisha kisha **K**ufikiria kwa kina, **K**uvuta taswira, na **K**uombea tena kwa Mungu **Notsi za Mahubiri au Somo lake** (Kurasa 21-24).

   ***Watie Moyo:*** Baada ya mmoja wa wanafunzi kushirikisha notsi za mahubiri na kisha kuutafakari kwa ajili ya darasa, watie moyo wanafunzi wote kuendelea na zoezi hili la kutengeneza notsi wakati wa mahubiri. Kusimamisha au kuacha zoezi hili kunaonyesha kwamba hatuelewi umuhimu wa kutafakari.

5. Jadili **Maswali ya Marudio ya Kazi ya Ziada** (Ukurasa 268).

   ***Maelezo:***

   - Tumia maswali ya 5, 6, na 7 katika ukurasa 268 kuwahamisisha wanafunzi kuzungumza kwa wengine juu ya Yesu na mambo anayofundisha.
   - Mruhusu mtu mmoja katika kundi asimulie kuhusu uzoefu wa juma lililopita wakati alipozungumza na mtu fulani kuhusu Yesu au kushirikisha jambo ambalo Mungu anamfundisha.

6. Soma/Jadili kwa kina somo la **Jinsi gani naweza kuyajaza maisha yangu na upendo kwa ajili ya wengine (Wakristo wenzangu na waliopotea)**? (Kurasa 187-191) Unaposoma na kujadili, mara kwa mara simama na kuwapa wanafunzi fursa ya **K**ufikira kwa kina, **K**uvuta taswira na **K**uomba**.**

***Kurasa 187-191:***

***Maelezo:*** "Kuwa na maisha yenye upendo wenye kiini cha Kristo kwa ajili yangu mwenyewe kama jinsi nilivyo" ni muhimu sana kwa sababu mara kwa mara Shetani anatushambulia. Mpango wake ni kutuharibu ama kwa kutufanya sisi tujisikie kiburi au kuwa makini kupita kiasi kuhusu udhaifu na hisia zetu.

- Tunaweza kupinga mashambulizi ya Shetani pale tunapokumbuka ahadi za Mungu na wema wake. Tunaweza kuhamisha kutoka kwenye kujihami kwenda kwenye kushambulia kwa kujizoeza Kanuni ya Kutumbukiza na Kuondoa (Kurasa 28-29)—kuendelea kuonyesha upendo kwa Mungu na kumshukuru Yeye kwa ajili ya ahadi zake nyingi kwetu katika mafunzo haya. Tunapofanya haya:
    - Tunaondoa mawazo hasi ya Shetani kutoka kwenye akili zetu kwa kutumbukiza mawazo ya kuabudu na kutoa shukrani kwa Mungu.
    - Tutaanza kujiangalia wenyewe katika mtazamo wa Mungu.
    - Tutaona jinsi Mungu anavyotuthamini.
    - Mtu mmoja alisema, "Nilikuwa na hali ya kutojiamini, lakini sasa ninatambua kwamba siyo tu hisia. Mimi ni mtu wa chini, kwa hiyo ninajiachilia tu katika udhibiti Wake na kushirikiana naye kadri anavyonibadilisha kuwa mtu anayetaka niwe."

***Watie Moyo:***

- Mtu unayemfundisha au mtu yeyote katika kikundi unachofundisha anaweza kuwa na hasira na Mungu kwa sababu ya namna alivyomuumba. Anaweza kujiangalia na kujiona kama mtu asiyevutia, au amemuweka au kukulia katika nyumba mbaya inayodhalilisha, au hakuonyeshwa upendo na heshima, au amekuwa na afya mbaya. Inawezekana hata hajui kwa nini ana hasira na Mungu.

- Mnapopitia mafunzo haya, mtake kila mmoja kutafakari kimyakimya kila mstari. Tulia kuruhusu wanafunzi mbalimbali kutafakari kwa nguvu kila mstari. Anaweza kuona muujiza anapo **F**ikiria kwa kina, **V**uta taswira, na **K**uombea kila moja ya mistari hii tena kwa Mungu kama maombi binafsi wakati wewe na wengine mnamsikiliza.
    - Ni vigumu kutafakari mistari hii na usione kwamba:
        - **Mungu anakupenda kwa kina.**
        - **Mungu ana mpango mkubwa kwa ajili ya maisha yako** bila kujali mazingira au mambo ya nyuma (yaliyopita).
            - **Bado hatujachelewa.** Tunaweza kuingia katika mpango wa Mungu kwa muda wetu wote wa maisha uliobakia, kuanzia leo.
            - **Maisha kwa Mkristo ni kuanzia hatua hii na kuendelea.** Maisha na Yesu ni safari. Chukua hatua inayofuata.
        - **Mungu anajali** na anajihusiha katika kila kipengele cha maisha yetu.
        - **Mungu ametupatia maisha kwa kusudi.** Tupo katika misheni kwa ajili ya Mungu wakati tunapokuwa hapa duniani.

7. Ruhusu kundi kugawanyika katika jozi (wavulana kwa wavulana na wasichana kwa wasichana). Mtake kila mmoja kushirikisha kisha **KKK** yafuatayo wakati mshirika wake mwenza akimsikiliza:

    a. **Mistari iliyokaririwa** juma hili lililopita:

    - 2 Timotheo 3:16-17 • Waebrania 4:12

    b. **NKSKB** (Kurasa 65-72) zilizotengenezwa juma lililopita.

- Wahamasishe wanafunzi kuwa mawakili wema wa muda huu na si kuzungumza juu ya jambo lingine lolote. Huu ni muda wa kujizoeza na kukua katika kanuni ya kutafakari.

8. Warudishe wanafunzi tena katika kundi kubwa na watake kuiweka mistari ifuatayo kwenye kadi ya mistari iliyokaririwa (Ukurasa 235):

   - **Isaya 41:10**
   - **Yeremia 29:11 (LIV)** **—angalia ukurasa 188**

   ***Watie Moyo:***

   - Waombe kukushirikisha jinsi walivyofaidika kutokana na kushika maandiko.
   - Waombe wanafunzi kuendelea kushika maandiko kwa muda wa maisha yao yote.

9. Jadili **Changamoto za Kila Siku katika Kujifunza Biblia Baada ya Kipindi cha 15** (Ukurasa 192).

   **Wahamasishe** wanafunzi kuendelea kujifunza Biblia wao wenyewe. Wahamasishe kujiwekea malengo na waende katika kiwango cha kasi yao wenyewe.

10. Jadili **Msaada katika Mafunzo Binafsi ya Biblia** (Ukurasa 193).

    ***Watie Moyo:*** Hakuna kitu kizuri kama kuchimbua Neno la Mungu (Kujifunza Biblia) na kugundua kanuni za thamani za kweli wewe mwenyewe.

11. Jadili **Njia za Kujifunza au kujisomea Biblia** (Kurasa 194-227):

    - Kwa Sura
    - Kwa vifungu
    - Kwa mistari
    - Kwa Vitabu
    - Kwa Maneno
    - Kwa mada au somo
    - Kupitia Wasifu au uzao

    ***Watie moyo:***

    - Mnapojadili mbinu au njia za hapo juu za Kujifunza Biblia darasani, wahamasishe wanafunzi kuanza mafunzo haya wao wenyewe na kuendelea kujifunza Neno

la Mungu kwa muda wao wote wa maisha uliobakia. Waambie:

- Asitarajie kujaza kila mstari katika mwongozo uliotolewa.
- Mwombe Mungu akusaidie, na kufanya kile unachoweza.
- Mwanzoni, fanya mafunzo ambayo ni rahisi kwako.
- Weka baadhi ya malengo na endelea kutokana na kasi yako.
- Kumbuka: Kusudi letu katika kufanya mafunzo ya Biblia ni kwamba tuweze kumjua Yesu zaidi kwa kina, kwa undani na kibinafsi.

12. Jadili Nyenzo za Msaada katika Kujifunza Biblia (Kurasa 228-232).

***Maelezo:***

- Katika kurasa hizi utapata taarifa juu ya:
    - Rasilimali za Bure Mafunzo ya Biblia katika mtandao
- Tumependekeza Wasambazaji wa Vitabu vya Kikrsto kwa sababu tunajua kwamba wakati mwingine wanauza vitabu kwa punguzo kubwa.

13. Wahamasishe wanafunzi kuonyesha upendo wao kwa Mungu mara tatu kila saa wanayokuwa macho juma hili: *"Ninakupenda, Ee Bwana, Nguvu zangu"* (Zaburi 18:1 NIV).

- Wahamasishe wanafunzi kuendelea kufanya mazoezi kwa muda wao wote wa maisha uliobakia.

14. Wahamasishe wanafunzi kutafuta fursa za kushirikisha kile ambacho Mungu anawafundisha.

***Maelezo:***

- Tunaweza kutaka kuwasaidia wanafunzi kuwa na utulivu katika kuzungumza juu ya Yesu katika kila eneo la maisha yao.

- Wahamaishe kufanyia mazoezi haya kwa kipindi chao chote cha maisha kilichobakia.

15. Hakiki **Kazi ya Ziada** ya Wanafunzi (Kurasa 269-271).

    ***Soma darasani:*** Ruhusu muda wa kusoma kurasa 269-270 kwa sauti darasani na hakikisha kwamba kila mmoja anaielewa kazi ya ziada.

    - Wahamasishe wanafunzi kuendelea kufanyia mazoezi mambo waliyojifunza majuma kumi na tano yaliyopita kwa kipindi chote cha maisha yao kilichobakia.
    - Wahamasishe kuwa waaminifu kwa Mungu kukutana Naye kila siku kwa ajili ya muda wao wa utulivu (ukimya) kwa kipindi chote cha maisha yao kilichobakia.
    - Jadili kipengele cha 9 kwenye ukurasa 270. kuona kama kundi lako liko tayari kukutana mara moja kwa mwezi kwa miezi saba ijayo kwa ajili ya uwajibikaji (ufuatiliaji) na kutiana moyo ninyi kwa ninyi.

16. Funga kwa Maombi.

    ***Hadithi ya mwisho:*** Mhuribi Hallock alizoea kusimulia hadithi ya tai ambao walijenga kiota chao na kulelea vifaranga vyao juu ya miamba midogo kwenye milima. Wakati vifaranga vilipokua kuweza kuruka, wazazi waliharibu tu viota. Ujumbe ulikuwa rahisi lakini ulio wazi (wa moja kwa moja). Ni wakati wa kuruka.

    - Tunatumaini kundi lako litaendelea kukutana mara moja kwa mwezi kwa miezi saba inayofuata. Tianeni moyo ninyi kwa ninyi na kuwajibishana kwa ajili ya nidhamu za kiroho mlizokuwa mkizifanyia mazoezi kwa majuma kumi na tanao yaliyopita. Wakati huo huo, tunatumaini mta. *"... kwenda na kufanya wanafunzi..."* Ni muda wa kuruka.

17. Mpe kila mtu kipande cha karatasi kilicho wazi na mtake kuandika na kukupa jibu kwa swali lifuatalo: **Je Jinsi gani Mungu alikukuta majuma kumi na tano yaliyopita na jinsi gani anakuona leo?**

***Maelezo:***

- Hii inampa mwanafunzi fursa ya kufikiri majuma kumi na tano nyuma juu ya kile Mungu amefanya katika maisha yao.
- Itakuwa baraka kwao na hamasa kwako.
- Kumbuka kwamba Mungu ndiye anayebadilisha maisha, na sisi ni wajumbe tu. Usikate tamaa kama mtu fulani anakataa ujumbe wako.
- Wape wanafunzi karatasi kuandika mawazo yao. Mara wanapomaliza, chukua karatasi.
- Itamhamasisha au kumtia moyo mtu ambaye umemfundishwa kama mnashirikishana naye shuhuda hizi.

# Ujumbe

Ili kuagiza nakala zaidi za

# USHIRIKA WA MTU *na* MUNGU

Tafadhali wasiliana nasi kwa anwani ifuatayo:

Go Face to Face International, Inc.
P.O. Box 447
Bethany, OK 73008-0447 USA

au

http://order.ONEonONEwithGOD.org

www.ONEonONEwithGOD.org